*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

## Kikao cha Nne – Tarehe 11 Aprili, 2022

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuna maswali kama kawaida yetu, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na swali la kwanza ni la Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 31

### Ukarabati wa Hospitali ya Wilaya ya Pangani

**MHE. MWANTUMU M. ZODO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa Hopsitali ya Wilaya ya Pangani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dokta Dugange majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshemiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa Hospitali kongwe 21 ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani. Aidha, kupitia mpango huo, kila hospitali kongwe imetengewa shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukarabati hospitali za Halmashauri ambazo miundombinu yake imechakaa ili kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini kote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, bado Hospitali ya Wilaya ya Pangani inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa vifaa kama vile *generator*, mashine ya kufulia na *ambulance*: Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inaondoa changamoto hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kupitia fedha za tozo, Kata ya Madanga tumepata shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya cha Kata ya Madanga: Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha inakwenda kukamilisha kituo hicho cha afya kwa haraka ili kuokoa maisha ya wananchi wa Kata ya Madanga, Kimang'a, Bushiri na Masaika?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Mheshemiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Hospitali hii ya Pangani ni chakavu, sambamba na hilo, ina vifaa tiba na vifaa kama mashine za kufulia chakavu na pia gari la wagonjwa ni chakavu sana. Naomba kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mwantumu Zodo kwa namna ambavyo anasemea wananchi wa Mkoa wa Tanga na Watanzania kwa ujumla, vile vile kwa namna ambavyo anashirikiana kwa karibu sana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Pangani, Mheshimiwa Jumaa Aweso, ambaye naye pia amekuwa anafuatilia sana kuhusiana na ujenzi na ukarabati wa Hospitali ya Halmashauri ya Pangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka huu wa fedha, Serikali imetenga fedha kwa ajili kununua magari 407 na kati ya hayo 195 ni magari ya wagonjwa na Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani itapata gari jipya la wagonjwa na kuondoa changamoto hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la vifaa tiba Serikali imeendelea kutenga fedha na tutahakikisha tunaenda kwa awamu kuboresha vifaa tiba katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kituo cha afya ambacho kimepata shilingi milioni 500, nimhakikishie kwamba kitakwenda kukamilishwa, kutafutiwa vifaa tiba na kuwekwa watumishi ili huduma za afya ziendelee kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kama ilivyo kwa hospitali kongwe, tuna vituo vya afya vikongwe na chakavu sana kama Kituo cha Afya cha Gungu kilichopo Korogwe. Ni lini Serikali italeta mkakati

wa ukarabati na kuboresha vituo vya afya vya siku nyingi na chakavu ili kuwapa huduma wananchi wetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshemiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnzava Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba Serikali imefanya tathmini ya vituo vya afya chakavu vyote nchini kote na mpango unandaliwa kuhakikisha vinakarabatiwa na vinakuwa bora kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya. Kwa hiyo, kituo hicho pia kitapewa kipaumbele. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mbunge wa Chemba.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Magari ya vituo vya afya vya Mrijo, kwa Mtoro na Makorongo yamechakaa kabisa na hayafanyi kazi. Naomba *commitment* ya Serikali sasa kama tunaweza kufanyiwa ukarabati au kama tunaweza kupata magari mapya. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshemiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza sana kwa kazi kubwa anayoifanya kwa wananchi wa Chemba. Nimhakikishie kwamba magari ya wagonjwa ambayo ni chakavu, Serikali inaweka mpango wa kutafuta magari mengine ya wagonjwa ili kuhakikishwa huduma za afya

zinaenda vizuri na tutatoa kipaumbele katika vituo vya afya ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Sillo.

Na. 32

**Ujenzi Kituo cha Afya Gidas**

**MHE. DANIEL B. SILLO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itasaidia ujenzi wa Wodi ya Mama na Mtoto na chumba cha kuhifadhia maiti katika Kituo cha Afya Gidas?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilipeleka shilingi bilioni 1.04 kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Babati Vijijini kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri, Kituo cha Afya, Nyumba ya Mtumishi na ukamilishaji wa zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uhitaji wa wodi ya mama na mtoto na chumba cha kuhifadhia maiti katika Kituo cha Afya Gidas.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo hiki kimeombewa fedha Hazina na ujenzi utaanza mara fedha zitakapotolewa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sillo.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. La kwanza: Kwa kuwa mahitaji ya wahudumu wa afya katika Kituo cha Afya Gidas ni 52 na waliopo sasa ni watano tu: Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wahudumu wa afya ili kuwasaidia wananchi hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Kwa kuwa kituo cha afya kiko mbali na hospitali ya wilaya: Je, Serikali ipo tayari kupeleka gari la kubebea wagonjwa ili kuwasaidia wananchi wetu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na upungufu wa wahudumu wa afya, Serikali inatambua upungufu wa wahudumu wa afya katika maeneo mbalimbali ya vituo vyetu vya huduma na ndio maana wiki iliyopita, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi alitoa taarifa katika Bunge lako kwamba Serikali imeweka mpango wa kutoa vibali na kuanza kutoa ajira; na katika ajira hizo watumishi wa sekta ya afya watakuwemo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafanya mkakati na mara watakapoajiriwa, tutahakikisha kituo hicho kinapata watumishi ili kuboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na gari la wagonjwa, kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu ya msingi, magari ya wagonjwa 195 yatanunuliwa katika mwaka huu wa fedha na yatapelekwa kwenye Halmashauri zote ikiwepo Halmashauri ya Babati Vijijini. Kwa hiyo, kituo hicho pia kitapata gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde, Mheshimiwa Jerry jiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Tabora Manispaa ina *population* kubwa ya watu zaidi ya 600,000; na pale Tabora Mjini kuna zahanati ambayo inazalisha watu 10 mpaka 20 kwa siku: Je, ni lini Serikali sasa itakuwa tayari ku-*upgrade* ile zahanati na kuwa kituo cha afya na kuiwekea wodi wa wazazi pamoja na *theatre? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munde, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafanya tathmini ya maeneo ambayo yana zahanati, lakini yana idadi kubwa ya wananchi na yana umbali mkubwa kutoka kituo cha afya au hospitali. Tutafanya tathmini kwenye zahanati hii aliyoisema ili tuone kama inakidhi vigezo iweze kupandishwa hadhi kuwa kituo cha afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jerry.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Hospitali ya Mama na Mtoto, Chanika ina upungufu wa *general wards* za wanaume, wanawake na watoto ili kukifanya kituo cha afya kitoke kwenye hadhi ya kituo cha afya kuwa hospitali: Je, ni lini Serikali itajenga wodi hizi ili kuweza kuwasogezea huduma karibu wananchi wa Kata za Zingiziwa, Chanika, Mkuyuni, Kongola na Pugu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Hospitali ya Mama na Mtoto ya Chanika ni hospitali ambayo inatoa huduma kwa akina mama lakini ina uhitaji wa wodi ya akina mama wajawazito na wodi ya watoto. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafanya tathmini na pia tunatafuta fedha kwa ajili kwenda kujenga wodi katika hospitali ile ya Chanika ili sasa iweze kuwa na miundombinu yote kwa ajili ya kulaza akina mama na mtoto. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kawawa atafuatiwa na Mheshimiwa Sima.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii nami niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sisi tuna vituo vya afya vya siku nyingi; Mkongo Gulioni, Mputa na Lusewa na havina vyumba vya upasuaji na wala Wodi ya Mama na Mtoto na vimechakaa sana: Je, Serikali inaweza kuwahakikishia wananchi wa Mkongo Gulioni, Mputa na Lusewa kama wapo katika *list* ya kukarabatiwa vituo vyao vya afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Natumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba vituo hivi vya afya na vilivyo vingi nchini ni vya zamani ni vituo ambavyo vina upungufu wa miundombinu hususan majengo ya upasuaji na wodi. Ndiyo maana katika jibu la msingi nimesema, tunafanya tathmini kwenye vituo vya afya vyote ambavyo vina upungufu mkubwa wa miundombinu hasa majengo ya upasuaji na wodi ili baadaye tutafute fedha kwa

ajili ya kuhakikisha majengo hayo yanajengwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo la Namtumbo na vituo vya afya ambavyo amevitaja, tutavipa vipaumbele.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sima, jiandae Mheshimiwa Matiko.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nataka kujua, ni lini Serikali italeta fedha katika Kituo cha Afya cha Kisaki ambacho kimejengwa kwa nguvu za wananchi na Kituo cha afya cha Mwaja ambacho kilipokea shilingi milioni 250 za mwanzo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mussa Sima, Mbunge wa Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza sana wananchi katika hicho kituo hicho cha afya ambao wamechangia nguvu zao na wanasubiri kuungwa mkono na Serikali. Niwahakikishie Serikali inatambua sana nguvu za wananchi na tutatafuta fedha, ikipatikana twende tukaunge mkono nguvu za wananchi kuhakikisha vituo vya afya vinakamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Hospitali ya Mji wa Tarime inakabiliwa na changamoto ya chumba cha kuhifadhi maiti kutokufanya kazi kwa takribani zaidi ya wiki tatu; na ukizingatia Hospitali ya Mji wa Tarime inahudumia zaidi ya Wilaya tatu, kwa maana hiyo, ina maana ina wagonjwa wengi, hivyo inakuwa na maiti nyingi ambazo zinahitajika kupelekwa Kituo cha Afya cha Sirari. Kwa sababu Halmashauri ya Mji wa Tarime haina fedha

za kuweza kukarabati chumba kile cha kuhifadhi maiti, Serikali haiweze kuchukua jambo hili kwa udharura na kupeleka fedha ili kunusuru adha ambayo wanaipata Halmashauri ya Mji wa Tarime? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la jengo la kuhifadhia maiti kutofanya kazi katika Hospitali ya Mji wa Tarime, naomba nipokee taarifa hiyo na tutaifanyia kazi kwa haraka iwezekanavyo ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma hiyo muhimu katika hospitali hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, kwa niaba yake, Mheshimiwa Asenga.

Na. 33

**Watumishi Waliosimamishwa Kazi Mwaka 2015 – 2020**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA K.n.y. MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza:-

Je, ni watumishi wangapi wamesimamishwa kazi tangu mwaka 2015 hadi 2022 ambao mashauri yao hayajaisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa nidhamu katika Utumishi wa Umma ni suala muhimu ambalo limeainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298; Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2003; Taratibu za Uendeshaji katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2003; Taratibu Bora za Nidhamu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2007 na Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2015 hadi mwaka 2022, idadi ya watumishi waliosimamishwa kazi katika Taasisi mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na Serikali Kuu ambao mashauri yao hayajahitimishwa ni watumishi 836. Watumishi hawa ni miongoni mwa watumishi 1,477 waliokuwa wamesimamishwa kazi kwa kukiuka sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayosimamia nidhamu katika Utumishi wa Umma. Mashauri haya yapo katika hatua mbalimbali za mamlaka za nidhamu ambazo ni waajiri mbalimbali na mamlaka za rufaa ambazo ni Tume ya Utumishi wa Umma, Tume ya Walimu na Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwakumbusha Waajiri/Mamlaka za Nidhamu kuongeza kasi ya kuhitimisha mashauri ya nidhamu yaliyopo kwa kuzingatia taratibu za uendeshaji wa mashauri ya kinidhamu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na changamoto kubwa kwa watumishi wa umma hasa hawa ambao mashauri yao yanaendelea kusikilizwa kwamba

yanachukua muda mrefu sana na hii inawanyima haki kama watumishi wa umma. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha haya mashauri yanakamilika kwa wakati? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Godwin Kunambi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotoa maelezo kwenye majibu yangu ya msingi, mashauri ambayo yapo, ya watumishi wanaotakiwa kuchukuliwa hatua za kinidhamu ni watumishi 1,477; mashauri yaliyokuwa kwenye Tume ya Utumishi wa Umma ni mashauri 598; na kati ya rufaa hizi ambazo zimetajwa kule Tume ya Utumishi wa Umma, rufaa 411 zina vielelezo vilivyokamilika; na rufaa 187 hazina vielelezo, kwa hiyo, zimerudishwa kwa waajiri na mamlaka za nidhamu ili ziweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kama nilivyoitoa awali, ni kwamba hawa ambao wanapeleka mashauri Tume ya Utumishi wa Umma hayana vielelezo, yaweze kuwa yamewasilishwa na vielelezo kamili ili haki ya watumishi ambao Mheshimiwa Kunambi ameizungumzia hapa, iweze kupatikana kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi huwa inatokea kwamba mashauri haya...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ameshakuelewa vizuri tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Noah.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza Waziri swali la nyongeza kwamba kulikuwa na watumishi wa Darasa la Saba ambao wamesimamishwa na walikuwa wamefanya kazi kwa muda mrefu na baadaye hawakupewa kiinua mgongo wala chcohote: Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu watumishi hawa ambao kwa kweli wametumikia pia Taifa kwa kipindi kirefu kwa ujuzi huo wa Darasa la Saba? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Noah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa darasa la saba walioajiriwa baada ya Mei, 2004 wale Serikali ilikwishatoa tamko na ilimradi wawe walikuwa hawakughushi nyaraka zao walipewa muda mpaka ifikapo Desemba, 2020 wawe wamejiendeleza na kuweza kuendelea na ajira zao na wale ambao hawakujiendeleza, tayari mamlaka ilishatoa tamko kwamba wale washughulikiwe walipwe michango yao ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hadi kufikia Desemba, 2020 jumla ya watumishi 1,191 walikuwa hawakujiendeleza na hivyo wanastahili kulipwa michango yao ya hifadhi ya jamii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mwita Waitara.

Na. 34

**Hitaji la Maji Ziwa Victoria – Tarime**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, ni lini maji kutoka Ziwa Victoria yatafika katika Mji wa Tarime, Sirari, Nyamwaga na Nyamongo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama na yenye kutosheleza. Katika mipango ya muda mfupi ya kupunguza kero ya uhaba wa maji katika Wilaya ya Tarime, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imekamilisha Miradi ya Maji ya Sirari na Nyamwaga na inaendelea kutekeleza Miradi ya Nyangoto (Nyamongo), Sabasaba na Gimenya (Mjini Tarime). Miradi hiyo inatarajia kukamilika mwezi Juni, 2022 ambapo hali ya huduma ya maji katika Mji wa Tarime itaimarika kutoka asilimia 45 hadi asilimia 56 na maeneo mengine ya Wilaya ya Tarime kutoka asilimia 70 hadi asilimia 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa muda mrefu, Wilaya ya Tarime itanufaika na Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28 ambapo chanzo cha maji cha Ziwa Victoria kitatumika. Kupitia Mradi huo Miji ya Tarime, Sirari, Nyamwaga na Nyamongo na maeneo mengine ya Wilaya ya Tarime yatanufaika na lengo la asilimia 85 vijijini na 95 mijini litafanikiwa ifikapo mwaka 2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nikiri kwamba Wizara ya Maji imetutendea haki Tarime angalau hali ya maji imeboreshwa. Nisipompongeza Mheshimiwa Waziri Aweso na Naibu wake

itakuwa sijawatendea haki. Pamoja na kazi nzuri ambayo imefanyika naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kwamba pale Sirari kuna mradi wa maji ambao tathmini ilifanyika ya kwanza ilikuwa shilingi 1,200,000,000, lakini tukarudia tathmini tukapata shilingi 534,000,000, sasa mradi unaendelea vizuri, imebaki shilingi 70,000,000 tu ili mradi ukamilike. Naomba nijue ni lini Serikali itapeleka fedha hizo pale mradi ukamilike Sirari ambapo ina wapigakura zaidi ya 17,000 ambao ndio ushindi wangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ningependa tu nijue kwamba ni lini sasa huu Mradi wa Ziwa Victoria utaanza kwa sababu hili ni swali muhimu sana kwa Mbunge wa Tarime Vijijini, Sirari, Nyamongo na Nyamwaga lini mwaka wa fedha huu, mwaka wa fedha ujao au upi, ni lini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nipende kupokea shukrani kwa namna ambavyo tunaendelea na kazi mbalimbali kwenye miradi mingi kote nchini lakini hususan kwenye Jimbo la Tarime Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ambao bado tu milioni 60 upo kwenye mchakato na mgao ujao kwa maana ya mwezi huu wa tano tutahakikisha tunawaletea hii milioni 60 ili mradi ukamilike, lengo ni kuona maji yanatoka bombani na tunawatua akinamama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, miji 28 tunatarajia kuanza kutekeleza hivi karibuni, tayari kile kipingamizi ambacho kilikaa kwa muda mrefu kimekwisha. Kipekee nipende kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais mama

Samia Suluhu Hassan kwa sababu ameingilia kati na sasa hivi tunakwenda vizuri, ni mfupa wa muda mrefu, lakini mama Samia ameweza kuutafuna, tunakwenda kuanza kazi katika miji 28.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Oliver, jiandae Aida.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Wilaya ya Ngara ina vyanzo vikuu vya maji ambavyo ni Mto Ruvugu na Mto Kagera. Pamoja na uwepo wa vyanzo hivi tatizo la maji katika Wilaya ya Ngara limekuwa ni kubwa mno.

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga mradi mkubwa unaotosheleza wananchi wa Wilaya Ngara? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, kutoa Mkoa wa Kagera kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ngara ni moja ya wilaya ambayo tumeipa jicho la kipekee kabisa kuona kwamba tunaenda kutatua changamoto za maji. Niseme tayari tuna miradi ambayo ipo kwenye utekelezaji, lakini tuna miradi ambayo tutaendelea nayo hivyo tatizo la maji linakwenda kukoma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Miradi ya Maji ya Wilaya ya Nkasi imekuwa ikusuasua sana pamoja na Mradi wa Namenyere ambao Waziri aliahidi ndani ya Bunge kwamba utakamilika mwezi Desemba mwaka jana, mpaka leo mwezi wa Nne mradi huo haujaweza

kuwanufaisha watu wa Wilaya ya Nkasi. Je, ni lini Serikali itaondokana na fikra za kutumia mabwawa badala ya kutumia Ziwa Tanganyika ambapo ni kilomita 64 tu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi ni lini.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nkasi, kama alivyouliza…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ukirudia alichokisema utakuwa unachukua muda zaidi, wewe mpige tu moja kwa moja

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kadiri tutakavyopata fedha tutakwenda kutumia Ziwa Tanganyika kukamilisha miradi ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hayo ndio majibu sahihi, hongera sana. Mheshimiwa Kakoso, jiandae Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Mkoa wa Katavi una miradi mingi midogomidogo ambayo imeletwa na Serikali na tunaipongeza, lakini mwarobaini wa Mkoa wa Katavi kuepukana na miradi hiyo midogomidogo ni kuleta Mradi wa Maji wa kutoka Ziwa Tanganyika kuleta makao makuu, je, ni lini mradi huu utaanza kufanyiwa kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Katavi ni moja ya eneo ambalo litakwenda kunufaika na maji kutoka Ziwa

Tanganyika kama nilivyojibu kwa Mbunge wa Nkasi, tutakapopata fedha hii ni miradi yetu ya kimkakati tutakwenda kutekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Ni lini bonde la Maji la Mitema ambalo lipo Jimbo la Newala Vijijini ambalo lina maji ya kutosha litafanyiwa kazi ipasavyo ili wananchi wa Newala, Tandahimba na Nanyamba waweze kupata maji ya uhakika kwa sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna, Mbunge wa Jimbo la Newala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikoa ya kusini tunakwenda kuinufaisha na miradi yetu mikubwa ya Mto Ruvuma pamoja na maeneo yote ambayo yanatupatia maji ya kutosha. Hivyo bonde la maji la Mto Mitema nalo lipo kwenye mikakati yetu na kuona kwamba maeneo yote ya Newala tunakwenda kuondokana na maji ya kuokota na maji aina zote ambayo hayafai kwa matumizi ya wanadamu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ishengoma jiandae Shekilindi, jiandae Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mji Mdogo wa Gairo ni mji ambao una matatizo ya maji, sasa naomba kujua Mradi wa Maji wa kutoka kwenye Milima ya Nongwe ni lini utakamilika ili wananchi wa Gairo waweze kupata maji ya kutosha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Morogoro, Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Maji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii anayoiongolea uendelevu wake unatokana na mapato ya fedha, kwa hiyo kadri tutakavyoendelea kupata fedha, namna ambavyo tumekuwa tukipeleka fedha nyingi sana kwenye maeneo yote, tutapeleka fedha kwani na Gairo pia tunatamani waondokane na tatizo la maji.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Shekilindi, jiandae Mheshimiwa Kilave.

**MHE. SHABAN O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Takribani miaka sita sasa imepita katika Kata ya Kwai iliahidiwa na Serikali mradi wa maji lakini mpaka sasa mradi ule hakuna chochote kilichofanyika. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji katika Kata ya Kwai ili wananchi waondokane na adha hii wanayoendelea kuipata sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kata zake nyingi katika jimbo tumeshazishughulikia, hivyo hata kata hii ipo katika mkakati wa kuona kwamba na wao wanaenda kupata maji safi na salama ya kutosha. Tukishindwa kukamilisha ndani ya mwaka huu wa fedha basi mwaka ujao wa fedha tutahakikisha hii kata nayo inakwenda kunufaika na kumtua mama ndoo kichwani.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali langu, ni lini sasa kituo cha afya kinachoitwa Malawi kilichopo Yombo Vituka kitapata maji? Tumepata vifaa vizuri sana vya ndani ya hospitali lakini maji tunayotumia ni ya visima, leo na tuko mjini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilave, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoa huduma ya maji katika maeneo kama ya hospitali, shule ni moja ya vipaumbele vyetu.

Kwa hiyo maeneo haya ambayo bado yanatumia maji ya visima tunatoa kipaumbele na tutahakikisha kwenye kituo cha afya tutapeleka maji safi na salama bombani kwa lengo la kuona kwamba wanaendelea kuishi kwenye karne ya mama Samia kwa sababu Serikali ya Mama Samia imeweza kutoa fedha nyingi kwenye miradi ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Neema Mgaya.

Na. 35

**Mradi wa Maji Igando-Kijombe Wanging'ombe**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji Igando - Kijombe ili kupunguza changamoto ya maji Jimbo la Wanging'ombe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe ni wastani wa asilimia 76. Katika kuboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Wanging'ombe, Serikali inatekeleza Mradi wa Maji ya Mtiririko wa Igando – Kijombe ambao utahudumia wakazi wapatao 14,377 katika vijiji 10 vya Malangali, Igando, Mpanga, Luduga, Mayale, Kijombe, Wangamiko, Hanjawanu, Iyayi na Lyadebwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo unahusisha ujenzi wa chanzo cha maji, chujio, ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilometa 28.9 na mabomba ya usambazaji yenye urefu wa kilometa 18.2; ujenzi wa matenki mawili ya kuhifadhia maji yenye ujazo wa lita 150,000 na lita 100,000, vituo vya kuchotea maji 22 na mabirika mawili ya kunyweshea mifugo (*cattle trough*). Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 70 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2022 na kuboresha huduma ya maji kutoka asilimia 76 ya sasa na kufikia asilimia 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi iliyoainishwa katika mpango wa kuhakikisha lengo la kufikisha huduma ya maji vijijini ni asilimia 85 na asilimia 95 mijini ifikapo mwaka 2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante Mradi wa Maji Matamba - Kinyika wenye thamani ya bilioni mbili ndani ya miaka minne sasa Wilaya ya Makete bado haujakamilika. Naomba kujua, je, ni lini Serikali itasambaza mabomba pamoja na kujenga ofisi ili wananchi wa Wilaya ya Makete waweze kupata maji kwa uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nipende kumpongeza Mheshimiwa Neema kwa ufuatiliaji mzuri wa miradi mbalimbali katika Mkoa wa Njombe. Kwa upande wa Makete nilifika huko na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo tulitembelea miradi hii yote na mradi huu ni kipaumbele cha Wizara kwa sababu unakwenda kuhudumia wananchi wengi na lengo la Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kuona maji yanapatikana katika maeneo yote. Maeneo ambayo muda mrefu hayajapata nayo yanakwenda kupata, hivyo hivi karibuni tutaendelea na utekelezaji wa mradi huu ili kuona kwamba maji yanapatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. EMMANUL BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza niishukuru Serikali kwa juhudi za kuendelea kuwapatia maji wananchi wa Jimbo la Kyelwa lakini tunao mradi wa Kyelwa, Nyaruzumbura, Nyakatuntu mpaka Kamuli, mradi huu tumeupitisha kwenye bajeti iliyopita lakini mpaka sasa mradi huu haujaanza, je, ni lini utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge wa Jimbo la Kyelwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii yote ambayo mtaji wake ni ukubwa bado tunaendelea kuona kwamba tunapata fedha na kwenda kuitekeleza. Hivyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge Bilakwate tunakwenda kuutekeleza huu mradi na si kwa kuona kwamba tunatekeleza tu wajibu wetu, bali tunazingatia pia uhai kwa sababu maji ni uhai.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naipongeza Wizara ya Maji kwa miradi inayotekelezwa ndani ya Jimbo la Mkenge Wilaya Misenyi, lakini miradi hiyo ya Igayaza, Byamte, Baishozi, Rutunga na Lwamachi Nakitobo imesimama kwa sababu ya kasi ndogo ya wakandarasi kwa kukosa fedha ambapo wameshaomba *certificate* Wizara ya Maji. Je, ni lini sasa wakandarasi hawa watalipwa ili miradi iweze kukamilika kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kyombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari wiki iliyopita tumeanza kulipa wakandarasi, hivyo huenda na mkandarasi huyo akawemo ndani ya ile listi na tunaendelea kulipa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asanye Mradi wa Matamba Kinyika ni mradi ambao ulikuwa unatekelezwa kwa bilioni nne lakini Mheshimiwa Waziri Aweso amepambana hadi umetekelezwa kwa bilioni mbili, lakini mradi huu una miaka minne na hadi sasa haujakamilika. Wananchi wa Kitongoji cha Itani, Mlondwe, Ngonde na Nungu bado wanahangaika na maji kupitia mradi huu. Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi huu ili wananchi wao wapate maji ya uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipokee shukrani, salamu za pongezi kwa niaba ya Waziri. Mradi huu kama

alivyosema kwa jitihada za Mheshimiwa Waziri ameweza kuona kwamba ameupunguza na sasa hivi tutaendelea kuleta fedha ili kuona kwamba tunaenda kuukamilisha hivi punde, kama si ndani ya mwaka huu wa fedha kufika Juni, kabla ya mwaka 2022 kwisha tutahakikisha kwamba tunakuja kufanya kazi kwa sehemu kubwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Hongera sana, sasa kapumzike. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

Na. 36

**Vyuo Vikuu Kuajiri Watumishi Wake**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza: -

Je, ni Vyuo Vikuu vingapi vimepewa fursa ya kuajiri watumishi wake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo Vikuu kama zilivyo taasisi nyingine za Umma huajiri watumishi baada ya kupata vibali vya ajira kutoka Wizara yenye dhamana na Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumla ya Vyuo Vikuu vya Umma 13 kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita (2018-2019

mpaka 2020/2021) vilipata vibali vya kuajiri watumishi 618 ambapo wanataaluma ni 333 na waendeshaji ni 285.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na fursa hizo za kuajiri watumishi zilizotolewa, bado Serikali inaendelea na taratibu za kuwahamisha watumishi wenye sifa kutoka sehemu mbalimbali kujiunga na utumishi katika Vyuo Vikuu. Aidha, Serikali itaendelea kutoa vibali vya ajira katika Vyuo Vikuu kwa lengo la kuviongezea fursa ya kuajiri watumishi kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu hayo ya Waziri, naomba kufahamu kuhusu wale Maprofesa na Madaktari 203 ambao walistaafu kwa sasa wako wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, sehemu ambayo nguvu zinaisha haziwezi kufanya kazi ni sehemu ya ubongo. Kwa hiyo ina maana kwamba mtu anaweza akafanya kazi hata akiwa na miaka 70 mpaka 75 kama tunavyoona baadhi ya maprofesa humu ndani. Sasa ni lini Serikali kama Waziri alivyoahidi mwaka jana, ni lini Serikali sasa itaruhusu hawa watumishi wanaostaafu kwa miaka 65 waendelee kubaki chuoni mpaka miaka 75?

**NAIBU SPIKA:** Swali la kwanza Mheshimiwa Waziri ni la takwimu huna haja ya kulijibu jibu la pili tu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ntara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Ntara kwa kufuatilia kwa karibu sana maendeleo pamoja na upatikanaji wa watumishi hasa Wahadhiri katika vyuo vyetu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni kweli kulingana na miongozo ya Utumishi wa Umma, wenzetu katika vyuo vikuu, Wahadhiri

wale pamoja na Maprofesa huwa wanastaafu wakifikia umri wa miaka 65, tofauti na maeneo mengine ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika kipindi cha miaka mitatu watumishi zaidi ya 203 walistaafu kwenye maeneo mbalimbali ya vyuo vyetu hapa nchini. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Ntara kwamba miongoni hawa watumishi 203 ambao wamestaafu basi watumishi karibu 103 walikuwa wamebakishwa vyuoni kwa mikataba maalum. Miongoni mwao walikuwa ni watumishi 98 ambao walikuwa ni Maprofesa na watumishi karibu watano walikuwa ni *Senior Lectures.*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante ameshakuelewa, Mheshimiwa Iddi Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Msalala ni miongoni mwa Halmashauri ambazo hazina Vyuo Vikuu na tayari kupitia mapato ya ndani tumetenga fedha kiasi cha Shilingi Milioni 212 kuanza ujenzi wa Chuo cha VETA. Sasa ni Serikali itatuongezea fedha ili tuweze kumaliza chuo hicho.?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali katika sera yetu tunahakikisha kwamba tunakwenda kuwa na Vyuo vya *VETA* katika kila Wilaya nchini, kwa kuanzia tulianza na Wilaya 29 na hivi sasa vyuo hivyo vinakwenda kumalizika pamoja na Mikoa Minne ambayo haikuwa na Vyuo vya *VETA*. Nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka wa fedha ujao, mambo mengi sana kulingana na upatikanaji wa bajeti vyuo hivi tutakwenda kujenga kwenye maeneo ambayo bado ujenzi haujafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mbunge Viti Maalum Dkt.

**MHE. DKT. PAULINE D. NAHATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Je, ni lini kutakuwa na usawa wa jinsia katika uongozi wa juu katika Vyuo vyetu Vikuu kwa sababu kwa sasa hivi katika Vyuo Vikuu hakuna usawa wa jinsia kwa uongozi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kuhusu suala la jinsia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Dkt. Nahato kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuna changamoto sana kwenye usawa wa jinsia kwenye *level* hiyo ya Vyuo Vikuu na hii ni kutokana tu kwamba wakati tunaendelea na masuala haya ya kusoma, wenzetu hawa wa jinsia ya kike huwa wana *drop* sana. Lakini nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge jambo hili sasa tunaenda kulizingatia katika taratibu za sasa hivi utumishi maeneo haya ya jinsia yanazingatiwa sana hasa katika mradi wetu ule wa *HEET* ambao nilizungumza katika kipindi kilichopita, zaidi ya Wahadhiri zaidi ya 600 tunaenda kuwasomesha na miongoni mwao tutaweka ajenda maalum kabisa katika kuhakikisha kwamba jinsia inaweza kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu kapumzike. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Hasunga.

Na. 37

**Ujenzi wa Kiwango cha Lami kwa Barabara ya Mahenje - Ndolezi - Hasamba hadi Vwawa**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mahenje - Ndolezi - Hasamba hadi Vwawa ambayo ni muhimu kwa utalii wa Kimondo cha Mbozi na usafirishaji wa mazao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Songwe inajenga kwa kiwango cha lami barabara hii kwa awamu. Hadi mwishoni mwa Machi, 2022 Kilometa 4.5 zimekamilika kujengwa kuanzia Mji wa Vwawa hadi Kijiji cha Mtambwe katika hospitali ya Mkoa wa Songwe. Aidha, ujenzi unaendelea kwa sehemu ya mita 800 na inatarajiwa ifikapo mwishoni mwa Mwezi Juni, 2022 ujenzi utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya barabara hii iliyobaki kilomita 26.56 kwa sasa inafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kampuni ya Mhandisi Mshauri *M/S Inter Consult Ltd* ya Dar es Salaam. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2022. Baada ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JOSEPHAT N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, eneo la Mlowo mpaka Vwawa kumekuwa na msongamano mkubwa sana wa magari na hasa malori ya mizigo yanayopitia pale Tunduma na kuelekea huku sehemu mbalimbali, na barabara hii ambayo tunaisema ya kuanzia Mahenje, Ndolezi, Hasamba inaweza ikangezewa upembuzi yakinifu katika eneo la Ilyika, kwenda kule Kilima Mpimbi mpaka hadi pale Iboya na ikawa ni *bypass*.

Je, Serikali iko tayari sasa kuongeza hicho kipande kilichobaki kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina na kuhakikisha kwamba inakuwa ni *bypass*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali pili, kwa kuwa sasa wanajenga hizo mita 800 mpaka hadi pale karibu na hospitali ya Mkoa wa Songwe.

Je, Serikali itakuwa tayari katika mwaka ujao wa bajeti huu ambao tunaujadili kutenga tena kiasi fulani cha fedha kwa ajili ya kujenga kutoka pale kwenda Hasamba mpaka Ndolezi kwenye kimondo ili kusudi watalii mbalimbali waweze kufika katika eneo la Kimondo?*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara ya kutoka Mlowo hadi Tunduma kumekuwa na msongamano mkubwa wa magari. Kama nilivyosema

kwenye jibu langu la msingi, tunafanya usanifu kuanzia Mahenje, Hasamba hadi Vwawa, sasa swali alilolitoa la kutoka Mahenje Vwawa na kufanya *bypass* hadi Iboya ni barabara ambayo kimsingi kwa sasa haiku chini ya *TANROAD* lakini wazo hilo kwa maana ya kupunguza msongamano kupita Wilaya ya Vwawa, Serikali imelichukua na italiangalia namna ya kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoisema ya kuendeleza ni utaratibu wa kuendelea na ndiyo maana tumesema tutakwenda kwa awamu. Kwa hiyo, tunauhakika kwamba katika bajeti inayokuja, baada ya kukamilisha hizo mita 800 tutaendelea na lengo ikiwa ni kukamilisha barabara zima ambayo sasa tunafanyia usanifu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokololo.

**MHE. AGNES E. HOKOLOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami, barabara inayounganisha Mkoa wa Lindi na Mtwara, RuangWa – Nachingwea - Masasi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hokororo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mpango wa Serikali kuijenga barabara ya Masasi -Nachingwea kwa kiwango cha lami, lakini itaanza tu pale ambapo Serikali itakuwa imeshapata fedha kwani tayari usanifu wa kina ulishakimilika, kwa hiyo kinachosubiriwa ni upatikana wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Magige, jindae Mheshimiwa Shonza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ujenzi wa barabara ya Loliondo - Mto wa Umbu, kipande cha Wasso - Sale umeshakamilika kwa kiwango cha lami. Nilitaka kufahamu, je, ni lini Serikali itaanza awamu ya pili ya ujenzi huu ambao ni Sale-Ngarisero.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imekuwa kero sana kwa kazi wa Ngorongoro, hasa Tarafa ya Loliondo na Tarafa ya Sale. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri anapokuja kunijibu naomba anipe la uhakika na linaloeleweka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu, uhakika mtakwenda kantini mtaambizana vizuri. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Magige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya Mto wa Umbu, Loliondo, Sale, hadi Wasso, kipande cha Sale Wasso kimeshakamilika na kipande cha Loliondo kuja Ngarisero kiko kwenye mpango wa kujengwa. Lengo ni kukamilisha barabara yote ambayo ni muhimu sana siyo tu kwa wananchi wa Loliondo lakini kwa shughuli pia za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Shonza, jiandae Mheshimiwa Chaurembo na Mheshimiwa Mafuwe ajiandae.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya foleni pamoja na msongamano wa magari kuanzia eneo la Mpemba, Sogea mpaka unafika *Custom* Tunduma. Naomba kufahamu Serikali imejipangaje kutuondolea adha hiyo wananchi wa Mkoa wa Songwe kwa kutujengea barabara kutoka Mbozi, kwa maana ya pale Mlowo mpaka kufika Tunduma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ni sehemu tu ya barabara ya Igawa, Mbeya hadi Tunduma, maeneo yote haya yameshafanyiwa usanifu na yale maeneo ya Miji, barabara hizi zitajengwa njia nne ili kupunguza msongamano wa katika maeneo ya Miji ikiwemo na hilo eneo la kuanzia Vwawa kwenda sehemu ambapo tutajenga mizani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chaurembo, jiandae Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi wa kutoka Mbagala Kokoto mpaka Kongowe ili kupisha ujenzi wa barabara hiyo ambayo umetengewa fedha katika mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chaurembo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya Kokoto kwenda Kongowe, hawa wananchi watalipwa fidia pale ambapo barabara hii itaanza kujengwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, jiandae Mheshimiwa Pallagyo.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kwasadala - Kware - Lemira Kati, kilometa 15.2 ni barabara muhimu sana inayoshusha mazao kwenye soko la Kwasadala na hatimae kuja huku Dodoma na sisi kuweza kuitumia.

Je, Serikali ni lini itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saasisha Mafuwe, Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ya Kware - Lemira ni barabara muhimu sana kwa wananchi wa Hai. Hivi tunavyoongea ni kwamba Serikali inatafuta fedha ili fedha ikipatikana barabara hii ambayo siyo ndefu iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara Serikali itakapopata fedha barabara hii ambayo inasimamiwa na *TANROAD* itajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Pallagyo, jiandae Mheshimiwa Bonnah.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLAGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Je, ni lini Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara ya njia nne kuanzia Tengeru kwenda Holili ambayo ni

sehemu ya mradi wa barabara ya Afrika Mashariki unaoanzia Sakina. Barabara hii ujenzi wake ulisimama takribani sasa hivi miaka Minne.

Je, ni lini ujenzi utaendelea kwa sababu barabara ile sasa hivi ina magari mengi sana na ajali ni nyingi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa swali zuri, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, Mbunge wa Meru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii inayotoka Arusha kwenda Holili ipo kwenye mpango, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tunategemea mwaka wa fedha unaoanza kujenga kati ya Tengeru na Usa River, barabara nne, lakini daraja la Kitafu litajengwa na barabara za Moshi Mjini zitajengwa katika huu mpango. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah, Mheshimiwa Tendega, Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni lini Serikali itakarabati daraja la Kimanga ambalo linazunguka Tabata, pamoja na Kata zingine? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Kamoli Mbunge wa Segerea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa barabara hii upo kwenye usanifu na mara usanifu utakapokamilika daraja hili litajengwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tendega, Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Ilula, Mlafu, kuelekea Kilolo ni barabara ambayo ni mbaya sana. Ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu wakulima wa kutoka Kilolo wanatataka kusafirisha mazao yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tendega Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara aliyoitaja iko katika hali mbaya lakini ni azma ya Serikali kwamba kabla ya kuanza kuijenga itaikarabati kwanza ili iweze kupitika wakati Serikali ikitafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Liwale inazo barabara moja muhimu sana, barabara ya uchumi, barabara ya Mkombozi. Barabara hii nimeizungumza mara nyingi mno, barabara ya Nangurukuru Liwale. Wananchi

wa Liwale wanataka kusikia barabara hii itajengwa lini kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ilishakamilishwa kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, Mheshimiwa Kuchauka atakubaliana nami kwamba Wizara ina mpango wa kuanza kuijenga barabara hii walau kwa awamu mwaka wa fedha unaokuja. Kwa hiyo, itategemea sana na upatikanaji wa fedha, lakini Serikali ina mpango kuianza kuijenga kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Livingstone Kaboyoka.

Na. 38

**Jukumu la Kusafisha Mifereji na Makaravati ya Barabara**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza: -

Je, ni nani mwenye jukumu la kusafisha mifereji na kuzibua makaravati ya barabara zinazojengwa chini ya *TARURA* au *TANROADS*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa

Naghejwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la usafi wa barabara na mifereji ikiwa ni pamoja na kuzibua makaravati ni la msimamizi wa barabara husika. Hivyo, kwa barabara za *TANROADS* mhusika ni *TANROADS* na za *TARURA* mhusika ni *TARURA*.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumuuliza Naibu Waziri kwamba kwa kuwa barabara nyingi zilizoko chini ya *TARURA*, mifereji yake imejaa takataka, imeota majani na ni nyingi na hasa zile Mjini. Na kwa kuwa, tunajua kwamba *TARURA* ina upungufu wa wafanyakazi;

Je, Serikali haioni ni muhimu wakaishauri *TARURA* iingie mkataba *agencies* yoyote ambayo inaweza kusaidia kufanya usafi wa barabara hizi?*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo tumelipokea, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zipo taratibu wa barabara hizi kufanyiwa usafi. Usafi ni pamoja na kufyeka, kuondoa mchanga, ama kuzibua makaravati yanayokuwa yameziba, kazi hizi huwa zinatangazwa ambapo Wakandarasi wanaomba na kupewa hizo Kandarasi kwa ajili ya kufanya huo usafi. Kwa hiyo utaratibu upo na barabara hizo zinasafishwa kwa upande wa *TARURA* TAMISEMI wanasimamia kuhakikisha kwamba barabara zinasafishwa lakini kwa barabara za *TANROADS* ambazo zipo chini ya Wizara ya Ujenzi pia zinasimamiwa

kuhakikisha kwamba barabara hizi hazizibi kwa sababu ya uchafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe rai kwa watumiaji wa barabara kwamba sehemu kubwa ya kuziba hii barabara na uchafu wakati fulani ni kwa sababu ya kazi za kibinadamu ambazo watu wanafanya kazi kwenye hifadhi ya barabara na kusababisha tatizo hilo. Kwa hiyo, niwaombe wananchi kupitia nafasi hii kutokufanya kazi za maendeleo kwenye hifadhi za barabara kwa sababu zinazababisha barabara hizo kuziba. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ameshakuelewa…

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** … zinazababisha barabara hizo kuziba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri, tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mohamed Abdulrahman Mwinyi.

Na. 39

**Hitaji la kituo cha Polisi- Chambani**

**MHE. MOHAMED ABDULRAHMAN MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi Jimbo la Chambani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri,

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdulrhman Mwinyi Mohamed Mbunge wa Chambani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Chambani liko katika Wilaya ya Mkoa wa Kusini Pemba. Wilaya hii ina vituo vya polisi vine ambavyo ni Mkoani, Kengeja, Mtambile, na Mkanyageni. Wananchi wa Chambani wanapata huduma ya polisi kwenye vituo vya Mtambile na Kengeja ambavyo viko ndani ya kilometa sita.

Kwa sasa Serikali kupitia Jeshi la Polisi linatarajia kujenga Vituo vya Polisi maeneo ya vitongoji, Pujini, Wesha na Gombani Wilayani Chakechake ambayo ina kituo kimoja tu cha Polisi katika mkoa wa Kusini Pemba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdulrahman.

**MHE. MOHAMED ABDULRAHMAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna vitendo vya uhalifu vinavyojitokeza katika Jimbo langu la Chambani, kama vile uwingizaji na utumiaji wa madawa, wizi wa mifugo na mazao.

Je, nili Serikali itaanza doria kwa kupambana na wahalifu hao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdulrahman Mwinyi Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Abdulrhman Mwinyi kwa kujali utulivu usalama na amani kwenye Jimbo Lake la Chambani. Hata hivyo, kwa kuwa ujenzi wa vituo hivi utachukua muda nitoe maelekezo kwa *RPC* Mkoa wa Kusini Pemba kuimarisha doria kwenye maeneo korofi ambayo ni pamoja na Dodo, Chambani Pamoja na eneo la Chonga ili wenye vitendo vya wizi wa mifugo na mazao waweze kukoma. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kituo cha Polisi Wilaya ya Itilima tayari umeshaanza na jengo limesimama, na Mheshimiwa Waziri kipindi kile alikuwa Naibu Waziri wa Fedha alikuja kutembelea, Waziri wa Mambo ya Ndani alikuja kutembelea.

Je, ni lini Serikali itatoa pesa za kumalizia ujenzi huo? Na Mheshimiwa Waziri nikuombe uje utembelee katika Wilaya yetu ya Itilima. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua juhudi za wananchi wa Itilima pamoja na Mbunge wao Mheshimiwa Njalu Silanga katika kufuatilia ujenzi wa kituo hiki. Na kuhusu ombi lake, kwamba nitembelee Itilima, niko tayari kutembelea Itilima ili kuweka msukumo wa kupata fedha kutoka tunzo na tozo ili ukamilishaji wa kituo hiki uweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Simai.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la moja la nyongeza.

Ni lini Serikali itajenga uzio kuzunguka eneo la Kituo cha Polisi lilolokuwepo Nungwi ili kuepusha uvamizi eneo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Simai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tutatathimini mahitaji ya gharama za ujenzi wa uzio huo ili kuweza kuanza mkakati wa ujenzi kupitia juhudi za mfuko wa tunzo na tozo kama ambavyo tumefanya kwenye maeneo mengine.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante; Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali imekuwa ikiahidi mara nyingi kujenga Kituo cha Polisi Itigi ambacho wanatumia majengo chakavu ya reli, angalau kituo cha daraja C. Sasa, je, ni lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Massare Mbunge wa Itigi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchakavu wa kituo kilichopo, tutafanya tathimini kuona kiwango cha uchakavu; na kama eneo hili halitoshi tuko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili eneo lipatikane la kutosha kwa ajili ya kujenga kituo chenye hadhi ya Wilaya ya Itigi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Venant.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wananchi wa Kata ya Tula na Goweko wameanza ujenzi wa vituo vya afya. Ni lini Serikali itapeleka fedha kuungana na wananchi kumalizia vituo hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tutafanya tathimini ya kuangalia kiwango cha ujenzi uliofikiwa ili kuona kiasi cha fedha ambazo zinahitajika kumalizia ujenzi wa kituo hicho, na gharama zitakapojulikana zitajumuishwa kwenye mapango wetu wa umaliziaji wa vituo vya polisi vikiwemo hivyo vya Goweko na Igalula**.**

**NAIBU SPIKA:** Haya wewe uliyesimama, unacheka hapo, wewe unaitwa nani.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Neema Mwandabila.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mji wa Tunduma upo mpakani na kituo kilichopo pale hakina hadhi ya kuweza kuhudumia katika eneo lile; wahalifu ni wengi kiasi kwamba kinalemewa.

Ni lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga kituo cha chenye hadhi ya Wilaya katika eneo la Tunduma?

**NAIBU SPIKA:** Haya, nii lini, Mheshimiwa Neema huyo anauliza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mwandabila kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu hivi majuzi kwamba Wilaya zote ambazo hazina vituo vya polisi ni mpango wa wizara kuanza ujenzi kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, eneo analolitaja hili ni moja ya maeneo ambayo yatazingatiwa katika ujenzi wa vituo vya polisi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swali la nyongeza.

Ni lini Serikali itajenga kituo cha polisi cha Wilaya Uvinza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu Wilaya ya Uvinza ni miongoni mwa wilaya mpya ambazo hazina vituo vya polisi, na kwa hiyo katika mkakati wetu wa kuhakikisha mikoa na wilaya zote ambazo hazina vituo vinajengewa vituo hivyo Uvinza ni eneo mojawapo litakalo zingatiwa katika ujenzi wa vituo vipya vya polisi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa mujibu mazuri, hongera sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa wale Wabunge Viti Maalum muwe mnakuja kuja kwa Naibu pale, mnajitambulisha, inakuwa rahisi kuwaona ona. Sasa mkijificha ficha ...*(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Jaza ujazwe.

**NAIBU SPIKA:** Na huu mwezi wengine hatuingii kantini siku hizi ila unakuja pale unajitumbulisha mimi fulani, ee! umesikia Bi. Neema? Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni waliopo Bunge asubuhi hii, wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wawili wa Mheshimiwa Venant Daud Protas -(Mbunge ambao ni ndugu zake kutoka Jimboni Igalula Mkoani Tabora; nao ni Ndugu Daudi Nteminyanda na Ndugu Juliana Mashaga. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni Wanachuo 15 wa Bunge la Serikali ya Wanafunzi wa Chuo

cha Mipango Dodoma wakiongozwa na Spika wa Bunge hilo Ndugu Jasson Makandala. Karibuni. *(Makofi)*

Katibu!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano, Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu tunaanza na Mheshimiwa Gwajima. Mjadala lete nondo mzee. *(Makofi/ Kicheko)*

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwanza wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyofanya kuwasaidia Watanzania. Pia nimshukuru Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hussein Mwinyi kwa namna anavyofanya kuisaidia Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi sana mimi nataka kujadili hoja iliyo mezani ya ofisi au hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kusema maneno haya, kwamba namshukuru sana Mungu, kwamba ninafikiri kuna sababu zinazoifanya nchi yetu ibaki pale ilipo kwa muda mrefu. Sababu mojawapo ambayo nimefikiri sana ni kwamba nchi yetu inahitaji dira au inahitaji ajenda ya taifa au maono ya taifa au mwelekeo wa taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia ina mataifa kama 197 hivi lakini kuna mataifa 193 yanayokubalika na Umoja wa

Mataifa. Kwa neema ya Mungu mimi nimewahi kufika zaidi ya mataifa 143, ni mataifa hamsini tu ya duniani ambayo sijawahi kufika. Lakini mshangao ambao nimekuwa nao sana kwa miaka mingi ni kwamba mataifa yote yenye watu wa asili ya Afrika, kwa maana ya ngozi yetu yana asili za kufanana yana matatizo yanayofanana na yapo nyuma kwa aina ya kufanana. Suala hili limenifanya nijiulize sana kwa nini mataifa yenye asili ya watu wa Afrika *wheather Latin America, or Afro-Caribbean* kwa maana ya Jamaica *Hyatt* na mengine yana matatizo yanayofanana?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja nikaligundua juu ya mataifa haya; kwamba mataifa haya hayana maono ya muda mrefu yanayoifanya nchi iwe *guided* kiasi kwamba kila utawala unapoingia katika mamlaka ufuate maono ya muda mrefu. Simaanishi kwamba hakuna maono kabisa, lakini hebu nitoe mfano kidogo. *United Arab Emirates* wana mpango wa kuanzia mwaka 2050 mpaka 2117 wa kuhamishia makazi ya kwanza katika Sayari ya *Mars,* ni mpango wa taifa wa muda mrefu. Lakini pia *United Arab Emirates* wana mpango wa kuwa nchi ya kwanza duniani katika nchi 10 zenye hifadhi ya chakula cha kutosha kufikia mwaka 2051. Vilevile, *United Arab Emirates* wana Mpango wa Taifa wa *Clean Energy* kuanzia 2020 mpaka 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna taifa lililoendelea duniani bila mpango wa muda mrefu. Tusipokuwa na mpango wa muda mrefu kasi ya maendeleo haitaenda kama inavyotakiwa. Niliwaza kwamba inawezekana labda tunashindwa kupanga mpango wa muda mrefu kwa sababu labda katiba haituruhusu au sheria haituruhusu. Nikasoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63 (3)(c) inasema hivi:-

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake –

(c) kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika

Jamhuri hii ya Muungano, na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaona kumbe katiba yetu inaruhusu, kwamba Serikali inaweza kuleta mpango wa muda mrefu wa namna ambavyo Tanzania iwe miaka 50 ijayo, Tanzania iwe miaka 80 ijayo ili kila utawala unaoingia madarakani ufuate maono ya nchi ambayo nchi imejipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hatari itatupata siku zijazo. Kwamba, ndiyo maana unasikia watu wanasema tunahitaji Rais mwenye maono, tunahitaji Rais mwenye maono kwa sababu nchi haina maono, tunahitaji nchi yenye maono ili kila Rais anayeingia madarakani afate maono ya nchi tuliyoiweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutaruhusu kila mtu anayeingia madarakani aongozwe na kichwa chake anavyowaza yeye kuna siku tutapata Rais wa ajabu tutadondokea pua hatutaamini macho yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unakumbuka vizuri baada ya vita vya pili vya dunia nchi za ulaya zilifilisika kabisa. Ukiangalia Wa-Marekani wakaanza mpango unaoitwa *marshal plan*, *marshal plan* kipindi kile Rais wa Marekani alikuwa *Truman,* wakaanza mpango wa kuzisaidia nchi 17 za ulaya magharibi zilizokuwa zimefirisika kabisa. Nchi hizo wakazipa *almost* dola bilioni 13 ambayo ni bilioni 115 kwa sasa. Marekani akawaambia kila nchi izalishe mpango wake wa muda mrefu na dira yake. Kila nchi ikazalisha dira yake, mpango wake na zikapewa hizo fedha; nan chi hizo zikatoka hazipo kama sisi tulivyo. Sisi mpango tulionao sasa ni kufikia tu 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi yangu ni kwamba tuipe dira nchi yetu, tuwe na mpango wa zaidi ya miaka 50 au miaka 60 au miaka 100 ya Tanzania ijayo ili mitaala yote ya shule na ilani zote za chaguzi na watoto wote waweze kuiona Tanzania kwenye *three D* na waweze kujifunza na kuiona Tanzania ijayo; vinginevyo tutapoteza muda mwingi

sana kwa kuzunguka pale pale na kufanya mambo yale yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupe mfano; tumekuwa na *regime* iliyopita ilifanya vizuri sana. Tumekuwa na Rais wetu Mwalimu Nyerere aliendelea kwa namna yake akaja Mwinyi aliendelea kwa namna yake, lakini alipoishia Nyerere, Mheshimiwa Mwinyi hajaendelea pale, alipoishia Mwinyi, Mkapa hajaendelea pale, alipoishia Mkapa, Kikwete hajaendelea pale, alipoishia Kikwete, Magufuli hajaendelea pale tunakuwa kila Rais anayeingia madarakani anaanza chake na matokeo yake tutapata Rais wa ajabu tutaangukia pua hujawaji kuona. *There is no country that can develop within a single regime,* nchi zote zinazoendelea ni mwendelezo wa *regime* ya kwanza, *regime* ya pili, *regime* ya tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ili *regime* ibaki kwenye *guidance* lazima yawepo maono ya taifa ili Rais anayeingia madarakani ayatumikie maono ya taifa na sisi wananchi tuyaone kama maono ya taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tu-*define* ni kitu gani sisi tunakiita maendeleo, tunachokiita maendeleo sisi si lazima kiitwe maendeleo Marekani. Kwa mfano; tunaweza kuwa na namna yetu ya kusema kwetu sisi maendeleo ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gwajima sekunde tatu malizia.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: ...**kwetu sisi maendeleo kila mtu awe na maji safi, kwetu sisi maendeleo tuwe na hospitali. Kwa hiyo, ninaomba kusema ni muhimu sana nchi yetu iwe na Dira ya Taifa na Maendeleo ya Taifa ili kila Rais anayeingia madarakani awe mzuri awe wa namna gani asimamie maono ya nchi tuliyoyaweka na wala si maono yake mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa, Mheshimiwa Sillo, jiandae Dunstan Kitandula.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanyia taifa letu, na sisi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, kwamba kuna kazi kubwa imefanyika katika majimbo yetu kwenye miradi mbalimbali ya maji, afya nakadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Makamu wa Rais lakini ikitokea pia nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayofanya ya kusimamia miradi mbalimbali ya Serikali pamoja na hotuba yake nzuri aliyotoa tarehe 6 mwezi huu katika Bunge lako Tukufu. Bajeti ambayo imeonyesha muelekeo wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia kwangu nitajielekeza katika maeneo makuu matatu. Eneo la kwanza ni Eneo la kilimo, eneo la pili ni migogoro ya ardhi, tatu ni ujenzi au uwekezaji katika balozi zetu za nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na Sekta ya Kilimo. Ni kweli kwamba tunafahamu sekta hii ya kilimo imeajiri Watanzania nguvu kazi zaidi ya asilimia 65, na asilimia 90 ya walioajariwa katika sekta hii ni wakulima wadogo na wa kati ambao bado hawana uwezo wa kupata mikopo katika Benki mbalimbali ikiwemo Benki yetu ya Kilimo. Kwa hiyo, wanategemea sana ruzuku ya Serikali ili waweze kuendeleza shughuli zao za kilimo. Maana yake nini? Maana

yake ni kwamba wakulima wetu wengi wanafanya kilimo cha kujikimu; kilimo cha chakula tu, lakini siyo kilimo cha biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna kazi kubwa sana inatakiwa ifanyike ndani ya Serikali kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanawezeshwa ili wafanye kilimo chenye tija, kwa maana ya kilimo cha chakula pamoja na kilimo cha biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu, takwimu zinasema Sekta ya Kilimo inachangia karibia asilimia 27 pato la Taifa, pia inachangia zaidi ya asilimia 60 ya malighafi viwandani, lakini mauzo ya nje ya nchi ni takribani Dola za Kimarekani bilioni 1.2 kwa mwaka. Sekta hii ndiyo inayolisha asilimia 100 ya chakula hapa nchini, kwa hiyo, ni sekta muhimu katika maendeleo ya Taifa letu na mustakabali mkubwa wa wananchi wetu. Hata hivyo, sekta hii inakua kwa wastani wa asilimia nne hadi tano kwa mwaka. Kwa hiyo, kuna kazi kubwa sana ya kufanyika ndani ya Wizara ya Kilimo ili tuweze kuwakwamua wananchi wetu katika sekta hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimu Naibu Spika, kwa maana hiyo basi, kuna umuhimu mkubwa sana kuwekeza katika sekta hii muhimu ya kilimo. Tuna mpango wetu wa Taifa wa Uchumi Shirikishi. Bila kuwekeza kwenye kilimo itakuwa ni ndoto kufikia uchumi shirikishi. Najua Waziri wetu wa Kilimo ana mipango mizuri sana kwenye sekta hii, namwomba sana aangalie sekta hii kwa jicho la pili ili kuhakikisha kwamba tunafikia uchumi shirikishi kwa kuiwezesha sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira haya basi, kazi kubwa ya Serikali ni kuandaa mazingira, maana tunaamini Serikali pekee haiwezi kufanya kazi hii ya kilimo lazima tushirikishe na sekta binafsi. Tuna mfano mzuri wa nchi yetu ya jirani hapo Zambia, Zambia leo kuna sekta binafsi imewekeza sana kwenye kilimo na kilimo kimefanikiwa sana. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Serikali kuandaa mazingira mazuri

ya kuwezesha sekta binafsi kushiriki katika suala zima la kilimo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia sekta mbalimbali, sekta kama ya nishati pamoja na miundombinu, zinachangia sana katika pato la Taifa, ni kwa sababu Serikali imewekeza. Kwa hiyo, hata sekta ya kilimo hii ikiwezeshwa, basi inaweza ikachangia kwa kiasi kikubwa sana kwenye pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Serikali ielekeze kwenye kuwekeza kwenye sekta za uzalishaji. Manufaa ya uzalishaji ni kama ifuatavyo: moja, unaongeza ajira kwa Watanzania, unaongeza malighafi za viwandani, unakuza biashara ya nje na ya ndani; na kupanua wigo wa kodi. Tumekuwa tukilalamika kwamba walipa kodi tunawarudia wale wale; tukiweza kwenye sekta za uzalishaji ni wazi kwamba tutapanua wigo wa walipa kodi na baadaye Serikali ipate mapato ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu sasa kwenye sekta hii ya kilimo, kwanza kama nchi lazima tujielekeze kwenye uzalishaji na siyo kwenye matumizi. Mambo ya kufanya ni kama ifuatavyo: Moja, ni kujenga au kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ili kuwe na kilimo cha msimu wote wa mwaka; la pili, lazima tuainishe maeneo maalum ya kilimo na aina ya mazao katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka kulikuwa na *crop map* hapa nchini, ni vizuri sana tukaifuata ili tuweze kuzalisha, tuwe na maeneo mahsusi kwa ajili ya mashamba, pia tuwe na aina ya mazao husika. Eneo lingine, lazima tuboreshe utafiti ili tuweze kuzalisha mbegu bora hapa nchini. Leo hii tunalia kilo moja ya mbegu ni Shilingi 12,000/=; gunia la mahindi ni Shilingi 20,000/=. Haileti tija kabisa! Kwa hiyo, kuna haja kubwa sana ya kuendeleza utafiti na hatimaye kuzalisha mbegu bora hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kutafuta masoko ya uhakika kwa mazao ya wananchi wetu. Nitatoa mfano,

Mkoa wa Manyara au Babati Vijijini kuna mashamba makubwa ya mbaazi, lakini wakulima wanalima na baada ya kuvuna, hawana pa kuuza. Kwa hiyo, naomba sana Serikali itafute masoko ya uhakika ya mazao yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuwa na mfuko maalum wa kuwalinda wakulima wetu hasa wakati bei za pembejeo zinapopanda na wakati bei za mazao yao zinavyoshuka. Mfuko utawasaidia sana wananchi wetu kujikumu na kuendelea na kilimo cha uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kujenga maghala ya kutosha ili kuokoa upotevu wa mazao. Taarifa inasema kuwa tunapoteza karibia asilimia 30, *postharvest loss.* Nina imani kubwa sana kwamba tukijenga maghala ya kutosha, basi hili litapungua sana. Kwenye eneo hili, naipongeza sana Serikali, imejenga maghala kule Babati, Sumbwawanga na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni migogoro ya ardhi kati ya wawekezaji na wananchi wetu. Naipongeza Serikali, iliundwa timu ya Mawaziri nane, walizunguka nchi nzima kutatua migogoro hii, lakini bado kuna migogoro katika maeneo yetu kati ya wawekezaji na wananchi wetu. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, bado kuna changamoto hii ya migogoro kati ya wawekezaji na wananchi wetu na katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua sana Sera ya Uwekezaji ni nzuri, inaleta ajira kwa Watanzania, lakini pia inaleta mapato kwa maana kulipa kodi ya Serikali. Nitatoa mfano, kule kwangu Babati kuna migogoro kati ya Kata ya Kiru kule Magara, lakini pia kiwanda cha Minjingu na wananchi wa vijiji vya *City* na Minjingu. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijielekeze katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kati ya Hifadhi na Vijiji vyetu. Natambua kazi kubwa ya Serikali iliyofanya kutatua migogoro kati ya Hifadhi za Taifa na vijiji, lakini bado changamoto ipo. Naiomba sana Serikali, Mawaziri

washirikiane na Wabunge ambapo sisi ndiyo wawakilishi wa wananchi, ndio tunajua migogoro iko wapi? Tukishirikiana kwa pamoja, naamini tukienda pamoja, basi migogoro hii itapungua au itakwisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ni ujenzi au uwekezaji katika Balozi zetu nje ya nchi. Natambua Balozi zetu zina viwanja vingi nje ya nchi; na ninaipongeza Serikali imeanza kujenga katika Balozi zetu kule Oman, lakini bado kuna viwanja havijaendelezwa. Nitatoa mfano kwa nchi ya Zambia. Zambia kwenye Balozi yetu kuna viwanja karibia nane na vipo kwenye *very prime area.* Kwa hiyo, nadhani tukijenga humo tutapata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna njia tatu; kuna *mortgage financing*, kuna mifuko yetu ya kijamii na *PPP.* Serikali ikijielekeza huko tutapata fedha...

*(Hapakengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, sekunde tatu malizia.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa nafasi hii, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Kitandula, jiandae Mheshimiwa Gambo.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kumshuruku Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema ambaye ameturuzuku uhai na pumzi hii tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanyika katika nchi yetu. Tumeona kazi kubwa inayofanyika kwenye Sekta ya Afya, tumeona kazi kubwa inayofanyika kwenye Sekta ya Elimu, tunaona kazi kubwa inayofanyika kwenye barabara za vijijini, hongera sana kwa Serikali. Tunaomba kazi hii iendelee ili tuweze kuwaondolea wananchi matatizo yanayowakabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii vilevile kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ziara ambayo aliifanya kwenye Jimbo langu la Mkinga, ziara ambayo imeleta chachu ya maendeleo katika Wilaya yetu. Hapa nitazungumzia kiujumla. Kuna kazi kubwa inafanyika kwenye vituo vyetu vya mipakani kwa *facilitate* biashara na kuingiza mapato kwenye nchi yetu. Kwa kipindi kirefu, *border* yetu ya Horohoro ilikuwa haifanyi vizuri, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja, amefanya kazi kubwa, na leo hii tunasimama kifua mbele, *border* ile inaingiza mapato mengi sana kwa nchi yetu. Tunaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naipongeza, yapo mambo ambayo tunayaona Mkinga na tunahisi vilevile kwenye maeneo mengine ya mipakani yapo. Pamoja na kazi kubwa iliyofanyika hii ya kukusanya mapato, lakini kituo chetu kile kina matatizo ya miundombinu ya usafiri. Kuna matatizo makubwa ya vifaa vya usafiri na vile vile kuna tatizo la huduma ya zimamoto. Vituo hivi vinakuwa na shehena kubwa ya mizigo. Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwezesha kupata *fire equipment* katika maeneo ya mipakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mkinga inapakana na nchi ya Kenya na mpaka wetu kule ni *porous,* kwa hiyo, tunahitajika kufanya ulinzi wa mara kwa mara; kufanya doria ya mara kwa mara. Tatizo tunaloliona, watu wetu wa vyombo vya usalama wana matatizo makubwa ya vyombo vya usafiri. Sasa naomba Serikali iangalie hili kwa jicho la pekee kwa Mkinga. Ninaposema hivi Serikali mnaelewa, *position* ya Mkinga tunahitaji kufanya doria ya nguvu, mambo ya

uhamiaji haramu mnayajua, tusaidieni watu wetu wa Polisi wapate gari waweze kufanya shughuli zao vizuri.

Mhehsimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kwenye ziara yake alitoa maagizo baada ya kusikia wananchi wana matatizo ya ardhi. Naishukuru Serikali inalifanyia kazi jambo hili kupitia kikosi kazi cha timu ya Mawaziri. Rai yangu, kikosi kazi hiki kinapofanya kazi nchi nzima, lazima kioanishe na ahadi walizotoa viongozi wetu. Kikosi kazi hiki kikienda kufanya shughuli kikasahau kutekeleza ahadi za viongozi wetu, tutakuwa tumewadhalilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja Mkinga, alisikia kilio cha wananchi wa Mkinga, pale Maramba hawana ardhi, akaagiza kazi ifanyike ya tathmini ya tatizo lile mwezi wa Pili mwaka 2020. Miezi sita baadaye Waziri Mkuu aliporudi Tanga, akatoa tamko akiwa Lushoto kwamba wanaenda kumega ardhi ya Shamba la Mwele ili wananchi wapate ardhi. Alipokuja Mkinga wiki moja baadaye akatoa agizo kwamba Serikali inaenda kumega sehemu ya shamba ili wananchi wale waweze kupatiwa ardhi. Tunaposema hapa ni kwa sababu ya tatizo kubwa la ardhi kwenye vijiji vile vya Maramba A na Maramba B.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maramba A yenye kaya 1,747 umiliki wa ardhi kwa kila mwananchi mmoja, ni asilimia 0.36 ya hekta; Maramba B yenye kaya 725, umiliki wa ardhi ni asilimia 0.6. Huu ni umasikini mkubwa kwa wananchi hawa. Tunampongeza Waziri Mkuu, aliliona hili. Tunaiomba Serikali, ahadi hizi za viongozi wetu wa wakuu ziweze kufanyiwa kazi. Hili linaenda sambamba na kazi kubwa iliyokuwa imefanyika tangu mwaka 2016 na kikosi kazi kilichoundwa na Serikali, kikafanya kazi kubwa ya kuzunguka vijiji vyote vinavyohusisha Pori Tengefu kwenye Wilaya ya Muheza, Wilaya ya Korogwe na Wilaya ya Mkinga. Maagizo yale tuliyokubaliana, tunaomba yahusishwe kwenye shughuli hii inayoendelea sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwenye Huduma ya Afya imetupatia Hospitali ya Wilaya. Naomba

sasa hospitali hizi zijengewe wodi ili wananchi waweze kupata huduma za uhakika. Tumeahidiwa kwa kuda mrefu bandari ya Moa, ambazo ni bandari bubu, kwamba sasa inaenda kuwekewa miundombinu ili biashara kati ya Mkinga na Zanzibar, Mkinga na Pemba iweze kuwa *facilitated.* Tunaomba ahadi hiyo iweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa jitihada za reli zinazofanyika; maendeleo kwenye sekta ya reli, lakini tunachokiona ni kwamba ujenzi wa reli ule hauendi sambamba na reli nyingine. Reli ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha imesahaulika, kazi inayofanyika sivyo kama tulivyokuwa tumeahidiwa mwanzoni. Tunaomba na reli ile iweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Gambo, jiandae Mheshimiwa Kakoso na Mheshimiwa Munde.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wenzangu kushukuru sana kupata fursa hii adimu niweze kutoa mchango wangu kwenye Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mwaka 2021 ajenda yangu kubwa ilikuwa utalii; mwaka huu ajenda yangu kubwa itakuwa ni sekta ya madini. Kabla sijaenda kwenye sekta ya madini, naomba nizungumzie changamoto tulizokuwanazo katika uwanda mzima wa biashara sisi kama Watanzania na pia kama Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukiangalia Sheria yetu ya Mwaka 2007, ukienda ukurasa wa 72 Kifungu cha 31, tunaambiwa kwamba *"The Business Licensing Act of 1972 is hereby repealed."* Kwamba sheria hii ya mwaka 1972 ilifutwa, lakini cha kushangaza sheria hii ambayo ilifutwa mwaka 2007 kupitia sheria ya *Business License Act* ya 2007 Kifungu 31, bado

tukaenda kuifanyia marekebisho mwaka 2014, 2015 na 2018. Yaani Bunge lako hili lilifuta sheria ya mwaka 1972, likaanzisha sheria ya mwaka 2007, lakini bado likaenda mwaka 2014 lirekebisha sheria ambayo ilishafutwa tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye sheria hii ya mwaka 1972, ukienda kwenye ukurasa wa 9, kuna *Act (No. 2) of 2014 Section No. 6;* ilifanyia marekebisho ya sheria ambayo imefutwa. Pia ukienda kwenye ukurasa wa 12, mwaka 2015 yalifanyika marekebisho kupitia Sheria ya Fedha kwa kuongeza maneno yafuatayo, pia ilienda ikafuta na jedwali, yaani imekwenda kurekebisha kitu ambacho Bunge tayari ilishafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo uone ni namna gani tulikuwa na changamoto kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ukienda kwenye Sheria yetu ya Madini, ukiangalia kanuni yetu, tulikuwa na kanuni ya mwaka 2002 ambayo tulikwenda kuifuta mwaka 2019. Mara baada ya kuifuta, tukaja kufanya marekebisho mengine mwaka 2021. Kinachonishangaza, ukiangalia hii Kanuni, inasema imekuwa *gazetted* tarehe 2/7/2021. Nimekwenda kutafuta gazeti la Serikali la tarehe 2/7/2021, sijaikuta hii kanuni. Ila nimekwenda kuikuta kwenye gazeti la Serikali la tarehe 9/7/2021. Gazeti lenyewe pia ukiangalia bado limeandikwa tarehe 2/7/2021, ukija hapa ni la tarehe 9 Mwezi wa Saba. Kwa hiyo, utajiuliza, ni kweli sisi wote ni vipofu? Yaani Bunge, Wizara ya Madini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wote hatuoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini yametokea haya? Yametokea haya kwa sababu tunajua Serikali inapotoa maelekezo, inatoa kwa nia njema sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokwenda Mererani tarehe 2/7/2021, alitoa maelekezo kwamba Sheria ya Madini na Kanuni zake viweze kubadilishwa. Tarehe 8 wakabadilisha kanuni, Waziri akasaini, tarehe 9 tukai-*gazette.* Katika uharaka wa namna hiyo bila kushirikisha wadau, lazima kuwe na changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niende kwenye hoja ya msingi. Ukienda kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 37 kipengele cha 67, Mheshimiwa Gwajima alikuwa anashika *documents* zangu, isije ikawezekana kwamba ameziweka pembeni; inasema kwamba, "Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi na kuanzisha masoko mapya ya madini na vituo vya ununuzi nchini kwa lengo la kupata takwimu sahihi za mauzo ya madini, kuongeza ukusanyaji wa maduhuli na kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata soko la uhakika na kupata bei stahiki kwa bidhaa za madini."

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu sote kwa mwaka, 2019 tulianzisha masoko ya madini. Arusha lilikuwepo, Mererani lilikuwepo na maeneo mengine mbalimbali katika nchi yetu. Kwenye masoko ya madini haya tulikuwa tunaruhusiwa kuuza madini ya aina zote, ukienda pale Arusha leo tuna madini kutoka Kongo DRC, kutoka Msumbiji, kutoka Ethiopia na kutoka Kenya, lakini *tanzanite* ambayo inapatikana Tanzania hairuhusiwi kwenda kuuzwa kwenye soko la Arusha. Maamuzi ya kubadilisha Kanuni yameipatia Serikali hasara kubwa sana naomba nikupe taarifa ifuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, wakati linaanzishwa soko pale Arusha, nikichukua taarifa ya Julai hadi Disemba, 2019 tulipata *carets* 76,000 lakini kodi iliyopatikana ya Serikali ilikuwa ni shilingi milioni 487. Ukiangalia kwenye *rough tanzanite* tulipata kiasi cha kodi shilingi bilioni 1,300,000,000/= na point kadhaa. Ukija mwaka 2020 tuliweza kuwa na *caret* ya 85,000 tuliweza kupata kodi ya shilingi milioni 332 lakini kwenye *rough tanzanite* tuliweza kupata kodi ya shilingi bilioni 1.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuhamishia Mererani ukiangalia kipindi kile kile cha Julai, 2021 tumeacha Disemba hadi Januari, Serikali imepata kodi kiasi cha shilingi milioni 339 kutoka shilingi bilioni 1.3. Unaangalia kwenye upande wa *caret* tumeweza kuwa na *caret* 15,000 kutoka 85,000. Kwa hiyo, unaona kabisa maamuzi haya yamekwenda kuitia hasara Serikali lakini pia, kwa mujibu wa

taarifa tulizokuwa nazo pale Arusha idadi ya *dealers* walikuwa ni 103, leo kuna *dealers* 48 tu kule Mererani. Kulikuwa kuna mashine za kukatia 427… *(Makofi)*

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa mtoa hoja taarifa kwamba madini ya *tanzanite* yapo katika Mkoa wa Manyara na katika takwimu zinaonyesha, Serikali imeweza kuongeza kipato toka soko liliporejeshwa katika Mji wa Mererani ambapo madini ndipo yanapochimbwa. Pia, imeweza kuwarahisishia wafanyabiashara pamoja na wachimbaji wadogo wadogo kuweza kuuza madini, kwa uhakika na usalama uliokamilika na kuendelea kuukuza Mji wa Mererani katika Mkoa wa Manyara. Hivyo, napenda kumpa mtoa mada taarifa kama anatamani madini ya *tanzanite* basi tunamkaribisha katika Mkoa wa Manyara, tuna maeneo makubwa bado tunahitaji wananchi wa kuja kuwekeza. Kwa hiyo, tunamkaribisha katika Mkoa wa Manyara ili apate madini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Gambo taarifa hiyo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwamba Wabunge watafute hoja za kuchangia sio tunadandia tu mradi tuonekane na wananchi wetu. Hapa tunaongea mambo *serious,* kwa hiyo sipokei taarifa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ajira ambazo zimepotea, ajira zaidi ya 413, kuna *ma-broker* pale kati ya 2,500 – 3,000 ambao pia wamekosa ajira. Hata hivyo, Serikali ikiwa imepata hasara Soko la Madini la Arusha inahusisha majengo ya *AICC, NSSF* na *PSSSF*. Serikali imepata hasara kiasi cha shilingi milioni 128 ambazo zilikuwa zinalipwa na wafanyabiashara wa madini kwenye maeneo hayo.

Naomba nitoe mapendekezo na ushauri kwa sababu wote tunajenga nyumba moja. Mapendekezo yangu; la kwanza, tunaomba masoko ya madini ambayo yameanzishwa kwa mujibu wa taratibu za nchi hii, yaruhusiwe kuuza madini ya aina zote, maana inashangaza kuona leo *Tanzanite* unachukua Mererani... *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo, malizia sekunde mbili, Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, unakwenda kuiuza India na Tanzania haipatikani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele hiyo ya pili, sekunde mbili malizia.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Kwa hiyo, napendekeza pia Mererani ibaki sehemu ya uzalishaji wa *tanzanite* na soko la malighafi kwa mfumo wa mnada mara moja au mara mbili kwa wiki. Kwa sababu...*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, mengine peleka kwa maandishi. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Munde, atafuatiwa na Mheshimiwa Kakoso na jiandae Mheshimiwa Rweikiza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri Mkuu na Mawaziri wetu wote kwa kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kilimo. Tumekuwa tukishuhudia upungufu mkubwa wa vitu kama mafuta kutokuwa na mkakati mzuri ambao ungeweza kutuondoa kabisa kwenye hiyo dhiki ya mafuta. Niongelee kuhusu *block*

*farm* mashamba ambayo yanalimwa kwa pamoja na yakiangaliwa na wataalam wetu. Najiuliza tu hivi kila Wilaya ingekuwa na *block farm* kubwa ambayo zile Wilaya zinakubaliana na alizeti, zikalima alizeti kuanzia heka 2,000 mpaka 3,000, naangalia ndani ya mwaka mmoja au miwili kweli tungekuwa bado tunapambana na kadhia hii ya mafuta ya kula? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni swali kubwa ambalo najiuliza nalo na niiombe Serikali iwe *serious* sasa kwenye suala zima la kilimo, ili kuokoa fedha zetu nyingi ambazo zinakwenda nje ya nchi kwa ajili ya kununua mafuta. Najaribu kuwaza tu kama tungeweza kulima heka 3,000 za mafuta kwenye Wilaya ndogo kwa mfano kama Urambo, heka moja wangeweza kupata shilingi milioni moja na nusu mpaka mbili tuseme wamekosa kabisa wamepata Sh.700,000/=. Ina maana Wilaya hiyo ingepata shilingi bilioni 2.1, ni ajira tosha kwa vijana wetu ambao tunahangaika nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka vijana wanamaliza Chuo Kikuu kuanzia 80,000 mpaka 100,000, hata Serikali ilete ajira gani hatutaweza kumaliza kuwaajiri. Ni lazima kwa makusudi mazima tuanzishe mashamba haya ambayo yatakuwa ni ajira kwa vijana wetu, lakini yatakuwa ni mwendelezo wa uchumi kwa Taifa letu. Tumemwona Mheshimiwa Rais anafanya makusudi mazima kuhakikisha anaweka mbele suala zima la kilimo, kwa ajili ya kupandisha uchumi lakini kwa ajili ya ajira pia kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais juzi tumeona ametoa pikipiki ambazo haijawahi kutokea kwenye historia ya nchi hii. Ametoa vipima udongo, binafsi nilikuwa sijui hata kama kuna vipima udongo, lakini Mheshimiwa Rais ametoa kwa nchi nzima. Yote hii sasa ibaki Wizara husika pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha na sisi tunakuwa *serious* katika kusimamia hii. Najaribu kufikiria tu je, *Ma-DC* wote wangepewa kwa maandishi kwamba ni lazima kila wilaya iwe na *block farm*, ni lazima kila wilaya ilime shamba la kimkakati leo hii tungekuwa na kilimo kiasi gani? Pia na

*Ma-RC* wetu ambao wanafanya kazi nzuri, lakini bado kwenye kilimo tunahitaji msisitizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tungekuwa tunashindanishwa labda katika mikoa na wilaya kwamba ni *DC* gani alikuta wilaya yake inalima alizeti kwa asilimia nne akapandisha ikaja asilimia 10 au asilimia 15? Hii ingetusaidia sana. Kwa hiyo niiombe Serikali sasa iwe *serious* kwenye suala zima la kilimo na viongozi wetu ambao ni *Ma-DC* na Wakuu wa Mikoa, wawekewe viwango, ni lazima tuone mkakati wa kuhakikisha kilimo kinasonga mbele hasa kilimo cha kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu Tabora tuna *DC* wetu mzuri sana anaitwa *Comrade* Nawanda. *DC* huyo ametafuta Kijiji kimoja Ikomwa akatenga eneo la *block farm* kwa ajili ya Kijiji cha Vijana tu. Tunaamini vijana pale wakikaa kama 3,000 au 4,000 tutakuwa tumepunguza tatizo kubwa la ajira, watu wengi wanaotaka ajira tutakuwa tumewapunguzia pale. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kumwomba Naibu Waziri Katambi, anakwenda Shinyanga njia yake ni Tabora. Tunaomba akipita Tabora aje apite pale Ikomwa aone shamba letu lile la vijana lililotengenezwa na *DC* wetu wa pale Tabora Mjini, ili aweze kutupa mawazo lakini ku-*empower* kwa kitu chochote kile ambacho ataona kitasaidia na vijana wenziwe watakuwa wamepata ajira. Tunamwomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona pale Manyoni kuna *block farm* ya korosho, inakwenda vizuri mno, karibu viongozi wote wa Kitaifa wamewekeza, wana mashamba pale kwa nini tusifanye kwa nchi nzima kwa zao linalokubalika? Kwa hiyo, niiombe sana Serikali ili kutoa tatizo hili ni lazima tuwe *serious* na tupitie kwa Wakuu wetu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuwapa maelekezo kwamba ni lazima kila wilaya na mkoa wake wapate *block farm*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi sasa kwenye Mkoa wangu wa Tabora niongelee kuhusu barabara. Niiombe Serikali sasa ituunganishe watu wa Tabora kutoka Tabora

kwenda Mbeya kupitia Ipole. Mpaka sasa hivi kutoka Sikonge kwenda Ipole kuna lami, kutoka Chunya mpaka Makongorosi kuna lami, lakini kuna eneo dogo lililobaki hapo katikati ambalo liwekwe lami basi tutoke Tabora mpaka Mbeya kwa lami. Niombe barabara ya kutoka Tabora kwenda Mambari, Mambari – Itobo, Itobo – Kagongwa ili iunganishe kwa lami kutoka Tabora – Mambari – Igongwa; na barabara hii ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi toka 2010. Tunashangaa Serikali inashindwa wapi kuimalizia barabara hii ambayo itakuwa ya ukombozi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naongelea tena barabara ya Tabora, Ulyankulu ambayo ina kilomita 90, tunaomba sana ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee suala zima la afya. Nimetoka kuuliza swali hapa kwenye Kituo cha Afya cha *Town Clinic* pale Tabora, kile kituo ni cha zamani sana na kiko mjini, sio kituo cha afya ni zahanati lakini zahanati hii inazalisha watoto 10 mpaka 20 kwa siku. Tunaiomba Serikali ipeleke pale Wodi ya Wazazi pamoja na *Theatre,* ili kusaidia mrundikano wa watu wengi wa Tabora Mjini wanaokwenda pale. Pale inakwenda Kata ya Chemchem, Kata ya Mbugani, Kata ya Tambukareli, Kata ya Ng'ambo, Kata ya Kanyenye, Kata ya Gongoni, ni kituo ambacho kinahudumia watu wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali yetu ya Wilaya ni nzuri lakini imejengwa pembezoni mwa Mji watu wa Mjini wanashindwa kwenda. Pia niongelee upungufu wa watumishi wa afya katika Mkoa mzima wa Tabora. Igunga tunatakiwa ikama yetu tuwe na watumishi 1,021, lakini tuna watumishi 386 tu unaweza ukaona tofauti ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Nzega *DC* watumishi 300, lakini tuna watumishi 172, Nzega *TC* watumishi 300, tuna watumishi 181. Hivyo hivyo, kwenye wilaya zote watumishi ni wachache sana tuna asilimia 60 ya upungufu wa watumishi kwa mkoa mzima ningeweza kutaja kote, lakini sitaji kwa

sababu ya tatizo la muda. Kwa hiyo, pia tulikuwa tunaomba Kituo cha Afya kijengwe Kata ya Kakola ambayo itahudumia watu wa Ikomwa, itahudumia watu wa Uyui na pale kuna Kituo kikubwa cha Reli ya *Stiegler's,* itasaidia sana hata mtu akipata ajali. Kwa sababu ni Kituo kikubwa cha Reli, basi itasaidia kuwatibu watu pamoja na watumishi. Kwa hiyo, tunaomba pale papatikane Kituo cha Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena niongelee suala zima la mgogoro wa ardhi. Kwenye Kata ya Mbugani pale Tabora kuna mgogoro wa ardhi wa muda mrefu sana tulishausemea sana humu Bungeni, baina ya Wanajeshi na raia wa pale toka mwaka 2016 mgogoro huu mpaka leo haujapatiwa majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara husika ikakae na wale Wanajeshi, ikae na wananchi pamoja na watu wote wa ardhi iamuliwe kama ile ardhi imeshachukuliwa na Jeshi basi wananchi hao walipwe fidia. Tabora kuna maeneo makubwa sana wapewe haki yao, wapewe fedha zao ili waweze kuendelea na maisha mengine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Nimemaliza, kengele ya kwanza au ya pili?

**NAIBU SPIKA:** Ya pili, malizia sekunde moja.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Mheshimiwa Rais ameshatoa maelekezo kwa Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Bashe nguo zake siku hizi ni magwanda ya Jeshi na tunaamini mambo yote yatakuwa mazuri.

Tunaendelea Mheshimiwa Kakoso, wajiandae Mheshimiwa Rweikiza na Mheshimiwa Muhongo Profesa. *(Makofi)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kupata nafasi hii. Kwanza, niipongeze Serikali kwa jitihada kubwa ambazo zinafanywa na Serikali yetu kwa kupeleka huduma muhimu za elimu, afya na maji na miundombinu kwa ujumla. Nataka nijikite kwenye eneo la Mradi wa Bandari ambao umewekezwa kwenye Wilaya ya Tanganyika, Mradi wa Bandari ya Kalema. Serikali imejenga Mradi wa Bandari ambao ni mkubwa na kimsingi tunayo fursa kubwa sana ambayo Serikali inaweza ikaipata pale ambapo tutafanya maboresho makubwa. Nchi ya *DRC* Kongo imejiunga na Umoja wa Afrika Mashariki, malengo ni kutaka kuitumia fursa ya soko la Afrika Mashariki. Sasa sisi kama Nchi ni vyema tukawa na uwekezaji mkubwa ili fursa iliyopo sasa, iweze kuwanufaisha wananchi wa Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa ile bandari hautakuwa na faida kama hatutakuwa na uwekezaji mkubwa na fursa ile itatumiwa na nchi jirani ambao wataichukua kama fursa muhimu. Niiombe sana Serikali ujenzi wa Bandari ya Kalema uende sambamba na uwekezaji wa ujenzi wa reli na uimarishaji wa reli ya kutoka Kaliua, Mpanda hadi Kalema. Sambamba na hilo ni lazima kuwe na mpango mkakati wa ujenzi wa barabara ya Kabungu hadi Kalema. Kwani, ile bandari itakapokuwa imekamilika kama hakutakuwa na miundombinu shirikishi ujenzi ule utakuwa hauna maana yoyote. Kwa hiyo, naomba na naishauri Serikali tuwekeze mradi ule uwe na matawi yake ya ujenzi wa reli na ujenzi wa barabara. Ni muhimu sana katika kuimarisha ushirikiano wa *East Africa* tufanye mipango na mikakati ambayo Serikali itaisimamia kuhakikisha Nchi ya Congo inatumia Bandari ile ya Kalema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kongo ni Nchi kubwa na ina madini na ina mzigo mkubwa sana ambao tukiutumia kwa Bandari ya Kalema na Bandari ya Kigoma tutakuwa na fursa

kubwa sana ya Bandari ya Dar es Salaam ikapata mzigo wa maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni suala la kilimo. Nchi yoyote ile inaendelea kwa kuwekeza kwenye kilimo, bila uwekezaji mkubwa wa Serikali kwenye kilimo hatutafanya kitu chochote cha maana. Naomba sana lazima Serikali ije na mpango mkakati wa uwekezaji kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji kitawasaidia watanzania wote na kitaimarisha uchumi kwa nchi yetu. Niiombe sana Serikali iwekeze kwenye kilimo cha kisasa tuwe na mabadiliko ambayo, yataanza kuepuka sasa kilimo cha kutegemea jembe la mkono. Sambamba na hilo ni muhimu kwa Serikali kuwekeza kwenye mbegu, tuwekeze kwa wataalam, lakini kubwa zaidi ni kuimarisha Vyama vya Ushirika. Kwenye Vyama vya Ushirika ndivyo vinavyoweza kumkomboa mkulima mdogo mdogo ambaye anaweza sasa kuwa kiunganishi na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji Serikali iangalie umuhimu wa kusogeza huduma za pembejeo. Bei za pembejeo ni kubwa sana kiasi kwamba Watanzania wanashindwa kumudu hizo bei. Niombe Serikali yetu iimarishe Mfumo wa kuleta pembejeo na kujenga viwanda vya pembejeo ambavyo vitasaidia kupunguza gharama. Sambamba na hilo ni kuimarisha masoko, mazao mengi ambayo yanalimwa masoko yake ni ya shida. Tutoe ukiritimba wa Serikali ambao mkulima akilima kwa jasho lake, wakati fulani huwa anaanza kupangiwa bei na kuzuiliwa mazao yake kutokupelekwa nje ya nchi. Hili tunaomba Serikali ilifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna ushauri kwa Serikali kwenye eneo la uvunaji wa hewa ya ukaa. Nchi yetu ina misitu mingi ambayo haijatumika vizuri, wenzetu wa nchi zingine wanatumia fursa ambayo ipo kwenye maeneo yao. Serikali ni vyema sasa ikaangalia Mfumo wa uwekezaji na kuwasogeza wawekezaji wanaokuja kuwekeza kwenye uvunaji wa hewa ya ukaa. Mataifa mengi duniani yanaharibu mazingira sisi tuna misitu ambayo inamilikiwa na Serikali za

vijiji, tuna misitu ambayo inamilikiwa na Halmashauri na misitu inayomilikiwa na Serikali Kuu. Katika maeneo haya ni vyema Waziri mwenye dhamana, akaja na mpango wa kubadili Sheria itakayonufaisha maeneo hayo yote yaweze kuvuna hewa ya ukaa. Kuna fedha nyingi sana ambazo tunazipoteza kama Taifa, eneo ambalo tuna Hifadhi za Serikali hawaruhusiwi kuvuna hewa ya ukaa. Sasa tukija na mabadiliko ya Sheria yatasaidia katika maeneo yote yaweze kuvuna hewa ya ukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwenye eneo hili ninaiomba Wizara ya Maliasili, mgogoro uliopo Wilaya ya Tanganyika kati ya *TAWA* na Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika waushughulikie ili wananchi waweze kunufaika kwani tayari tulishafanya mpango mkakati ambao utawawezesha wananchi kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika wapate fedha karibu zaidi ya Shilingi Bilioni Tano ambazo zitawanufaisha kwenye huduma zile za kimsingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie suala la barabara. Barabara inayotoka Mpanda kwenda Uvinza inayounganisha Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma, tunaomba Serikali iishughulikie na kuijenga ili iweze kuwa kiunganishi kwani ni barabara ambayo inaunganisha nchi na nchi, lakini kwenye maeneo haya tutakapokuwa tumejenga hii barabara Watanzania na nchi jirani watanufaika kwa sababu, miundombinu ndiyo inayoleta mazingira mazuri ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba na kuishauri Serikali mradi wetu wa maji wa Mkoa wa Katavi kutoa maji Ziwa Tanganyika kuja Makao Makuu ya Mkoa wa Katavi, tunaomba sana mradi huu ufanyiwe kazi ndani ya kipindi hiki kwani miradi mingi midogomidogo imekuwa haina tija na kwenye Mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi ndiyo mikoa ambayo haijanufaika, wanayaangalia maji ambayo yapo kwenye Ziwa Tanganyika bila kunufaika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Rweikiza, Mheshimiwa Muhongo, jiandae Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi nami nichangie katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Niseme kabisa kwamba, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imetuwekea misingi mizuri ya kupanua uchumi wetu na kuukuza kama nchi.

Mheshimiwa Naibu Sika, tunapozungumzia bajeti, tuko humu kwenye Bunge la Bajeti, tunazungumzia uchumi na uchumi imara ndiyo Taifa imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa nimshukuru Mheshimiwa Rais Samia kwa kuweka nguvu nyingi katika kukuza uchumi wetu. Nataka kuzungumzia suala la kilimo na majuzi hapa tumeona Mheshimiwa Samia, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pale kwenye mkutano uliofanyika katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete kazi aliyoifanya ni kubwa sana ya kuboresha kilimo chetu. Nampongeza na kumshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka nizungumzie suala mahsusi kuhusu kilimo. Kilimo tunasema ndio uti wa mgongo na kwa kweli ndio ukweli wenyewe, bado uchumi wetu mkubwa unategemea kilimo. Tuna maeneo nchi hii ambayo ni mazuri yana rutuba sana, wote mnayafahamu maeneo mbalimbali ukienda Morogoro Mkoa mzima una rutuba kubwa sana, ukienda maeneo ya Kusini kule Tunduru, ukienda Katavi, ukienda Rukwa, ukienda Kigoma, maeneo mbalimbali yote Kahama, kule wapi, kuna rutuba nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nchi hii tumejaliwa tuna mito mingi. Licha ya mvua tuliyonayo ya kutosha kumwagilia mashamba yetu vilevile kama kuna shida ya mashaka ya mvua tuna mito kwa hiyo, tuna uwezo wa kulima kwa

kutegemea umwagiliaji ambao sio wa gharama kubwa kwa sababu ya mito. Tuna mito kama Mto Mara, umeongelewa juzi hapa, tuna Mto Kagera, tuna Mto Pangani, tuna Mto Malagarasi, tuna Mto Ruvu, tuna Mto Ruvuma, kila mahali kuna mito mingi sana hiyo ni mikubwa. Iko mito midogo ambayo inaingia kwenye mito hiyo inapita maeneo ambayo nimeyataja yale ya ardhi ambayo ina rutuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninapozungumzia kilimo leo nataka nizungumzie maeneo haya. Kabla sijaenda kwenye maeneo hayo niseme kwamba, tuna vijana wengi nchi hii ambao hawana kazi, lazima niseme wazi. Hawana ajira, hawana kazi wanayoifanya, hawana biashara wapo tu, wengi sana. Ukienda Dar-es-Salaam ndio kabisa, ukienda pale Mwenge, ukienda Manzese, Tandika, Buguruni, Miji yote ukienda Mwanza, ukienda Arusha, wako vijana wanauza pipi, wanauza vitambaa vya jasho, siku hizi *charger* ndio zimekuwa *deal* ya kuuza *charger* kama vile zina uadimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hawa vijana wana nguvu, miaka 25 miaka 20 hawana ajira, lakini mimi nasema tuna ardhi nzuri sana maeneo mengi ya nchi hii. Nchi hii ina hekta karibu Milioni Moja haijalimwa zaidi ya nusu haijaguswa, sasa nikasema vijana tulionao nguvu kazi hii kubwa ambayo haitumiki, siyo tu kwamba tunapata hasara kutokutumia vijana hawa, vilevile ni hatari kubwa ambayo tumeiangalia, tunakaanayo hatuitumii ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nipendekeze hapa jambo mahsusi. Nataka nipendekeze na Serikali naomba jambo hili ilichukue tuanze kilimo cha makambi. Peleka vijana kwa mfano 200 kwa mfano kwenye kambi moja, tafuta eneo pale na mchango wangu huu unahusu Wizara nyingi sio huyu wa kilimo peke yake, Wizara nyingi zaidi ya kumi, iundwe *task force* ya Wizara zaidi ya kumi jambo hili lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, peleka vijana kwa mfano 200 nimesema kwenye kambi moja, wape mkopo, Serikali itafute fedha iwape mikopo ili wanapokwenda pale vijana

200, maana yake ni mbugani, porini, hakuna nyumba, wajenge nyumba za *full suit* za kuanzia, juu bati chini bati. Wapate *tractor,* ukitumia jembe la mkono unajidanganya haina tija na ni mateso, wapate ma-*tractor* angalao mawili, *power tiller* angalao mbili, wapate mbolea, wapate mbegu, wapate pembejeo mbalimbali. Chakula cha kuanzia angalao miezi sita, wanunue chakula na mahitaji mengine waanze pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya hesabu hapa za kirejareja, ukipeleka vijana 200 kwenye kambi ukawapa eka 2,000, ukawapa Milioni 200 kama mkopo wakaanza kulima kwa *tractor* ndani ya muda mfupi utapata mazao mengi sana na pesa nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema nimefanya mahesabu ya kukadiria hao watakaoundwa, kama itakuwa imeundwa hiyo KAMATI itafanya hesabu za uhakika, lakini ukiwapa vijana eka 2,000 vijana 200 wakaanza kulima kwa utaratibu watakaokubaliana wa kambi, wakaanza na mazao ya muda, maharage, mahindi, alizeti, ufuta, mpunga na mazao mengine ndani ya miezi mitatu, miezi minne, wataweza kuvuna mazao mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, wakilima mahindi wakapata eka moja magunia 20 kwa kiwango cha chini, ndani ya miezi mitatu wamevuna mahindi ya kutosha kuuza kupata fedha ya kutosha. Ndani ya mwaka mmoja wakilima misimu miwili, misimu mitatu, kama wanamwagilia maji watalipa lile deni, wataanza kujiendeleza. Pale palipokuwa kambi ya muda ya mabati ya *full suit* watajenga nyumba za kudumu, watajenga shule, zahanati, wataweka mitaa na maendeleo mengine, tutaongeza ajira, vijana hawa ambao wako Mijini wanazurura tutakuwa tumewaondoa tumeleta maendeleo makubwa, tutauza chakula hiki nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutauza Uarabuni ambao hawalimi lakini wanakula vizuri. Tutauza Congo, tutauza hapa Kaskazini kote kuna shida ya kilimo tutapata fedha nyingi na

vijana hawa tutakuwa tumewaondoa kwenye balaa ya kukosa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwangu Jimboni pale kuna vijana wanaendesha pikipiki bodaboda hizi wako nchi nzima. Kule vijijini unakuta kituo kidogo kina bodaboda 40, wanafanya kazi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, anakaa mpaka jioni hata abiria mmoja hampati anaondoka hana kipato. Wakiwa kwenye kambi ya kilimo hii baada ya mwaka mmoja wataweza kupata pesa hata kujilipa mshahara wa Shilingi Milioni Moja kwa mwezi, watajilipa watakuwa wamejiendeleza na watapata ufanisi mkubwa sana na nchi itapata chakula cha kutosha itaweza kuuza chakula hiki nje na kuboresha maisha ya Watanzania na kuboresha uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mchango wangu mimi ni huo kwamba, tufanye kilimo cha makambi ambacho kitaondoa baa la vijana kutokuwa na kazi, baa la kukosa chakula, amesema Mheshimiwa Mbunge hapa tunahangaika na mafuta, tukilima alizeti shida hii itakuwa imekwisha kwa wingi na tutapata mazao mengi sana. Nchi itaneemeka, hiyo mikopo italipwa na vijana itarudishwa Serikalini na tutakuwa tumepiga hatua ya maendeleo nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Muhongo, jiandae Mheshimiwa Esther Matiko na ajiandae Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kutoa shukrani kwa Serikali, Jimbo la Musoma Vijijini linaridhika sana

tunapata miradi na ni Jimbo pekee ambalo ukitaka mradi wako utekelezwe njoo Musoma Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani ya pili ni kwa Serikali kwamba, kuna wajanja-wajanja ambao hawakutekeleza miradi yetu vizuri sasa Serikali imeanza kutumia vyombo vyake kufanya uchunguzi. Nitoe pongezi Serikali kuamua kufanya uchunguzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani nyingine ni ya kufufua mradi ulioanzishwa na Mwalimu, wote wameongea hapa kilimo cha umwagiliaji na eneo ambalo Mwalimu alikuwa amelitenga mwaka 1973/1974 aanze kumwagilia kwa hekta 2,500 kule Bugwema natoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais alivyokuwa Musoma Vijijini tukamuomba kwamba, ule mradi uanze na ninadhani bajeti itakayosomwa ya kilimo itaelezea jinsi ambavyo Bugwema *Irrigation Scheme* itafufuliwa na ninadhani tutalisha Tanzania nzima na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mbali ya hayo ya Jimboni nije kwenye hoja ya Waziri Mkuu, ambayo naiunga mkono. Mimi nitaongelea sehemu mbili kuhusu sera na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sera. Kama Taifa inabidi tuwe na sera nzuri sana ya mambo ya utafiti, maendeleo ya utafiti na ubunifu *(Research Development and Innovation).* Yote tunayoyaongea haya tukitaka kufanikiwa lazima tuwekeze kwenye utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mwaka 2020 nchi ambayo ilitumia pesa nyingi kwenye utafiti ukilinganisha na *GDP* yao ni Belgium na Sweden, ndiyo zilitumia asilimia 3.5. Nchi za Kiafrika mwaka 2006 tulipitisha kule Sudan Azimio kwamba, angalau tutumie asilimia moja ya pato letu la Taifa kwenda kwenye utafiti. Nchi nyingi za Afrika hazijafika huko, waliokaribia ni *South Africa,* Kenya na Senegal na wako 0.8 Tanzania tuko 0.5. Kwa hiyo, ninaomba kwa ajili ya sera na ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu ndiyo inachukua kila sekta hii tuongeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hiyo 0.5 nadhani haijatoka kama ipasavyo, maana yake tukichukua *GDP* yetu kama sasa hivi ni Dola tuseme Bilioni 60. Ukichukua asilimia Moja ya hiyo, karibu ni Dola Milioni 650, ukichukua 0.5 ni zaidi karibu Dola Milioni 300, sidhani kwamba, tunatumia. Maeneo ambayo tunapaswa kuweka mkazo kwenye sera ya utafiti, nimechukua ni maeneo matano na Kiswahili chake wataalam watakuwa wanatafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza ni mambo ya *space science* na *technology.* Tunataka kilimo bora, lazima tujue mambo ya *space science.* Tunataka uvuvi, tunataka utalii, lazima twende kwenye *space science* na *technology.* Wengi wakisikia *space* wanadhani ni kitu kikubwa sana kinatisha, hapana! Tunahitaji kuwa na *satellites.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sikilizeni ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, Kenya wana *satellite,* Uganda watarusha moja mwaka huu, Zambia watarusha mwakani moja, Rwanda wanayo moja, *Egypt* wanazo tisa, Nigeria wanazo saba. Kwa hiyo, kwenye mpango wa utafiti na vyuo vyetu lazima tuanzishe *degree programs* ambazo zinajielekeza huko kwa sababu, *satellite* siyo kitu cha ajabu, tunahitaji kwenye mawasiliano na hata kwa mambo yetu ya hali ya hewa na madhara mengine ambayo yanaweza yakatupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni haya maeneo ninayoyataja karibu dunia nzima imeweka macho hapo ni *life sciences,* mambo ya kilimo, mambo ya mazingira, lazima tuwekeze kwenye *life sciences.*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni *nuclear sciences. Nuclear* siyo kwa ajili tu ya kutengeneza mabomu, lakini vifaa vingi sana vya hospitali vina *nuclear science* na *technology* ndani yake. Eneo hili hatujawekeza, lazima vijana wetu tuanze kuwasomesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la nne ni *environmental sciences.* Wengi wameongea, mazingira hata

yale ya Mto Mara tungekuwa na wataalam wengi yasingetupata yaliyotupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho la tano, kama tuna fedha zinatosha basi tuweke kwenye *artificial intelligence.* Hilo ndiyo eneo jipya ambalo tunakwenda, lakini tukitaka kufanya hayo pendekezo langu moja kubwa na ninaomba nilirudie ni lazima ile *COSTECH* ibadilike, *COSTECH* isiwe idara ndogo ni lazima tutengeneze kitu kinaitwa *National Research and Innovation. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ile *COSTECH* tuibadilishe iitwe *National Research Foundation and Innovation.* Mambo yetu yote tunayoyataka ya utafiti na wapate hizi fedha ambazo tunazipigia hesabu, Mamilioni ya Dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nilipenda kuchangia ni ajira. Wengine wote wameelekeza hukohuko kwamba, Tanzania kama tunataka kutoa ajira siyo ya kuajiriwa Serikalini, hatutaweza. Saa hizi tuko watu karibu Milioni 65 wanaoajiriwa hawajafika hata Milioni Moja, mahali ambapo watu wataajiriwa ni kwenye kilimo, kwenye uvuvi na ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huko tunakotaka kwenda ni kwa sababu sasa hivi duniani tuko watu karibu Bilioni Nane na hesabu imepigwa kila mwanadamu anahitaji chakula kwa siku kinachokwenda kwenye kilo 1.4. Kwa hiyo, tulime mazao ambayo tutaenda kuyauza huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia mazao yanayopendwa, vyakula vinavyopendwa duniani ni 12, nitavitaja kwa haraka haraka; *salad, chicken , cheese, rice tea, coffee, milk, eggs, apples, soup, yoghurt* na *bread.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ndivyo vyakula vinavyopendwa sana duniani. Vyakula vyote hivi tuwe na mpangilio wa kuzalisha kuuzia dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ili tufanye hivyo tunahitaji kuwa na kilimo cha umwagiliaji kama ambacho tutakuja kufanya kule Musoma Vijijini kwenye Bonde la Bugwema. Lile bonde ni kubwa ni zaidi ya hekta 10,000. Kwa hiyo, turudi pale Mwalimu alipotaka kuanzia, hebu tuanzie hekta 2,500 halafu viwanda tunavyovijenga ni lazima viwe viwanda ambavyo vimejiegemea sana kwenye mazao ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu tunaolima pamba tungetaka kuwa na *ginneries,* tulitaka kuwa na viwanda vya nguo, ambao tunafuga kama kule kwangu Musoma Vijijini na Mkoa wa Mara tunataka tena tuanze kuwa na viwanda vya maziwa na *cheese* na *butter* kama ambavyo dunia inahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukienda kwenye kilimo nashukuru sana hawa vijana wa magwanda kweli wanachapa kazi, lakini lazima tushindane na wakubwa. Nimechukua hapa takwimu zinaonesha namna ambavyo wale wakubwa wanalima na sisi tujaribu kwenda angalao hata asilimia 10 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukichukua mchele China inaongoza duniani inazalisha tani milioni 150, Tanzania tujipime.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimechukua ngano China ya kwanza. Karibu mazao mengi ni wachina.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hiyo ni kengele ya pili malizia kwa sekunde tatu.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sekunde tatu; ni kwamba, tujitahidi hata wanigeria tuwazidi kuvuna mihogo ambao wao wana tani milioni 60 sasa Tanzania angalau tufikishe tani milioni 40. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko, jiandae Mheshimiwa Waitara, na baada ya Waitara Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia fursa nami kuchangia kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza kwenye maeneo makuu mawili, ambayo migogoro ya ardhi pamoja na uwekezaji wa tija kwenye malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua kwamba wananchi wanakuwa wanatwaliwa maeneo yao aidha na mwekezaji au na idara mbalimbali za Serikali. Tumeshuhudia, mathalani mimi tangu niko Bunge la Kumi hapa naongelea mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wananchi wa Bugoth na Kenyambi kule Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho Wizara ya Fedha iliandika barua kwenda kwa Halmashauri ya Mji wa Tarime Novemba 18 ikiwaeleza kwamba wameshapokea tathmini kutoka kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na kwamba wanaenda kutoa fedha takriban bilioni 2.5 kwa ajili ya maeneo ya Tarime, Usule kule Tabora na eneo la Nyangurunguru Mwanza; ambapo kwa Tarime ni takriban bilioni 1.6. hata hivyo mpaka leo, walienda wakafanya tathmini na uhakiki wa mwisho na wakawaambia kufikia Februari watakuwa wamepeleka hela.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufuatilia kwa Katibu Mkuu Hazina na hata kwa mama yangu pale, Mheshimiwa Stergomena Tax, tukahakikishiwa kwamba kufikia Machi hela zitaenda, lakini mpaka leo wananchi wa Tarime, Bugosi na Kenyambi hawajapatiwa hela na wanapata adha kubwa. Kama mnavyowajua, wenzetu wa Jeshi la Wananchi, ukikatiza kwenye maeneo yale unapigwa unapewa adhabu kubwa. Ng'ombe wakijitokeza wakiingia wanapigwa faini kubwa, mpaka laki tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba, kwamba hawa Watanzania ambao wamezuiliwa kufanya uendelezaji wowote ule; kuanzia mwaka 2010 mpaka leo, walipwe fidia ili waende maeneo mengine wakafanye uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa ninasema hapa, kwamba kama wameshindwa kulipa fidia basi Jeshi hili lirudi kule Nyandoto ambako kulikuwa na kambi yake ili wale wananchi nao waendelee na uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuhusu uwekezaji wa *Barrick.* Kuna maeneo ambayo walifanyia tathmini kule Nyamongo, maeneo ya Nyamichele na kwingineko. Kwa mfano Nyamichele pale zaidi ya wananchi 2,000 mpaka leo waliwakatia mazao yao wakaonesha kwamba wanaenda kuwalipa lakini hawajawalipa mpaka leo, wale wananchi wanasubiria hawajaweza kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba, tunapokuwa tunatoa hizi ardhi basi tuhakikishe tunalipa fidia kwa stahiki kwa mujibu wa sheria inavyosema; msiendelee kuwatia umaskini, hawajiendelezi hamuwalipi hela wanakaa tu; ili waweze kwenda sehemu waweze kuzalisha na kuweza kuongeza tija kwenye taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine ni uwekezaji wa tija kwenye malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ambayo yanaanzia mwaka sifuri mpaka nane. Sote tunatambua kwamba mtoto hata ubongo wake unakuwa kwa asilimia 90 katika umri huu. Na nimesema niongelee hili hapa kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu ndio waratibu na wasimamizi wa *program* jumuishi ya miaka mitano ambayo mmeianzisha, na ambayo ndiyo ya mama; sasa nikasema niongee na nitanabaishe changamoto ambazo tunakutana nazo na ni vipi tutazitekeleza. Tusiishie kuwa na *document* tu, tuna *document* nzuri tunai-*document* lakini kiuhalisia *(in practiclal)* unakuta haifanyiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua kwamba watoto hawa umri wa miaka sifuri mpaka nane ni takriban

milioni 16.5, ambao ni kama 30% ya *population* tuliyonayo. Katika *program* hii inaeleza kwamba kumsaidia mtoto katika kumlea, kumlinda, kumuhudumia kupata elimu bora ya awali, kuwa na afya bora, lishe bora kuhakikisha kwamba hadumai na mengineyo. Kuanzia kwanza mama akiwa mjamzito mpaka anazaliwa anafikisha miaka nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa Tanzania ni tofauti kabisa. Sote tunatambua kabisa kwamba kama Serikali ingefanya uwekezaji wa tija kwenye eneo hili ina maana umeshamjengea huyu mtoto *foundation,* tunakuwa na rasilimaliwatu yenye tija ambao wanaenda kulijenga taifa kwa baadaye. Tusipowekeza katika *foundation* ya umri huu ina maana tutaendelea kuwa na Taifa ambalo kwa kweli hatutaona hata huo uchumi unatamalaki. Tutajiegeza aidha kwa kutegemea ma-*experts* kutoka sehemu nyingine; kwamba, hatutakuwa na watu ambao ni *analytical,* watu ambao wamepevuka na ubongo wao umekuzwa vizuri, hawajadumaa, hawajashambuliwa na magonjwa mbalimbali, wamepata elimu ya awali vizuri na wanaweza kuwa hivyo. Kwa hiyo ni lazima tuwekeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti mbalimbali zimefanyika na zinaonesha kwamba leo ukiwekeza dola moja kwa huyu mtoto au katika hizi *program* za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto faida yake au uzalishaji wake ni dola 17 za kimarekani. Lakini pia umeona kwa Watanzania zaidi ya asilimia 43 ya hao watoto hawafikii ukuaji timilifu, hawapati haya malezi kama yanavyotakikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia ukatili, mathalani nitatoa mfano kwenye ukatili tu, maana tunatakiwa tuwekeze kwenye lishe, elimu ya awali, kwenye kuhakikisha mtoto anahudumiwa vizuri na tuwekeze kwenye kumlinda; na naangalia hapa kwenye kumlinda na usalama wa huyu mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matukio ya kikatili dhidi ya watoto kwenye taifa letu ambayo yamekuwa ni mwendelezo. Nita-*site* tu mfano ambao nimeshuhudia kwa

wiki moja tu hii, na nitaanza jana kwenye Jimbo la Shinyanga Mjini la Waziri Patrobas pale. Kuna mtoto wa mwaka mmoja na miezi 18 amebakwa na baba wa kambo au baba yake mlezi. Amepelekwa hospitali Kambarage pale, wakapelekwa *Government Hospital* wakasema wakampa *referral* kwenda Bugando. Yule mtoto ameharibiwa kwa kutobolewa kote, mbele na nyuma. Inasikitisha sana! Inasikitisha sana! Mtoto wa mwaka mmoja na miezi kumi na moja!

Mheshimiwa Naibu Spika, na haya matukio ni mengi, mengine yanakuwa *reported* mengine si *reported*. Kama taifa huyu mtoto hata akipona atakuwa *affected* kisaikolojia. Sasa wako wangapi kama hawa kwenye taifa letu? Tunachukua hatua gani dhidi ya haya yanayoendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tena nilikuwa naangalia taarifa ya habari juzi kule Songea Shule ya Msingi Tembo Shujaa sijui kijana wa miaka 19 amebaka na kulawiti watoto wa Shule ya Msingi zaidi ya nane, wadogo! Lakini kuna siku tulikuwa tunapata semina hapa, dada yangu Jesca hayupo leo, kule Iringa watoto wadogo wamelawitiwa na kubakwa! Sasa *what are we doing?* Mnafanya nini? Yaani tunafanya nini kama taifa? Kwa sababu hata hizi sheria tunazoziweka mimi naona kama vile zinakuwa *loose. At a time* unafikiri hata hao watu wawe wanahasiwa kabisa *or even you remove that part* ili jamii iweze kukaa vizuri, kwa sababu *its unbecoming* kabisa kwa taifa; *its unbecoming.*

Mheshimiwa NaibU Spika, kwa hiyo *we end up documenting these things* lakini hamna *implementation so ever.* Inaumiza sana! Inaumiza sana kama taifa; na kama mzazi kwa kweli naumia; kwa sababu pia nina watoto wadogo wa kiume na wa kike huwezi kujua huko wanafanyiwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tumeshuhudia watoto hawa wananyanyasika wanauawa majumbani; yaani kuna mambo mengi sana. Mimi nafikiri tutafute *approach* nzuri ya kuhakikisha kwamba tunatatua hili tatizo. Tutafute *the better approach*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri yafuatayo; moja; Serikali kama imedhamiria kutekeleza huu mpango itenge bajeti ya kutosha na katika hizi bajeti najua kuna *settle means* ziko huku katika kila Wizara ihakikishe ina kifungu kidogo cha bajeti kwenye Wizara husika; Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya TAMISEMI yenyewe pamoja na Wizara ya Elimu Sayansi ya Teknolojia ili sasa tuweze kutekeleza kwa ukamilifu kwa kila mtu pale inapomgusa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine tuhakikishe basi kunakuwa na uratibu na usimamizi wenye tija kuhakikisha kwamba hawa watoto tunawalinda na wanakua kwa ktimilifu, yaani tusiishie ku-*document* ndugu zangu! naongea kwa ku-*bold!* Tukiishia ku-*document* hizi *paper* hatutafika popote pale tutakuwa na taifa ambalo limekuwa *affected* kisaikolojia, tutakuwa na taifa ambalo haliwezi kuzalisha kwa tija…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho dakika moja tu kwenye elimu ya awali ili watoto waweze kupata hizi elimu mbadala walimu ni wachache

**NAIBU SPIKA:** Haya, sekunde moja

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaleta kwa maandishi ahsante sana

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea sasa tunakwenda kwa Mheshimiwa Waitara. Nimeletewa taarifa hapa kuwa Jackson Kiswaga umeshachangia kwenye bajeti ya Waziri Mkuu.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika! Bado sijachangia.

**NAIBU SPIKA:** Alaa! Maana takwimu zinaonesha umeshachangia

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapana mimi sijachangia bado ndiyo leo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Kwanza namshukuru Mungu kupata fursa ya kusimama kwenye hili Bunge Tukufu kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu; na kuna mambo mawili yawekwe mstari vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapokuwa kiongozi wa Serikali unaisemea Serikali, unapokuwa Mbunge unasemea wananchi wako. Haya mambo mawili lazima yapigiwe mstari vizuri, la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo ameifanya, hasa katika Mkoa wa Mara, ndio mkoa ambao hauna Hospitali ya Rufaa sasa kwangu inaendelea kujengwa, watu wetu wataishia pale Musoma hawataenda Bugando. Vilevile Musoma kulikuwa na shida ya uwanja wa ndege kwa muda mrefu, ametoa fedha nyingi mkandarasi yupo *site,* tutapata huduma ya ndege pale katika Mkoa wa Mara. Mheshimiwa Rais pia ametoa fedha katika majengo yetu ya mkoa, na tunamshukuru sana tunaomba aendelee kufanya hivyo kwa sababu Mkoa wa Mara kwa kweli kwa hadhi yake na heshima kubwa ungeweza ufanane na hadhi ya Mwalimu Nyerere, lakini kuna mapungufu ya hapa na pale ambayo naamini kwamba yataendelea kutekelezwa kadri ambavyo Wabunge wenzangu wataendelea kuleta maoni ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwamba, kule Tarime tuna barabara yetu ya Tarime - Mugumu - Serengeti yenye urefu kilometa 86; nimeambiwa hivi asubuhi kwamba kuna mkataba angalau

kilometa 25 kutoka pale Mgabili mpaka Nyamongo watajenga. Huu utakuwa ni mkombozi mkubwa sana katika eneo hili. Tuombe aendelee kutoa fedha ili tuweze kupata miundombinu watu wetu waweze kufanya kazi ya kuhudumiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze mambo maalum katika Jimbo la Tarime Vijijini, na hili ni jimbo maalum ndiyo maana kuna kanda maalum. Sasa ondoa mawazo ya polisi, tuje kwenye huduma za kijamii, maliasili na ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimuomba Waziri akiwepo Mheshimiwa Ndumbaro tangu mwaka 2020 aende kule Tarime kwenye kata ya Nyanungu, Kwihancha, Korongo na Nyarugoba hakwenda; lakini namshukuru Mheshimiwa Rais aliunda kamati ya Mawaziri wanane wakazunguka walienda wakaishia Musoma Mjini pale kwangu hawakufika, lakini wakanipa idadi na orodha ya vijiji ambavyo Mheshimiwa Rais ametoa kibali kwamba wananchi wale watapata eneo angalau la kuchunga na kutoa huduma kwa mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niliomba kwamba mambo haya, na nimewasiliana na wenzangu wa Mkoa wa Mara, watu wa Serengeti, Mbunge wa Serengeti, Mbunge wa Bunda na mimi Tarime Vijijini; kwamba maeneo haya kuna malalamiko ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo *GN* ya mwaka 1968 ambayo wananchi wenyewe wanajua wapi kuna *beacon* na wapi hakuna *beacon;* na kumekuwa na ugomvi wa muda mrefu katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais ametoa maamuzi ya kutoa baadhi ya maeneo yaende kwa wananchi, lakini bahati mbaya; mimi ninapozungumza hapa nimeona juzi Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Naibu Waziri wa Maliasili walikuwa Musoma na wakatoa tamko, nikauliza wenzangu kikao kinachoendelea mmeshirikishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, niliposema kwamba nendeni kule *site* na nikatoa hoja kwa Mheshimiwa Rais alipokuja tarehe tano Februari kule Musoma nikazungumza habari hii ya hifadhi ya Serengeti na malalamiko yaliyopo ya muda mrefu yaondolewe ili sisi Wabunge tupate amani na kuwa na mahusiano kati ya wananchi na Hifadhi ya Serengeti; kwa sababu pia inalazimika kutoa huduma kwa watu ambao wanazunguka pale kwenye mambo ya usalama na kwa ajili ya rasilimali za taifa na yeyote anayekwenda katika eneo lile. Kazi hiyo haikufanyika.

Sasa badala yake wametoka watu hapa Wizara hizi mbili wameenda kule Tarime, Serengeti, Nyamongo, Kwihancha, Gorong'a pamoja na Nyanungu; na wananchi wamenipigia simu kwamba sasa wanakagua mipaka ile. Kule Kwihancha ambako tulisema waende hakuna shida kwa sababu wananchi wameonesha *beacon* na wamekubaliana na wapimaji na watu wa hifadhi ya Serengeti. Lakini Gorong'a na Nyanungu wameenda kuonesha *beacon* juu ya mlima ambako kuna vijiji ambako kuna vijiji vya watu. Sasa wananchi wanauliza Mbunge anajua? Mbunge sijui.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kilichoniuma ni kwamba wamekwenda Nyanungu ambako mimi ndiyo Mbunge, watu wamenipigia kura, nikawaahidi wakati wa uchaguzi kwamba nitawatetea na Mheshimiwa Rais amekubali kutenga eneo mchunge. Sasa wale watu wameambiwa kwamba Mbunge wenu ameshirikishwa ingawa hapa hayupo; na ni uongo.

Sasa *imagine;* pale Ilala pale kwenye Bonde la mto Msimbazi wanaenda kuhamisha watu unaambiwa umeshirikishwa na hukushirikishwa. Kwa nini Waheshimiwa viongozi tunategeana mabomu njiani? Hizi ni ajali! Kwa sababu unaweza kutoa taarifa za uongo kabisa katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Waziri wa Ardhi twende na Wabunge wa Mkoa wa Mara wenye migogoro, twende tukae na wananchi wetu. Hamuwezi kwenda peke yenu kule mnawapa taarifa za

uongo, halafu nikitoka Bungeni nikafanye kesi. Mimi si dhaifu kiasi hicho; sitafanya biashara hiyo, tutagombana. Tunataka twende sawasawa pamoja. Kama kuna jambo lipo, Mbunge ameleta Bungeni Waziri amshirikishe Mbunge ampe na *background,* wapange ratiba waende, kuna haraka gani katika jambo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba, na hili uwe ni ujumbe kwa Waheshimiwa Mawaziri, sina ugomvi nao mimi, ninachosema, Mawaziri hawa tunaweza kuwatengenezea shughuli nzuri Wabunge wakashinda wakae hapa *comfortably,* lakini kwenda kutoa taarifa ya uongo halafu unasema Mkoa wa Mara unaongoza kuvamia maeneo; sasa hiyo taarifa mmejadili na nani? Unakuta Mwenyekiti wa Kijiji ambaye hawezi ku-*argue,* unaongea naye halafu unauliza Mbunge niambie, mimi nipo Dodoma nyie mpo huko Tarime Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba hili kweli lifanyiwe kazi vizuri, na iwe ni maeneo yote tushirikishane tu kuna ugomvi gani? Bora nialikwe hata nisihudhurie; lakini sijashirikishwa, watu wanaambiwa Mbunge wenu ameambiwa mnaniwekea bomu hilo ambalo nitakubali tulipukiwe wote siyo mimi peke yangu...

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa madini na mazingira, na hapa naomba Waziri wa Madini na Waziri wa Ardhi na Mazingira wanisikilize vizuri. Katika Jimbo la Tarime Vijijini eneo la Nyamongo kuna malalamiko ya muda mrefu sana, na ni malalamiko ambayo ni *very genuine,* yanaonekana kwa macho. Nataka nisema, tunayo changamoto ya maji machafu, ni malalamiko ya muda mrefu, tunayo changamoto miradi ya maendeleo, tuna changanoto ya fidia katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Murwambe, Kumalela, Nyamichele tangu mwaka 2012 watu waliahidiwa hawajalipwa nitaomba watu hawa, mgodi umeagiza kulipa tumeongea na Rais wa *Barrick* duniani wamekubali kulipa naomba haya mambo yafanyiwe kazi.

Lakini ningetaka nisema kwenye miradi hii ya *CSR,* kengele imegonga ya kwanza. Miradi ya *CSR* nataka niulize Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI anisaidie. Hivi, mimi ni Mbunge, nilikuwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Naibu Waziri wa Muungano na Mazingira, Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Mbunge wa kipindi cha pili, mwanasiasa wa siku nyingi, nimekaa na Halmashauri yangu, tumejadili mipango ambayo ninayo hapa, ambayo inatoa kero Nyamwaga hospitali, maji Nyamongo na vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeuandikia na mgodi *correspondences* nyingi tukajibiwa, tumeandika tumepeleka TAMISEMI tukajibizana na Profesa Shemdoe, tukajibiwa, barua imetoka imeenda Wizara ya Fedha tukajibizana Tutuba tukakubaliana. Tunataka fedha iende kwenye miradi ya maendeleo. Wako akinamama pale Nyamwaga wanajifungulia barabarani kwa sababu wodi haijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo kule Nyamongo hii ripoti ya Jafo ya maji machafu imeharibu hali ya hewa kwa sababu watu wanaogopa kunywa maji na kula Samaki, lakini kwenye fedha hiyo ya *CSR* kuna fedha milioni 900 mgodi wamekubali kutoa maji kwenye chanzo chao, maji yaende pale Kewanja na Nyangoto ili wapate maji. Hizo fedha Mkuu wa Mkoa peke yake ambaye ni mgeni Mkoa wa Mara amekuja ameandika barua kwenda Wizara ya Fedha amezuia fedha zote. Angalia, Mbunge amekaa Halmashauri imekaa, TAMISEMI imeandika, Fedha imeandikwa, Mkuu wa Mkoa bosi mkubwa ameandika barua peke yake miradi sasa imerudishwa Tarime wakajadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Serikali za Mitaa ninayo hapa inaeleza Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya wata-*facilitate* na watengeneze mazingira mazuri kuboresha miradi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge nimekuja hapa nazungumza habari ya fedha iende kule yeye amezuia. Nataka niambiwe utaratibu ukoje? Yaani Baraza la Madiwani limepitisha, sasa huyu mtu mmoja anazuiaje? *Afterall* fedha

ya *CSR* hii fedha wala hatupewi *cash,* tunakaa kwenye vijiji. Kwa mara ya kwanza Tarime baada ya kuwa Mbunge fedha hii ilikuwa inasaidia vijiji 11 tu kati ya vijiji 88; tumekaa na Wenyeviti wa Vijiji, Madiwani wa Kata 26 bila kubaguana vyama, tukakubaliana sisi tufanye kazi ya Tarime Vijijini tupunguze malalamiko na kero, wakaridhia kila kijiji, kila kata ina mradi huu. Ningeomba nielezwe tukileta mipango kwenye halmashauri yetu inakuwa kuwaje tunakwamishana njiani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili hiyo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Rais anafanyakazi nzuri naomba viongozi wengine aliowateua wamsaidie, Wabunge mliopo humu mtarudi hapa Bungeni kama kazi nzuri inafanyika kwenye majimbo yenu tushirikishane baada ya kuyasema hayo.... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya! Ahsante Mheshimiwa Waitara, lakini Mheshimiwa Waitara wewe ulikuwa Naibu Waziri wa Mazingira na ulikuwa unakwenda kwenye migodi wala Wabunge wenzio huwaambii, na umemaliza ukaenda huko Uchukuzi, unakwenda huko unakagua huwaambii, lakini hoja yako ni ya msingi; kwamba Mawaziri mkienda huko muambizane haya bwana lakini habari ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Kiswaga, jiandae Mheshimiwa Khalifa Mohamed.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Waziri Mkuu. Kwanza napenda kukupa taarifa pia, mimi humu ndani najuiliakana kama Chifu Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga. Sasa nimeshangaa kwamba sijachangia, lakini umejua nimechangia, lakini nafiri ni *error* kidogo. Yupo Kiswaga mwingine, lakini humu ninajulikana kama Chifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza nimshukuru sana Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, hata Jimbo langu limefaidika sana katika kipindi cha mwaka mmoja ambapo Rais huyu ameingia madarakani. Pongezi hizo zinakwenda kwanza kwa kuwa nimeweza kupokea fedha, na kulikuwa kuna kilio kikubwa katika Kata ya Ifunda kwenda Lumuli, watu walikuwa wanashindwa kuvuka wakati wa mvua, lakini kwa fedha za dharura nimepokea kama shilingi milioni 900, tumeshaweza kutengeneza daraja pamoja na kivuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru kwa sababu nimeweza kupokea shilingi milioni 500, tunajenga Kituo cha Afya pale Kiwele; pia nimepokea shilingi milioni 446, tumeunganisha Kijiji cha Mlanda pamoja na Magulilo ambapo ilikuwa ni shida sana kuvuka. Vile vile nimepokea shilingi milioni 470 kwa ajili ya kujenga Shule ya Sekondari pale Luhota. Pia nimepokea kiasi cha shilingi bilioni moja kutoka kwenye Mfuko wa UVIKO kwa ajili ya madarasa. Kwenye UVIKO pia nimepokea shilingi milioni 500 ambazo zinakwenda kwenye maji pale Magulilo Kijiji cha Nega ‘B’. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yametekelezeka, kwa hiyo, nimeona nami niweze kumpongeza. Nilikuwa najaribu kuangalia mambo haya mengi yamefanyika kwa muda mfupi Rais huyu akiwa mwanamama, nasi akina baba tulikuwepo, hatukuweza kufanya haraka haraka namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia dunia kwa ujumla wake, nikaona kwamba wanawake huwa hawapati nafasi sana za kiutawala. Nikiangalia katika mataifa makubwa, kwa mfano, Uingereza, tangu mwaka 1801 kumekuwa na Mawaziri Wakuu 55, lakini kumekuwa na wanawake wawili tu; alikuwepo Margaret Thatcher na baadaye akaja Theresa May. Huyu mama, Margaret Thatcher ambaye alikuwa mwanamke wa chuma, alifanya kazi kubwa sana za kuinua uchumi katika Taifa lile; na ndiye Waziri Mkuu peke yake aliyetawala muda mrefu na tunaamimi na Mama huyu atatawala muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikwenda pale Ujerumani nikaona kumekuwa kuna ma-*chancellor* 33 tangu mwaka 1867, lakini ni mwanamke mmoja tu anaitwa *Chancellor Angela Merkel,* ametawala kwa miaka 16, kwa muda mrefu baada ya *Chancellor* yule mwanzilishi ambaye alikuwa *Otto Von Bismarck.* Kwa hiyo, wanawake wanafanya kazi kubwa katika dunia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikija kwenye hoja baada ya kutoa hiyo shukrani, ni kwamba katika Hotuba ya Waziri Mkuu imekuwa ikieleza mambo mengi; inaeleza mipango ya maendeleo katika maeneo mbalimbali na inagusa miundombinu na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikielekea kule kwangu, Jimbo la Kalenga na Mkoa wa Iringa kwa ujumla tuna mambo ambayo tulikuwa tukitamani Serikali iweze kufanya. Kwa mfano, kwenye upande wa miundombinu, tuna barabara mbili muhimu sana na nyingine za kiuchumi. Ukiangalia ile barabara inayotoka Iringa kupita Kalenga ikaenda kule *Ruaha National Park* kwa ndugu yangu Mheshimiwa Lukuvi, na ile barabara inayotoka Iringa, inapita Jimboni kwangu inaenda kule Kilolo, barabara hizi tumezizungumza mara nyingi, lakini tunaendelea kusisitiza kwa sababu zina umuhimu mkubwa sana katika uchumi wa Mkoa wa Iringa na kwa Taifa kwa ujumla kwa sababu zinakwenda katika maeneo yenye Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nimefanya vikao na Afisa Mtendaji Mkuu wa *TANROADS,* amenipa matumaini. Ameniambia hii barabara ya kutoka Iringa kwenda Kilolo tutaanza pengine mwezi wa Saba kwenye bajeti ya *RISE*; tunaomba hilo litekelezeke. Pia amenipa taarifa kwamba barabara ya kwenda *Ruaha National Park,* mazungumzo yanaendelea na *World Bank,* pengine tunaweza tukasaini mkataba mwezi wa sita na ujenzi ukaendelea.

Kwa hiyo, tunaomba haya mambo yatekelezeke ili Mkoa wa Iringa uweze kufunguka na uchumi uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana *TARURA* kwa kazi kubwa ambazo wanaendelea kuzifanya. Bajeti tumeongezewa kwenye Jimbo langu na kwenye maeneo mengine ya Taifa. Changamoto kubwa tulizonazo katika kutengeneza miundombinu ya barabara za vijijini, tumekuwa hatutengi bajeti vizuri kwa ajili ya mifereji pamoja na makalati. Hilo limekuwa ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali na *TARURA* kwa ujumla, tunapokwenda kuweka hizi bajeti, tuzingatie sana makalavati pamoja na madaraja madogo madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia *CEO* wa *TARURA,* ndugu yangu Seif, nimefanya naye vikao kadha wa kadha na amenihakikishia kwamba mwaka huu katika Mradi wa *RISE* vijijini, tutakwenda kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka pale Uwenda, ikatokeze Mgama kilometa 19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba hilo litekelezwe kama tulivyoongea ili sasa tuweze kuomba mahitaji mengine. Kwa mfano, barabara inayotoka Kalenga kwenda Mafinga kupita Wasa, kupita Maboga, ni barabara muhimu sana ambayo kama mkoa tunaweza kuitumia kama njia mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna changamoto kubwa sana kwenye nchi yetu, maeneo mengi hayana barabara mbadala. Kwa hiyo, ikitoka kama *jam* au ajali njiani, unakuta kwamba kunakuwa na ucheleweshaji mkubwa. Kwa hiyo, kama tukitengeneza hii barabara ya Kalenga, ikaingia Uwasa, ikatokea Mafinga itakuwa ni njia mbadala ya Mkoa ili hata ikitokea tatizo, tunaweza kuitumia. Yale mazungumzo nimeshaanza kufanya na *TANROAD* na *TARURA,* tumekubaliana kwamba tutaitembelea. Naomba hii iingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge ili ije itekelezwe baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, Serikali imekuwa ikifanya kazi nzuri sana kwenye miundombinu ya elimu na madarasa mengi tumejenga lakini changamoto

kubwa ambayo tunayo ni upungufu wa walimu na mabweni. Tunatamani sana sasa Serikali ijielekeze kwanza kukarabati shule kongwe. Tuna shule kongwe nyingi ambazo zimejengwa tangu miaka 1970 na kuendelea, ambazo zimechakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna upungufu wa walimu. Kwa mfano, *weekend* nilikuwa Jimboni, nimekuwa vijiji vya Nega 'B' na vijiji vya Mlanda. Kijiji cha Nega 'B' Shule ya Msingi ina walimu watano. Mfano tu natolea, Mlanda Shule ya Msingi ina walimu saba. Kwa hiyo, naomba Serikali sasa iweke nguvu katika kupeleka walimu kwenye shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ujenzi wa vyoo; ukiangalia tumepewa fedha kwenye vituo shikizi. Hivi vituo shikizi vimekuja bila fedha ya choo. Kwa hiyo, hilo nalo tuliangalie kwenye bajeti zetu, maana kuna Halmashauri nyingi ambazo hazina uwezo. Hilo tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tukija kwenye Afya, sera yetu inasema kwamba tutakuwa na zahanati kila Kijiji, na nguvu za wananchi zimekuwa zikitumika maeneo mbalimbali, na tuna vijiji vingi ambavyo tayari vimeshakamilisha maboma. Kwa mfano, nilikuwa Ndiwili Jumamosi, wameshakamilisha boma, lakini bado hawajaezeka. Sasa Serikali lazima iwaunge mkono mara moja ili sasa nao waweze kufurahia ile kazi yao ambayo wanaifanya na Serikali kuwaunga mkono kwa haraka. Hata pale Nega 'B' tayari wameshakamilisha boma lakini bado hatujaweza kuwakamilishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwa upande wa vituo vya afya, ni kweli tunayo sera ambayo inasema tuwe na vituo vya afya kila kata. Sasa kazi kubwa imefanyika. Kwa mfano, Jimbo la Kalenga lina vituo vitatu ambavyo vimekamilika. Kwa mfano, kituo cha Nzihi ni cha siku nyingi lakini hakina *wards.* Kwa hiyo, hiyo ni changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ukienda kwa mfano Kituo cha Mgama; pale Mgama wananchi wameshaweka

msingi kwenye kujenga wodi kwa ajili ya akina baba na akina mama, lakini miaka karibu minne hakijamalizika. Kwa hiyo, naomba Serikali kwenye bajeti zake sasa ikamilishe hivi vituo vya zamani ukiacha hivi vipya ambavyo tunavileta ili sasa na wananchi waweze kuifurahia Serikali yao kwa kazi kubwa ambayo inafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambazo nilipenda pia kuzungumzia ni kwenye upande wa umeme. Serikali imeagiza kwamba ifikapo mwezi wa 12 tuwe tumemaliza umeme kwenye vitongoji vyetu vyote, lakini nikiangalia kasi tunayokwendanayo sasa, bado tupo nyuma sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja, mengine nitaandika kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Khalifa Mohamed jiandae Mheshimiwa Yahya Mhata.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Mwenye Mungu Mtukufu kwa kutujalia uzima na afya katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan na kuweza kutekeleza nguzo hii muhimu katika dini ya Uislam. Pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mchana huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii haiwezi kupita bure kama sikumshukuru sana Mama yetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Samia kwa kweli amekijaa kiti chake na amekuwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kujali siasa, itikadi za vyama, wapinzani na chama Tawala. Kwa hiyo, Mheshimiwa

anakusudia, na ni dhamira ambayo tunaiona wazi kabisa ya kuliunganisha Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sasa nimekuwa mshabiki wake mkubwa wa kusikiliza hotuba zake. Ninafuatilia ratiba zake, nafuatilia hotuba zake. Hotuba zake zote zinaonesha anataka kuiunganisha nchi, na anazungumzia utengamano wa wananchi wote bila kujali itikadi zao. Hivyo basi, mfano mkubwa katika kipindi kifupi cha mwaka mmoja hiki, Mheshimiwa Rais ameshakutana na viongozi wa vyama vya upinzani. Pia karibuni hivi, alikuwa katika Mkutano wa *TSD;* karibuni pia alikuwa akipokea taarifa ya kikosi kazi ambacho amekiunda na ameyakaribisha mapendekezo yote kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba wasaidizi wake wasimwangushe. Nia njema hii ambayo Mheshimiwa Rais ameionesha ya kuliunganisha Taifa, basi taifa hili ni letu sote, tuna tofauti ya mawazo yaheshimiwe, naye ndiyo mwelekeo anakwenda nao. Kwa hiyo, ningetoa tena wito kwa wasaidizi wake Mawaziri, wamsaidie kutufikisha pale ambapo tunataka. Tuna mambo mengi kwa sababu mapendekezo yanakusanywa, anapelekewa. Sina haja ya kwenda huko, najua kuna muda mfupi wa kutekeleza mambo, kuna muda wa kati na kuna muda mrefu. Kwa hiyo, tuwaachie mambo haya yachakatwe yapelekwe ili yatolewe maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuondoka hapo, nami nipate fursa ya kuzungumzia hali ya maisha ya wananchi kwa ujumla. Kwa kweli hili halitaki tochi, halitaki taa ya mwangaza mkali wa kuona hali halisi ya maisha ya wananchi wetu. Kwa kweli *purchasing power* ya wananchi imepungua sana kwa sababu mifumuko hii ya bei ya vitu mbalimbali na upandaji wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya utafiti mdogo katika masoko yetu haya hapa Dodoma ambapo mahitaji yetu mengi tunakwenda kuchukua. Utavikuta vitu vipo kwa wingi sana katika masoko; ukitaka vyakula vya maganda hivi,

mboga mboga, matunda na bidhaa nyingine, lakini ukimwuliza muuzaji, atakwambia unaweza ukakaa kutwa nzima ukauza shilingi 2,000/= au shlingi 3,000/=. Watu wanavitaka vitu, lakini bei ni kubwa na mifukoni kunakuwa hamna kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili jambo ni la kuzingatiwa mno. Biongozi wetu na wataalam wetu wakae waone kwa namna gani watamnusuru huyu mwananchi hasa wa kipato cha chini kuweza kumudu maisha yake na kipato chake na chakula chake walau cha siku nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo nizungumzie hali ya UKIMWI katika nchi, kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati yako ya Mambo ya UKIMWI, Dawa za Kulevya, Magonjwa yasiyoambukiza pamoja na *TB*. Kwa kweli hali ya UKIMWI katika nchi yetu, bado UKIMWI upo katika nchi na wananchi waelewe UKIMWI bado ndio ule ule unaua. Kwa hiyo, ipo haja ya Serikali, wananchi na jamii kwa jumla kuweza kupiga vita hivi ili tuweze kuvishinda walau tumudu kutokupata maambukizi mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inakisiwa tu, na mpaka takwimu za Desemba, 2020 tuna watu ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI karibia 1,700,000, ingawa ukiangalia *trend* ile toka miaka ya 2004 huko mpaka sasa, ile graph linakuwa *declined,* linapungua pungua yale maambukizi mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kuna rika muhimu kweli kweli ambalo linapata maambukizi mapya. Hili ni *group* la vijana wetu ambao wana umri kuanzia miaka 15 mpaka 24. Vijana hawa wanachangia asilimia 40 ya watu wote ambao wana maambukizi. Katika vijana ambao wana umri huo, vijana wa kike kwa asilimia 80 katika maambukizi hayo, wao wanaongoza vijana wasichana; na hao wasichana katika *group* hili ndio ambao wapo katika vyuo vikuu, wapo katika Shule za Sekondari nakadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasichana hawa ndio *target* kubwa ya wanaume wakwera, Mheshimiwa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya UKIMWI ana neno lake analitumia kwa hawa wanaume ambao wanawanyemelea vijana hawa. Ukiangalia, ni dhahiri kwamba hata hapa Dodoma ukifuata nyendo fulani fulani hivi unaweza kuona vijana hawa wadogo ndio ambao wameingia katika ushawishi huu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajumbe wenzangu wa kamati hii ya mambo ya UKIMWI tulipokuwa katika ziara ya kukagua maendeleo, tulikuwa katika mkoa mmoja huko sitaki niutaje, lakini walipokwenda kufanya utafiti katika maeneo yao, walikaribishwa pale. Ajabu ni kwamba, unapewa *option;* walipofika wakapewa *option,* kama unataka kula ndizi na ganda lake au unataka ule ndizi ganda ukiwa umelitoa? Kwa hiyo, kuna viwango; ukitaka ule na ganda lake, basi ni shilingi 10,000/=, lakini ukitaka ulitoe lile ganda, basi kuna shilingi 15,000/=. Kwa hiyo, hii ni hatari ambayo Serikali pamoja na jamii na wazee, lazima tushirikiane tuwalinde vijana hawa. Hawa vijana ni wetu na kwa kweli tusi... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Hiyo ya pili, malizia sekunde moja.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa ufupi mimi niseme tu kwamba kuna magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza pia, ni janga, kwa hiyo...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Yahya Mhata, jiandae, Mheshimiwa Bupe, atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Ulenge.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehrma ambaye ameniwezesha leo hii kusimama mbele ya Bunge lako hili

Tukufu kuchangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Pia naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nampongeza sana Waziri Mkuu na watendaji wote wa Ofisi yake ambao wameshiriki kwa njia moja au nyingine kufanikisha bajeti hii. Naomba nijielekeze katika Kilimo. Mimi natoka Jimbo la Nanyumbu. Ndani ya Jimbo langu, Korosho ndiyo uti wa mgongo wa wananchi wa Jimbo langu. Karibu asilimia 95 ya wananchi wanategemea zao hili la Korosho, hivyo naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri mwenye dhamana na Kilimo kwa kazi nzuri anayoifanya kuhakikisha kwamba zao hili la Korosho linasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2021 sisi ni mashahidi, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ilitoa pembejeo bure kwa wananchi wote wanaolima zao la Korosho. Wananchi wa Jimbo langu walinufaika sana, kwa hili nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshmiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, mwaka huu Waziri mwenye dhamana ametangaza kwamba wananchi wote watakaolima Korosho ndani ya Jimbo la Nanyumbu watapata pembejeo bure kama ilivyo mwaka 2021. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili naipongeza sana Serikali kwa kuhakikisha kwamba Maafisa Ugani walioko ndani ya wilaya yetu wanapewa vitendea kazi. Sisi ni mashahidi, karibu pikipiki 7000 zimetolewa na naamini kabisa lengo ni kuhakikisha kwamba kilimo kinasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, tumeona Serikali imeongeza mitaji katika Benki ya Kilimo, Benki ya Kilimo iliyoanzishwa mwaka 2012 ilikuwa na mtaji na bilioni 60, Serikali imeongeza karibu bilioni 208, lakini Mfuko ule wa Ufaransa

wa Maendeleo umeongeza karibu bilioni 210. Kwa hiyo kuna fedha nyingi ndani ya benki hii ambazo zina lengo kubwa la kuhakikisha kilimo chetu kinasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye korosho ili tuweze kuzalisha zaidi sio suala la pembejeo na viatilifu peke yake, kwa sababu ili korosho uweze kuvuna unahitaji kupalilia korosho. Katika hali ya kawaida, mkulima wa kawaida, hana uwezo wa kupalilia hekari 10 yeye mwenyewe kwa hiyo lazima ataajiri vibarua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika korosho ili uweze kupata tija kupata mavuno mazuri, lazima upulizie korosho, unahitaji mabomba ya kupulizia, mafuta ya petroli, vibarua wa kukusaidia kupulizia, kwa sababu korosho una amka kati ya saa 8 usiku na saa 10 alfajiri kwenda kupulizia korosho, kwa hiyo lazima uajiri watu wa kukusaidia kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ili upate mavuno mazuri lazima uwe na vibarua wa kuokota korosho zako, debe moja la korosho tunaokota kwa sh.1,500, lakini pia korosho unahitaji watu wa kukusaidia kuhamisha kutoka shambani na kupeleka nyumbani.

Kwa hiyo vitu vyote hivi vinahitaji fedha. Sasa Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa kwamba kuna benki ambayo ya kumsaidia mkulima, naomba nitoe ushauri, wakulima hawa wapewe mikopo haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuwapa mikopo hii pembejeo na viatilifu itakuwa kazi bure kwa sababu mikorosho itakuwa porini watashindwa kupalilia, watashindwa kupulizia, watashindwa kuokota, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe benki zetu *CRDB, NMB*, zinatoa mikopo kwa wakulima ili waweze kuzalisha kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana kwa utaratibu huu huu wananchi walizalisha na Mheshimiwa Waziri ni shahidi, zaidi ya tani 26,000 zilizoongezeka, lakini bei ya korosho ilikuwa ndogo kuliko miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha aeleze ni mambo gani yaliyosababisha bei ya korosho kuteremka na je, wananchi wanaambiwaje kuhakikisha kwamba msimu ujao bei itakuwa nzuri. Mambo haya tusipoyafanya tunaweza kuwavunja nguvu wakulima wetu, kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, hili ni jambo ndani ya wilaya yangu. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri aliliingilia kati lakini bado halina ufanisi. Msimu umefungwa wakulima wa jimbo langu bado wanaidai Serikali, bado wanavidai vyama vya *MAMCU* zaidi ya sh.26,000,000, korosho wameuza, wamepeleka mnadani, mnada umefanyika, lakini wakulima bado hawajalipwa fedha zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametoa agizo kwamba walipwe ndani ya wiki moja. Nashukuru tutafuatilia kwa pamoja kuhakikisha wakulima wale wanalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ahadi ya viongozi wakuu; viongozi hawa wetu wanapokuja katika majimbo yetu wanatoa ahadi. Naomba sana ahadi hizi ziwe *documented* lakini zitekelezwa kwa muda husika. Nina ahadi kule tangu ya Awamu ya Pili ya Mzee Mwinyi mpaka leo haijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Kijiiji cha Mikuva Mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi aliahidi kujenga Kituo cha Afya mpaka leo haijatekelezwa, Waziri Mkuu 2018 aliahidi kujenga barabara za lami kilometa tano ndani ya jimbo langu, mpaka leo haijatekelezwa. Mama yetu Samia Suluhu Hassan wakati anainadi Ilani ya Chama Cha Mapinduzi aliahidi kutengeza barabara ya lami kutoka jimboni kwangu kupitia Selous hadi Morogoro mpaka leo haijatekelezwa na

sijui itatekelezwa lini. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja aeleze hizi ahadi za viongozi zitatekelezwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu maji; maji ni uhai na ndani ya jimbo langu Mradi wa Maji kutoka Mto Ruvuma kuja Mji wa Mangaka ndio uliopo ndani ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu hoja asubuhi alisema alisema hivi karibuni, sisi wananchi wa Jimbo la Nanyumbu tunataka kujua lini mradi huu wa maji wa Miji 28 utaanza kutelezwa lini tupate *time,* kwa sababu ukimpa mtu muda unampa matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tumenunua ndoo shilingi 2,500, mwananchi wa kijijini anapata wapi uwezo wa kuzalisha hiyo hela akanunua maji. Kwa hiyo naishauri sana Serikali, mradi huu ni mzuri na wa maana sana tuambiwe lini mradi huu utaanza ili wananchi wangu waweze kuwa na imani na Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni la mawasiliano, tumeelezwa hapa Mkongo wa Taifa umeshafika Mtambaswala na umeunganishwa na Msumbiji, lakini nataka nikwambie kuna mambo ya ajabu sana ndani ya mkongo ule. Tulielezwa Mkongo wa Taifa faida zake kwamba, gharama za kupiga simu zitapungua, sidhani kama zimepungua. Tulielezwa mawasiliano yatakuwepo, mawasiliano mpaka sasa ni magumu, lakini pale Mtambaswala...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. YAHYA A. MHATA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja naomba Serikali itekeleze hayo yaliyoelekezwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe, jiandae Mheshimiwa *Engineer* Ulenge

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi iliniweze kuchangia katika hoja hii muhimu ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na kutupa kibali cha kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya, lakini kipekee nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Samia Suluhu kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya. Kwa kweli Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya na kibali ili kuwatumikia Watanzania vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza nakuishukuru Serikali kwa mambo mazuri ambayo wameendelea kufanya. Sisi wanawake tunashukuru sana kwa kitendo cha kutujali kwa kutupa asilimia 10 ya wanawake, watu wenye ulemavu na vijana, kwa kweli tunashukuru sana, hiyo asilimia 10 imefaidisha sana, ikiwemo na sisi wanawake wa Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza Serikali tumeona madarasa mazuri kabisa ya kisasa, watoto wetu wanasoma bure, tunaishukuru sana Serikali. Haikuishia hapo tu tumezunguka kukagua miradi ya maendeleo miradi, inakwenda vizuri, miradi mikubwa na midogo inaendelea, kwa kweli kazi ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza Serikali na kuishukuru kwa suala zima la hotuba ya Rais aliyohutubia siku ya tarehe 4 Aprili, ambayo iligusa moja kwa moja kwenye suala zima la kilimo. Tunajua kilimo ndio ilikuwa ndio kilio kikubwa sana kwa wananchi wa Tanzania, lakini ile hotuba inakwenda kuwafungua wakulima kuwapa ahueni, inakwenda kuwafanya walime kilimo cha kisasa, lakini chini ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ambaye kaka yetu

tunamwamini sana, kwa hiyo tunaishiwa hoja za kusema kwa sababu tayari ameonyesha mwelekeo wa kwenda kumsaidia mkulima. Ahsante sana Serikali, tunamtia moyo Mheshimiwa Waziri kwenye suala zima la kilimo, akaze buti tuko nyuma yake, aendelee kuwa ngangari, ahsante sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi sasa niinge kwenye changamoto za Mkoa wangu wa Rukwa. Nianze kwenye changamoto ambayo inawasibu sana wana Rukwa kiasi kwamba wamenituma nije niseme mbele ya Waziri Mkuu. Kwa kweli tunashukuru sana Serikali imeweza kutujengea stendi mpya ya kisasa ambayo iko mbali kidogo na Mji wa Sumbawanga Mjini. Pamoja na mafanikio hayo kutujengea stendi mpya, stendi hiyo imekuwa na machungu ndani yake kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Rukwa wanapata mateso makubwa sana pale ambapo Serikali imepiga marufuku wananchi wale kupanda magari wakiwa Mjini Sumbawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, magari yamepigwa marufuku kushusha au kupandisha pale Mjini Sumbawanga. Kwa hiyo adha hii imewafanywa wananchi wa Mkoa wa Rukwa hasa Sumbawanga Mjini wanapata mateso makubwa sana. Tunaomba Serikali pamoja na kwamba imejenga stendi mpya ya nzuri mpya ya kisasa hiyo stendi iko mbali na Sumbawanga Mjini, kwa hiyo tunaomba zitumike stendi zote mbili wananchi wapandie stendi ya zamani ambayo iko mjini, lakini pia wapandie na ile stendi mpya, zitumike stendi zote mbili, kuliko sasa hivi wananchi wanapata adha kubwa sana wanatumia usafiri kutoka pale mjini kwenda kufuata stendi ambayo iko mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule unakuta wananchi wanaamka asubuhi saa 10 kufuata stendi iliko mbali, ni gharama kubwa, lakini pia magari yanayotoka mikoani au wilayani yanaishia huko nje ya mji, kwa hiyo inakuwa ni adha kubwa sana. Tunaomba leo hii ningechangia kwenye wizara husika ningeweza kushika shilingi ya Waziri mhusika wa hiyo, lakini kwa vile nimechangia kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu namheshimu sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu

amekuwa akifanya kazi nzuri kazi kubwa kwa hiyo siwezi kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba atakapokuja kuhitimisha hoja yake hili suala la kutumia stendi zote mbili, basi atoe neno moja tu ili wananchi wa Mkoa wa Rukwa na wananchi wanaoishi Sumbawanga Mjini waweze kupona roho zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kwenye changamoto za Mkoa wangu wa Rukwa. Tuna changamoto ya maji, lakini naishauri Serikali, suluhisho kubwa la tatizo la maji katika Mkoa wa Rukwa, tunaomba tuna chanzo ambacho kinaweza kuwa ni suluhisho la kudumu, chanzo cha kutoa maji kwenye Ziwa Tanganyika na kuleta kwenye Wilaya zote za Mkoa wa Rukwa. Hiki ni chanzo ambacho hakiwezi kuleta tena shida, tunaomba kama ikiwezekana, basi Serikali iweze kutoa maji Ziwa Tanganyika na kuleta kwenye Mkoa wa Rukwa kwa ujumla na mikoa mingine ya pembezoni.

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hapana ni ya kwanza, endelea.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine, tunaomba barabara narudia tena, nimewahi kuleta hoja hii hapa barabara ya kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga Mjini. Barabara ile nilisema ina matuta mengi makubwa sana, matuta yale yaliweza kusababisha viuno vya wanaume wa Mkoa wa Rukwa kutokufanya kazi ipasavyo, sasa naleta tena hoja hii naomba sana, Serikali inapata ugumu gani wa kutoa yale matuta? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana yale matuta yanatuletea matatizo makubwa sana, hata kwenye magari yanaharibika, ile barabara tunaitegemea kwa uchumi wa Mkoa wa Rukwa, matuta yamekuwa ni kitu ambacho kinatuletea matatizo. Rais hayati aliyekuwepo...

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa tu Mheshimiwa anayezungumza hivi sasa hoja ya matuta na viuno wanaume wa Mpanda wamethibitisha wanalalamika sana humu ndani ya hili jingo. Nakushukuru sana*. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe, taarifa hiyo?

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa tena kwa mikono miwili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameona tunavyopata tabu sana wanaume wa Mkoa wa Rukwa, kwa kweli ni shida nyumba nyingi zinavunjika chanzo ni matuta, matuta ni makubwa sana hata hayati Dkt. Magufuli alimwambia Waziri wakati ule alikuwa Waziri wa Mambo ya Uchukuzi, alimwambia matuta yale nakupa mwezi mmoja yatoke, lakini haikutosha hata Katibu wa Chama Cha Mapinduzi alipofanya ziara kuja Mkoa wa Rukwa alipata tabu mgongo siku hiyo hakulala. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akawaa anawapa wiki mbili watoe hayo matuta, lakini mpaka leo hii imekuwa ni kimya. Tunaomba basi Serikali iweze kulitilia maanani suala hili matuta yale yaweze kuondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, naomba kuhusiana na barabara inayotoka Kibaoni kwa Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Pinda inayopita Muze, Kilemba, Kiriyamatundu inakuja kutokea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita *Engineer* Ulenge, jiandae Vincent Mbogo jiandae Dkt. Alice Kaijage.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kunemesha neema kubwa na mwenye kuneemesha neema ndogondogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukuwe fursa hii sasa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayofanya kufuatilia shughuli za kila siku za Serikali, hakika anaitendea haki nafasi yake hii. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayofanya ya kuhakikisha anatuletea maendeleo Watanzania na hakika Mheshimiwa Rais wetu amedhihirisha upendo wake kwa Watanzania wote kwa kuanzisha Wizara maalum ya wanawake jinsia na makundi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonekana kabisa adhma ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha anakwenda sambamba na malengo 17 maendeleo endelevu ya dunia ya kuhakikisha kwamba hakuna anayeachwa nyuma katika maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba Serikali ilianzisha na kuunda Tume ya Sekretarieti ya Ajira kwa mujibu wa kifungu cha 29(1), Sura 298, iliipa mamlaka ya Sekretarieti ya Ajira iajiri kwa niaba ya Serikali. Sasa hili Wizara hii mpya ambayo imeundwa iweze kufanya kazi na kuleta tija kwa makundi yale yaliyolengwa wakiwemo waajiri wangu wanawake wa Mkoa wa Tanga. Naiomba na kuishauri itoe kibali cha muda kwa Wizara hii ili iweze kuajiri Maafisa Maendeleo Jamii Kata na Afisa Maendeleo Jamii ya Vijiji kwa sababu ni wachache mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, peke yake kuna upungufu wa 2,322 Maafisa Maendeleo Jamii Kata, kwenye ngazi ya kata, lakini Maafisa Maendeleo Jamii wa Mkoa kuna upungufu wa 2,284 na Maafisa Maendeleo Jamii wa Wilaya

kuna upungufu wa Afisa Maendeleo Jamii 41. Niiombe sasa Serikali itoe kibali kwa mamlaka ya ajira za wilaya na za mkoa na hata ngazi ya wizara hii ili iweze kuajiri kwa muda ili wizara hii mpya ikaweze kuleta tija kwa makundi yaliyolengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuchangia ukurasa wa 10 mpaka wa 13 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais ambao umeeleza mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza mpango na bajeti ya mwaka 2021/2022. Miongoni mwa mafanikio yaliyotajwa ni pamoja na kukamilika kwa kulipa fidia maeneo ya kipaumbele katika mradi wa bomba la mafuta linalotoka Hoima mpaka Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa zilizopo miongoni mwa maeneo ya kipaumbele ni pamoja na eneo la Mkuza ambapo ndiyo bomba linalazwa mita 30, kwa maana ya 15 kutoka kila upande lakini Mkoani Tanga takribani wananchi 100 hawajalipwa mpaka sasa kutoka mwaka 2018 Juni. Sasa mkisema kwamba mnawalipa maeneo ya kipaumbele vipi wananchi hawa waliopisha eneo la Mkuza mpaka leo hawajalipwa? Tunaishauri Serikali iwalipe wanachi hawa tangu Juni, mwaka 2018 ni miaka minne sasa wameyatoa maeneo yao na mpaka leo bado hawajalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna makampuni ambayo yalikuja tangu Julai mwaka 2019 kuchukua maeneo katika upande ule ambapo mradi utaelekea. Alikuja *TPA,* alikuja Mihan Gas, amekuja Ngorongoro, amekuja Simba lakini wengi wao pia hawajalipa. Kwa mfano, *Black Oil* wamechukua hekta 200 hawajalipa mpaka sasa na tathimini ilikwishafanyika vilevile Ngorongoro hekta 100 hawajalipa mpaka sasa na sasa hivi ni takribani miaka minne inakwenda mnawaambia nini wananchi wale wa Tanga waendelee kukaa *Idle* mpaka lini sasa?

Niiombe na kuishauri Serikali iwahimize makampuni haya yaliyochukua maeneo kule Mkoani Tanga kwa ajili ya bomba la mafuta, wafanye hima na haraka kuhakikisha wananchi wale wanalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani tumeshafanya tathmini na kila kitu leo unakuja kumwambia mnazi wake ulikuwa asilimia 50 sasa hivi mnazi umefika asilimia 100 umlipe kwa thamani ile ya asilimia 50 haiwezekani! lazima wa-*consider time value of money* kwa sababu ni muda mrefu sasa umepita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumze suala la elimu nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuwapa mabinti *second chance* ya kurudi mashuleni baada ya kujifungua na inaonekana kuna baadhi ya watu ni kama wanaona kitu kile hakiwezekani, binafsi yangu nampongeza sana sana Mheshimiwa Rais kwa azma yake hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tujiulize katika Taifa letu hili sisi wanawake tulioolewa tumetoa *second chance* mara ngapi kwa waume zetu labda wanapotutenda au akina Baba mmetoa *second chance* mara ngapi kwa wake zenu wanapowatenda, inakuwaje binti aliyepata ujauzito asipewe *second chance* ya kurudi shuleni? Mimi ninampongeza sana Mheshimiwa Rais amejipanga vizuri, kuhakikisha kwamba *no one is left behind* katika maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshauri sana Mheshimiwa Rais wetu pamoja na Serikali yetu kwamba ili sasa Binti yule ayafikie malengo ambayo Mheshimiwa Rais wetu anayatamani na ninafikiri hii itakuwa *legacy* kubwa kwa Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha anajenga mabweni nchi nzima kuwapunguzia watoto wanaotembea mwendo mrefu na hapo katikati ndiyo wanapopata vishawishi na kuharibiwa, pia kuwatengenezea mazingira wezeshi ya kuweza kusoma kwa bidii. Naiomba sana Serikali iweke *legacy* hii wakati huu wa Mheshimiwa Rais wetu mwanamama kabisa, kuhakikisha wajukuu zake na watoto wa kike wanapata mazingira mazuri wezeshi ya kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongezea hapo, naomba niikumbushe sasa Serikali ikamalizie bweni katika shule ya Sekondari ya Mfundia kwenye Kata ya Kerenge kule Korogwe Vijijini. Bweni limeshajengwa lakini limekaa muda

mrefu halijakamilika, binafsi yangu nimekwenda kujitolea kupeleka milango katika bweni lile ili watoto wa kike waweze kusoma, lakini mazingira bado hayajakaa vizuri namuomba sana Mheshimiwa Waziri husika ahakikishe bweni lile kwenye shule ile ya Mfundia Korogwe Vijijini linakamilika na mabinti wetu waweze kusoma. Mtu ukitembea ukifika shule ya Mfundia hakika mazingira is very *conducive* kwa kupiga *book* lakini mabinti wanahangaika mazingira siyo wezeshi. Niiombe sana Serikali ikamilishe jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niseme kwamba wakati tukimtazama Mheshimiwa Rais wetu jinsi ambavyo anapambana kwenda sambamba na dunia kama mwenyewe alivyosema ukitaka kwenda mbali nenda pamoja lakini ukitaka kwenda peke yako ina maana utakwenda haraka. Anaonyesha dhamira yake ya dhati kwenda na ulimwengu lakini cha ajabu sera zetu za nchi hii baadhi bado zipo nyuma. Wakati tunafikiria au dunia inazungumza maendeleo endelevu 17 kuna sera bado zipo kwenye maendeleo ya *millennia!* inasikitisha kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaziomba zile Wizara ambazo bado zina sera zilizopitwa na wakati zirekebishe sera zao yaani kuna Wizara kila uki-*google* inakuletea sera ya mwaka 2002 wakati tumeshatoka huko sasa hivi tupo mwaka 2020. Tunaomba sana sera hizi ziboreshwe ili kwenda sambamba na mipango ya maendeleo endelevu kama ambavyo Mheshimiwa Rais anayatendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais amefanya vizuri kwenye lengo Namba Tano la Maendeleo Endelevu, lengo Namba 10 la Maendeleo Endelevu na hata alipokaa juzi na kutafuta maridhiano ametekeleza lengo Namba 16 la Maendeleo Endelevu ya Dunia inakuaje sasa sera za ndani ya nchi mpaka leo nyingine zipo rasimu unakuwa na rasimu ya sera miaka mitano, miaka saba kwa nini zisikamilike ili kwenda sambamba na maono ya kidunia na maono ya Mheshimiwa Rais wetu?*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapa nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Vincent Mbogo, jiandae Mheshimiwa Dkt. Alice jiandae Mheshimiwa Michael Mwakamo.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu kwenye bajeti yake ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nzuri sana imegusa maeneo mengi ya nchi hii. Kwanza kabisa napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Rais ameupiga mwingi sana. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana ya maendeleo ndani ya nchi yetu na nje ya nchi. Ukiangalia katika Jimbo langu la Nkasi Kusini lilikuwa na Kata 11 kituo cha afya kilikuwa kimoja tu, ndani ya uongozi wa Mama Samia Suluhu Hassan nimejengewa vituo vya afya vine! Mama Samia safi. Madarasa yamejengwa, Vituo vya Afya vimejengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji. Kwenye changamoto ya maji kuna miradi mingi kichefuchefu ndani ya Wilaya ya Nkasi pamoja na Mkoa wa Rukwa mzima. Naomba ile miradi kichefuchefu ipewe Jeshi la Ulinzi. Jeshi la Kujenga Taifa tumeona linafanya kazi vizuri sana kwenye miradi mbalimbali, ile miradi kichefuchefu basi wakabidhiwe Jeshi ili iweze kwenda kwa haraka na kumalizika kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mradi wa maji Mlale, upo mradi wa maji Kizumbi una miaka nane sasa hivi bado umetekelezwa ninaomba Wizara ya Maji ikae chini miradi hii ikabidhiwe Jeshi la Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nkasi Makao Makuu ni aibu, ina changamoto kubwa sana. Nadhani Tanzania nzima Wilaya ya Nkasi haina maji, ninaomba kuna

mradi wa Ziwa Tanganyika lakini tuwe na mradi wa dharura kwa sababu huu mradi wa Ziwa Tanganyika utachukua muda, tuwe na mradi wa dharura wa kuokoa maisha ya watu wa Wilaya ya Nkasi. Ipo mito, mto Mfwizi na Mto Zimba, mito hii ni vyanzo sahihi havikauki maji kiangazi na masika, ninaomba Wizara ya Maji ije itengeneze mradi wa maji kwenye hii mito miwili Zimba na Mfwizi maji ya mserereko yaweze kwenda Wilaya ya Nkasi kama mradi dharura ambao utaweza kunusuru maisha ya watu wa Wilaya ya Nkasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije Ziwa Tanganyika. Ziwa Tanganyika toka tunasoma tunaulizwa Ziwa lenye kina kirefu majibu ni Ziwa Tanganyika, Ziwa hili hakuna meli hata moja, hakuna usafiri wowote ndani ya Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, uchumi wa Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Katavi ume- *paralyze* japo bajeti ipo ya kutengeneza meli Liemba na Meli MV Mwongozo, naomba hili la meli Ziwa Tanganyika liwe dharura ni janga kama *UVIKO!* haya ndiyo maeneo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwona Mheshimiwa Rais anahangaika kufungua milango ya kiuchumi, Congo imeingia Afrika Mashariki, amejenga Ubalozi lakini miundombinu inayoelekea kwenye lango la uchumi bado ni shida, niiombe *TARURA* iongezewe bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais alitupa Bilioni Moja na Milioni Mia Tano kwa ajili ya Miundombinu katika Majimbo yetu, Mheshimiwa Rais Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la *TARURA* iongezewe kuna barabara ya Ninde, Kizumbi, Wampembe, kuna vilima hizi barabara hazipitiki. Ndani ya Jimbo langu Kata Nne magari hayaendi, ikifika masika ndiyo kabisa. Kwa hiyo, meli usafiri wa ndani ya Ziwa Tanganyika meli hakuna na hizi Kata zipo ndani ya Mwambao wa Ziwa Tanganyika, usafiri ndani ya Ziwa hakuna, barabara hakuna kwa hiyo, wale watu unaweza ukapata picha wanaishi maisha ya namna gani, hata mzunguko wa pesa hakuna! Kwa hiyo wanamaisha magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba Wizara ya Miundombinu suala meli Ziwa Tanganyika ni janga ifanye kama dharura imeingiza kwenye bajeti lakini bajeti inaweza ikatumia miaka miwili mitatu wananchi wanateseka hakuna mawasiliano na nchi za jirani za Congo, Zambia na Burundi ambao ndiyo chanzo cha uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa ajira nashukuru sana Ndugu yangu Mama yangu Jenista Mhagama amesema Rais atatangaza ajira, nipende kumshukuru sana. Ajira hizi wafanye utafiti zielekee vijijini kwa sababu kuna shule zina Walimu wawili, vituo vya afya vina Muuguzi Mmoja, mfano Nzinga kuna Muuguzi Mmoja, Mwinza kuna Muuguzi Mmoja, Kizumbi kuna Wauguzi Wawili, kwa hiyo wanapotoa ajira hizi waelekeze maeneo ambayo kuna upungufu wa Wauguzi au watumishi wa afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja kwenye Mahakama, hotuba ya Waziri Mkuu hapa ilionyesha mahakama nyingi nchi nzima zinajengwa lakini nchi hii tuwe na vipaumbele kuna maeneo ambayo ni nyeti kila Mbunge humu akikaa akaorodhesha maeneo nyeti kwa sababu mahitaji ni mengi, vipaumbele vipo vingi, lakini tufike sehemu fulani tuwe na maeneo ambayo yanaweza kuchangia pato ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ndani ya Jimbo langu ipo Kata ambayo Hakimu anatumia stoo ya mazao ndiyo anahukumia kesi mule ndani! Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Pinda alifika tumemkuta hakimu yupo ndani ya *godown*. Kwa hiyo, tungeanza kuwatoa kwanza Mahakimu ambao wanatumia ma-*godown* ndiyo tuanze kukarabati hizo nyingine na tujenge hizo nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa mawasiliano. Nina Kata tano kwangu Jimboni hakuna mawasiliano kabisa. Simu hamna na zipo mwambao kwao hata uhalifu na hata usalama wa nchi hii unakuwa hatarishi. Mfano Kata ya Kala, Kata ya Wampembe, Kata ya Ninde, Kata ya Kizumbi, hizi

Kata ndiyo uvuvi unafanyika mkubwa sana hakuna mialo, miundombinu mizuri, hakuna masoko hakuna vituo vya Polisi, kwa hiyo mtu akivua leo hii akiuza jioni anavamiwa anachukuliwa nyavu ananyang'anywa fedha. Ninaomba Wizara ya Mambo ya Ndani baada ya bajeti hii anapohitimisha aje aseme Kala Kituo cha Polisi kinaanza kujengwa lini? Kwa sababu mimi kama Mbunge wao tumeshachanga fedha *cement* tumejenga imefikia kwenye *renter* ni wao Wizara ya Mambo ya Ndani kuja kumalizia pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya mwaka mmoja wamevamiwa mara nne wananyang'anywa dhana zao za uvuvi, wananyang'anywa fedha, wanapigwa baadae wanahamia ng'ambo wakisha wadhulumu wakishawaibia, wakishawavamia kwa sababu hakuna Kituo cha Polisi. Kwa hiyo watu biashara zao hawafanyi kwa sababu hakuna amani, hakuna mialo kama miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii sijaona ujenzi wa masoko ukanda wa Ziwa Tanganyika ambako ndiko mazao ya samaki inatakiwa kuwe na kituo cha Kitaifa cha masoko ili mtu anapokwenda kufanya biashara yake ya mahindi kupeleka Congo kuwe na kituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, njooni mjenge soko Wampembe, Mheshimiwa Jafo amefika Wampembe anakufahamu, njooni mjenge Wampembe soko la biashara la mazao ya Samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu lina changamoto kubwa sana, upande wa vituo vya afya. Nimesema toka nimeingia kituo cha afya kilikuwa kimoja nacho kilijengwa kwa kuchukua fedha za zahanati. Ina maana mpaka tunavyoongea hivi ni ndani ya Mama Samia ndiyo vituo vya afya vinajengwa Vinne. Hakuna vituo vingine. Kwa hiyo, ni shida sana jiografia ya Jimbo langu la Nkasi Kusini kidogo lilikuwa limesahaulika upande wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *TARURA* waongezewe fedha ili tuweze kumaliza changamoto ya

barabara mwambao mwa Ziwa Tanganyika pamoja na Jimbo la Nkasi Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Namuita sasa Dkt. Alice Kaijage, jiandae Mheshimiwa Michael.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kunipa kibali pia cha kusimama, nampongeza sana Mama Samia Suluhu Hassan na Serikali yake yote kwa jinsi ambavyo wanaendelea kufanya kazi kwa umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa yasiyoambukiza ni magonjwa mengi na mengi yao yanazuilika, machache ni ya kurithi lakini ndiyo maana tumeendelea kuishauri Serikali katika Sheria zisizopungua 62 ambazo zimepitishwa na Bunge hili, nyingi sana kwa njia moja au nyingine zinahusika katika masuala mazima ya kuzuia magonjwa haya yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, tunaomba Serikali izipitie na kuziboresha sheria hizi ili ziendane na mapambano dhidi ya kuzuia magonjwa ya kuambukiza ambayo hakika mengi yanazuilika. Sheria hizi ni kama moja apo Sheria ya Tumbaku, Sheria ya Bima ya Vyombo vya Moto vya Barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali za barabarani zinatokana na vyombo vya moto ni mojawapo ya magonjwa yasiyoambukiza, tatizo hili limekuwa tatizo kubwa sana. Nimeona nizungumzie hili kwa sababu lina kuja kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kwamba Serikali ije na mpango wa uhakika sana wa kuhakikisha inapunguza madhara inayotokana na vyombo vya ajali barabarani. Kama inawezekana Serikali iunde Mfuko wa Ajali za Barabarani tunaita *(Road Accident Fund)* huu mfuko utasaidia kwanza kupunguza gharama kuwagharamia wale watu wanaopata madhara ya hizi ajali za barabarani ambao ni mojawapo wa ugonjwa usioambukiza, lakini pia mfuko huu utasaidia vituo vyetu vya afya viwahudumie hawa waathirika au waliopata madhara ya ajali kwa haraka kwa upesi bila kujali kabisa rasilimali fedha, yaani huu mfuko utasaida akipata ajali tu paa! akienda kituo cha afya atahudumiwa bila kungoja kwanza malipo ya rasilimali fedha. Kwa hiyo, mfuko huu utasaidia sana kuokoa maisha ya ndugu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninashauri uboreshwe kwamba wahanga wanaotokana na ajali hizi wawe wanalipwa kutokana na bima ya chombo kile kilichosababisha ajali. Kwa sababu sasa hivi ni mpaka dereva ashitakiwe ahukumiwe aonekane anahatia ndiyo yule muhanga wa ajali alipwe fidia au wale wafiwa walipwe fidia.

Mimi nashauri iboreshwe hii bima kuna Sheria ya Bima ya Vyombo vya Moto iboreshwe kwamba, wahanga walipwe siyo kwa kuzingatia mashtaka au ya dereva kuhukumiwa hapana! *As long as* chombo kimethibitika ndiyo kilisababisha ile ajali au kile kifo basi sheria iboreshwe kwamba wawe wanalipwa kutokana na ile bima ya kile chombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hii sheria iboreshwe kwa sababu ni sheria mojawapo ambayo inahusika na magonjwa yasiyoambukiza ambayo ni ajali imezidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni masuala ya magonjwa yanayohusika na masuala ya UKIMWI. Ni suala lisilopingika kwamba asilimia 90 ya mapambano au madawa Afua zote za kupambana na UKIMWI tunategemea wafadhili, ni suala lisilopingika kwamba viwanda katika nchi au

maboresho ya viwanda katika nchi ni mojawapo ya mustakabali wa kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? Kulikuwa na kiwanda Arusha cha kutengeneza dawa za kuzuia makali ya *virus* vya UKIMWI mwilini, kiwanda hicho kilikuwa kimepewa ufadhili mkubwa wa *European Union* wakatengeneza mitambo ya kisasa kweli kweli, lakini kiwanda hiki kimekufa. Ninaishauri Serikali kupitia *MSD* wakifufue kile kiwanda, Msajili wa Hazina na asilimia 40 wale Wawekezaji walikuwa na asilimia 60 sasa *MSD* kwa maana ya Serikali ilinunua asilimia 60 ya kiwanda kile. Kwa nini nasema hivyo? Dawa, matibabu kwa mwananchi ni suala la usalama. Hatuwezi kutegemea kila siku matibabu ya mwananchi wako yatoke nje ya nchi. Huwezi kujua mtu anawaza nini, kuna vita kuna kila kitu!

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo kuna vita mtu atakazana kutengeneza dawa akuletee wewe, aache kupambana na vita yake? Kwa nini tusiwekeze kwenye viwanda vyetu hapa nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusiwekeze kwenye viwanda vyetu hapa nchini? *MSD* kwa miaka miwili sasa hivi kwenye ile Keko *Pharmaceutical Industries* walianza kutengeneza dawa moja tu ya *paracetamol,* na sasa hivi wana *products* kumi, vilevile wale wale wametengeneza barakoa. Mwananchi wa kawaida alikuwa hawezi kununua barakoa, lakini sasa hivi tumetengeneza barakoa pale Dar es Salaam, tuna kiwanda. *MSD* pia imetengeneza kiwanda cha *gloves* kule Mufindi kwenye baridi, maana ndiyo mazingira yanayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyo bado tuna uwezo wa kufanya vitu vyetu. Suala la dawa ni usalama, usalama kabisa kwa wananchi ambao unawaongoza. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la dawa za kulevya. Haya ni mapambano ambayo ni nyeti sana. Wenzetu wanatumia vyombo vya kisasa ambavyo ni

*sophisticated* kama vile boti na mitambo mbalimblai. Sasa nishauri tena kwa mara ya tatu, hii mamlaka itengewe fungu la maendeleo ili waweze kununua vifaa vya kisasa, pamoja na kujenga vituo ambavyo waraibu wakishahitimu wanaenda kufundishwa stadi kazi ili wasirudi tena kwenye dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii mamlaka sitoiongelea sana; kila siku naongea, kwamba waongezewe fungu la maendeleo, waongezewe fungu la pesa kwa kuwa kazi yao ni ngumu na ni ya kishawishi sana. Sijasema waongezewe mafao binafsi, waongezewe mazingira ya kufanya kazi, waongezewe wafanyakazi, kwa sababu wana upungufu wa wafanyakazi zaidi ya 189. Kazi yao ni ngumu. *MACH clinic* zao ziko chake. Kwa mfano Kanda ya Ziwa yote ina *MACH clinic* moja tu ambayo iko Mwanza. Ile dawa wanakunywa kila siku, hivyo haiwezekani utoke Ukerewe uje Mwanza leo asubuhi halafu kesho urudi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyo nashauri tena kwa mara ya tatu katika michango yangu. Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya itengewe fungu, iongezewe fedha kwa kuwa kazi yake ni nyeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu *Workers Compensation Fund.* Nimeiona imeelezwa vizuri; lakini nilikuwa nashauri, lengo lisiwe tu kutoa fidia au ufanisi uwe tu kwa sababu umetoa fidia, hapana. Lengo liwe ni kuwekeza maeneo ambayo yatasaidia kupunguza ajali maeneo ya kazi; siyo mafanikio ni kufidia, hapana. Lakini pia nilikuwa nashauri, ikiwezekana mitaala ya *medical schools* zote iwe inajumuisha masuala ya ulemavu utokanao na ajali na magonjwa mahala pa kazi. Mitaala ya *medical schools* ihusishe masuala yote ya tathmini ya ulemavu unaotokana na ajala na magonjwa mahala pa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho kabisa ni suala la wenzetu *OSHA*. Nipongeze kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya ya kuhakikisha usalama wa nguvukazi mahala pa kazi. Hata hivyo, nilikuwa naishauri

Serikali, kwamba, ije na sheria, kama ikiwezekana, ambayo itawezesha kuajiri *either part-time or fulltime* watu wote wanaohusika na masuala ya *OSHA* mahala pa kazi ili kuhakikisha usalama wa nguvukaziwatu mahala pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Michael Mwakamo. Jiandae Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi ya kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza naipongeza Serikali kwa namna ambavyo inatekeleza majukumu yake na namna ambavyo inahudumia wananchi kwenye maeneo mbalimbali kwa kipindi kizima hiki cha mwaka ambao tunaumaliza sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilisimama kwenye eneo hili, nilitoa shukrani na nilitoa tamko la kuomba eneo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, na tulipatiwa pale eneo la hekari 4,000 na hadi sasa hekari 2,500 zimeshapata wawekezaji na kazi inaendelea. Kwa hiyo nawapongeza sana Serikali kwa kutuletea wawekezaji hawa na kuanza kufanya uwekezaji katika maeneo ambayo yapo kwenye Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mazuri yote haya ambayo nayaeleza, ninalo ombi dogo ambalo ningependa nilitangulize kabla sijatoa mchango wangu kwenye maeneo ambayo nimejipanga kuyazungumza; kwamba wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini na hususani kwenye maeneo ya majimbo ya karibu wanaishukuru sana Serikali, hasa Mheshimiwa Rais kwa kufanya ziara maeneo mbalimbali katika maeneo ya jirani na Mkoa wa Pwani na kushiriki nao katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo. Lakini kuna ombi moja kubwa sana, na nitumie nafasi hii niliwasilishe ombi hili ili Serikali isikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo langu wanamuomba sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muunguano wa Tanzania afike pale Mlandizi azungumze nao, kwa sababu aliwaahidi kuwa atafika wakati ule wa kampeni. Kwa hiyo natumia hadhara hii leo kumuomba akumbuke ahadi ile, afike, afanya mazungumzo nao ili awasikilize wananchi moja kwa moja pamoja na mimi Mbunge wao ninayewazungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya ombi hilo leo nataka kujielekeza kuzungumzia sekta ya uzalishaji, hasa kwenye habari hii ya kilimo. Wabunge wengi tumezungumza habari ya kilimo, tumeiona kwenye bajeti kwenye hotuba hii ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu amewasilisha. Ametambua kwamba sekta ya kilimo uzalishaji ina takriban asilimi 65 ya wananchi wa Tanzania ambao wanafanya shughuli za kilimo. Hata hivyo, zipo changamoto ambazo pia zimeelezwa, lakini vile vile na mafanikio makubwa ambayo yameelezwa kwenye sehemu hii. Mimi nataka nizungumzie maeneo machache makubwa, hasa yale ambayo mimi nimeyaishi kama mtoto wa mkulima katika maeneo, ambayo waliomo humu wengi naamini nao wameyaishi kama watoto wa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wengi katika nchi hii ni wakulima wa ngazi ya chini sana. Ni wazee wetu ambao wanalima kwa kutumia jembe la mkono, ndio wazee hawa ambao wao tunapozungumzia masuala ya upatikanaji wa mbegu ni wale ambao wanavuna mazao yao, wanahifadhi kwenye maghala ya asili na mwaka mwingine unapokuja wanakwenda kupanda tena. Sasa tumezungumza hapa na tunaona mipango ya Serikari, wanajaribu kuzungumzia upatikanaji wa pembejeo za kilimo, na naona kazi kubwa inayofanywa na Waziri wa Kilimo juu ya kukisimamia kilimo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe Serikali; kwamba tunapotazama ukubwa wa kukikuza kilimo tusisahau hili kundi kubwa la wakulima ambao wanaishi vijijini, na ndio hawa ambao wanalea familia kwa kutumia nguvu zao kwa

kulima kwa jembe la mkono. Ndio hawa ambao wanalima na wanahakikisha watoto wao katika maeneo ya vijiji wanakwenda shule. Lakini wanapata changamoto mbalimbali ikiwemo suala la kutumia mabonde yaliyopo ambako bodi za mabonde wanawawekea mazingira magumu ya kufanya shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mmoja mdogo sana. Kwenye Jimbo la Kibaha Vijijini wengi wakuliwa wanalima kwenye bonde la Mto Ruvu. Mwaka jana tunakumbuka, na si mwaka jana tu, tulipata tatizo kubwa la mto ule kupungua maji. Baada ya kutokea tatizo lile kukatokea saka saka kubwa sana ya kukamata wakulima ambao wanalima pembeni mwa lile bonde. Sasa mimi ningeomba Serikali, pamoja na kwamba vyombo vyote hivi vinafanya kazi ya kuwahudumia wananchi, lakini ijaribu kuangalia namna ambavyo watawaelekeza, kwamba ni namna gani wayatumie yale maji ili nao waweze kufanya maisha yao yaendelee. Kwa sababu unavyokwenda kumzuia asifanye shughuli ile, unapokamata mashine zake anazotumia kumwagilia tunasahau kwamba mkulima huyo hana njia nyingine anayoweza kuitumia ili kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ingekuwa vizuri sana kama ungewekwa utaratibu mzuri wa kuelekezwa namna gani bora wanaweza kuyatumia maeneo yale ili waweze kuendelea kuendesha kilimo chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeona Serikali imewekeza nguvu kubwa sana kwa hawa maafisa ugani. Lakini maafisa ugani ambao wamewapatia uwezo huu wa kuwahudumia wananchi, wanahudumia wananchi wengi ambao ndio wale ninaowazungumzia, wakulima wadogo; wakulima ambao Serikali imewazungumzia, ukitazama kwenye mipango mingi mikubwa sana inayoendelea hapa. Tunazungumza benki ambazo zinatakiwa ziwakopeshe wakulima. Sasa, tujiulize, ni kwa kiasi gani benki hizi zimewafikia hawa wakulima wadogo? Ni kwa kiasi gani wakulima wadogo hawa wanafaidika na hii mipango mikubwa ya Serikali? Tukifanya hivi na tukihakikisha Serikali inaelekeza

nguvu kule, ndivyo tutakavyokuwa tumesaidia kundi kubwa la wananchi ambao watahudumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka nilizungumzie hapa ni eneo la mawasiliano. Tumeona kwenye hotuba, ni namna gani Serikali inaongeza kilomita nyingi za kuhudumia Mkongo wa Taifa. Hata hivyo, mawasiliano vijijini bado ni tatizo kubwa sana. Kwa mfano ukienda kwenye jimbo langu tu kuna Vijiji vya Milalazi, Kimalamisale pamoja na Magindu wanapata mawasiliano kwa shida sana. Na hili nimetaja hapa kama sehemu ya mifano, lakini vijiji vingi nchini vina shida ya mawasiliano. Kwa hiyo, ni vizuri tunapozungumzia suala la mawasiliano tujielekeze katika kupeleka mawasiliano haya vijijini, kwa sababu tunaona kila Wizara kila Idara inayozungumza maendeleo inahusisha maendeleo na masuala ya mawasiliano. sasa kama vijijini kutakosa mawasiliano mazuri yenye uhakika, watu hawa tutawatoaje kwenye mazingira hayo ya mawasiliano? Kwa hiyo ningeomba tuone namna bora ya kushughulika na jambo la mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka nizungumzie ni kuhusu Mkoa wa Pwani. Mkoa wa Pwani una mkakati mkubwa sana wa kimaendeleo; nilizungumza mwaka jana na ninalirudia tena, na ninafahamu kwamba Serikali ina mipango mikubwa ya juu ya kuendeleza maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la Mkoa wa Pwani tunalo eneo la Bagamoyo; eneo ambalo lina mkakati mkubwa sana. Tunasikia kwamba kuna mikakati mikubwa ya kuimarisha bandari ile. Ningeomba zifanyike jitihada kubwa sana, yatoke maelekezo ya wazi ya namna gani bandari ile ianze kushughulikiwa ili iweze kubeba mzigo mkubwa wa uzalishaji unaofanyika kwenye viwanda vya Mkoa wa Pwani pamoja na kuwa njia ya kupitisha mizigo inayoelekea maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na tutapoimarisha bandari ile naamini kabisa tutaimarisha barabara inayozungumzwa

siku zote, ile inayokatiza Mlandizi kuelekea Nzenga na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa machache haya naomba niunge mkono hoja na mengine nitachangia kwenye Wizara zinazohusika. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu mchana huu wa leo.

Naomba nianze tofauti kidogo na mwaka jana wakati nachangia hotuba hii. Mwaka jana nilisema Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ina miaka 41 lakini haikuwa na jengo hata moja lenye hadhi ya kuitwa Wilaya. Hata hivyo, leo nasimama hapa kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana sana sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Rais msikivu. Lakini vile vile namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwakweli hotuba yangu aliitendea haki mwaka jana. Leo nasimama hapa tayari tumeshapokea fedha zaidi ya bilioni moja kwaajili ya kujenga jengo la Halmashauri, tumepokea milioni 500 tunajenga jengo la mkuu wa wilaya, tumepokea milioni 450 tumeanza ujenzi wa mahakama ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni jambo la kushukuru sana. Tangu tumepata uhuru hatujawahi kupata miradi mingi kwenye Halamshauri ya Wilaya ya Liwale kama tulivyopata mwaka huu. Mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, nasema ahsante sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile naomba nijielekeze kwenye mchango wangu kwenye kuboresha baadhi ya mambo machache yaliyojiri kwenye hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mimi nianze kuzungumzia upande wa ajira. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais, kwa

kuonesha nia na kudhamiria kuajiri watumishi wengi zaidi kwenye Wizara yetu ya Afya pamoja na Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mchango wangu ni kwamba; ninaomba Serikali izingatie ajira hizi kulingana na jiografia za mahali Halmashauri hizi zilipo. Mimi kule kwangu watu wanakuja kuchukua *cheque number* tu. Watumishi wengi wanaoajiriwa kuja Liwale wanakuja kwa ajili ya kuchukua *cheque number* tu. Mwaka juzi nilipata watumishi 81 kwenye kada ya afya, lakini kila tukikaa Kamati ya Mipango na Fedha, watumishi 10 hadi 20 wanahama. Kila mwezi 10 hadi 15 wanahama, kiasi kwamba mpaka leo hii nimerudi kule kule kwenye uhaba wa watumishi. Lakini wakati ule inaajiri kuna vijana walioko kule Liwale wanajitolea kwenye shule zetu na kwenye vituo vyetu vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo ulisema kwamba wanapoomba ajira basi waende kwa Mkurugenzi waambatishe na CV; yaani Mkurugenzi aandike kuonesha kwamba hawa vijana wamejitolea kwa muda ili waweze kupewa vipaumbele, lakini jambo hili halijawahi kufanyika. Ninao vijana pale wana miaka mitano wengine miaka sita wanajitolea wanataka kufundisha, wanafundisha shule kule lakini walimu wanaokuja kutoka nje wanakuja kuchukua *cheque number* na wanaondoka. Naomba jambo hili lizingatiwe kwenye suala la ajira ya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile, kwenye hiyo hiyo ajira wako watu waliomaliza mafunzo, yaani kwenye vyuo vya elimu pamoja na vyuo vya afya kwa mwaka 2019 au 2018 au 2016 lakini wanaajiriwa wengine wa mwaka 2019, 2018 na kwamba waliomaliza mwaka 2016 au 2015 bado hawajapata ajira. Jambo hili nalo liangaliwe. Kwanza wenyewe watakosa umri wa kuajiriwa. Maana kama umemaliza chuo mwaka 2014 leo hii 2022 tayari wanaoomba kuajiriwa utakuta umri umempita. Kwahiyo tutakapoajiri jambo hili mimi ningeomba lizingatiwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka huko nielekee kwenye wananyamapori. Suala la wanyamapori hasa kwa

sisi wenye halmashauri ambazo tunaishi karibu na hifadhi suala la wanyamapori limekuwa ni kero kubwa sana, hasa kwa upande wa madhara wanayapata wakulima kwa mazao yao kuliwa na wanyamapori.

Ipo sera inasema wanapata fidia, lakini fidia zenyewe zinakuwa ni kidogo halafu zinakuja kwa kuchelewa. Ombi langu kwenye upande huu wa wanyamapori, Serikali sasa ione namna ya kuweka askari wa wanyamapori kwenye hizi kata ambazo ziko karibu na hifadhi ili waweze kupata ulinzi. Kata zenyewe ziko mbali, unaweza kukuta kata labda iko kilomita 70 au kilomita 100 kutoka Halmashauri ya Wilaya. Sasa ukitoa taarifa, mpaka anapokuja askari tayari kwenye vijiji vile watu washapata madhara yakutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ombi langu hapa, Serikali ione namna, ikiwezekana tuanze kuajiri polisi kata; yaani wale askari wa wanyamapori wa kata kama ilivyo kwa polisi kata ili tuweze kusaidiana kukabiliana na tatizo hili la wanyamapori kwenye hizi kata ambazo ziko kwenye mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye suala la lishe. Pamezungumzwa kwenye lishe; mimi naomba nitoe ushauri, kwa sababu mimi mwenyewe ni mtaalam wa mambo ya usindikaji wa nafaka. Tanzania tuna tatizo kubwa sana kwenye usindikaji wa nafaka. Sisi kitaalam nafaka inasindikwa tuna-*extract* unga kwa asilimia 85. Lakini kwa utaratibu wa Kitanzania, ili uweze kukoboa watu wanakoboa mahindi mpaka asilimia 60. Kwa hiyo zaidi ya asilimia 40 ya nafaka tunapoteza. Na hii ni kutokana na kwamba sera haijawekwa, vizuri sijui wapo *TBS* sijui ni *TFDA* wale ambo sasa hivi wamebadilisha sijui wanaitwa nini sijajua vizuri. Sera zao hazieleweki, hawatoi mwongozo; kwamba ili mtu upate unga kutoka kwenye nafaka inakobolewa kwa asilimia ngapi ili unga uwe na ubora. Sasa hivi mnalisha watu pamba tu, kwa sababu kama mahindi au nafaka yote umeikoboa kwa asilimia 60 unabakiza nini? Tunashindana hata na panya; panya kwenye mahindi anakula kiini kile na lile ganda lote analiacha na sisi ndio tunaneemeka nalo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ipo haja ya kubadirisha sera yetu ya ulaji. Lazima *TFDA* itoe mwongozo; kwamba kila aina fulani ya chakula, ili ukipate kwenye uhalisia wake kinatakiwa kiwe *processed* kwa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano, Mikoa ya Njombe, Iringa na Ruvuma ni wakulima wazuri sana wa mahindi lakini ndiyo mikoa inayoongoza kwa utapiamlo; unauliza watu wanapataje utapiamlo ilhali wanakula asubuhi, mchana na jioni? Tena unakuta vitumbo vimepanda kwa ajili ya sembe. Lakini wamekula pamba, hawajala chakula kinachotakiwa. Kwa hiyo ni lazima twende na wakati huo huo tuone namna ya kufika hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine; kulikuwa na miradi ilianzishwa kwenye nchi hii, kwamba kila halmashauri ilitakiwa ilete miradi ya kimkakati. Lengo la miradi ile lilikuwa ni kuongeza mapato kwenye halmashauri zetu. Baada ya mapato mengi ya halmashauri kuletwa Serikali Kuu wakasema sasa halmashauri nendeni mkatengeneze mkakati wa kubuni miradi, na watu wakabuni miradi. Kuna watu walibuni masoko, stendi; na sisi kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya ya Liwale tulibuni stendi, tukaletewa fedha lakini fedha zile kutokana na zile sheria zetu za manunuzi ambazo zinachelewa fedha zikaondoka, mpaka leo mradi ule umekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ile sera ya kuitaka halmashauri ije na miradi ya kimkakati imekufa? Maana tangu fedha zile zimeondoka huu ni mwaka wa tatu, hazitarajiwi kurudi. Lakini vilevile tulikuwa na mradi mwingine, mradi wa soko, hatuelewi uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naiomba sana Serikali, kama kweli tunataka kuendeleza halmashauri zetu na kukuza vipato kwenye halmashauri zetu basi hii miradi ya kimkakati ipewe kipaumbele. Kama miradi iliyochukuliwa fedha zake basi fedha hizo zirudi, na kama hii miradi mingine mipya ianze ili kweli halmashauri zetu zipate mapato ambayo yanaweza kuhudumia jamii zetu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba nijielekeze kwenye upande wa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Jambo lingine muda wako umekwisha.

**MHE.ZUBERI M. KUCHAUKA:** Muda umeisha!

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo. Mwongozo wa kiti.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ABDALLAH SHANGAZI:** Mwongozo wa Naibu Spika, Mwongozo wa Kiti.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba Mwongozo wako kwa kiti chako kwa Kanuni ya 76 na naomba nisiisome.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mjadala unaendelea, Mheshimiwa Gambo alivyokuwa anachangia alipewa taarifa na Mheshimiwa Asia Halamga, lakini wakati anajibu taarifa ile kuna maneno ameyazungumza ambayo si ya Kibunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Asia Halamga ni Mbunge kijana ambaye tunaamini kwamba Taifa hili linamtarajia ajifunze, na Mheshimiwa Gambo ni mzoefu na aliwahi kushika wadhifa mkubwa tu Serikalini, lakini Bunge lako haliruhusu maneno ya kejeli, dharau kwa Mbunge lakini kwa mtu mwingine yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Mwongozo wa kiti chako, je, jambo hili linaruhusiwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi ambaye ndiye *Chief-Whip* wa Chama nakushukuru kwa Mwongozo wako na Kanuni vilevile zinanipa fursa ya kwenda kutafakari na kupitia *Hansard* kuona maneno aliyoyaomba Mheshimiwa Asia na majibu yaliyotolewa maana kwa kunisaidia ni maneno yapi ambayo ameyasema.

Kwa hiyo, baada ya hapo tutakaporudi tutatoa Mwongozo na kuweka mambo sawa kama vile ulivyoomba. *(Makofi)*

Kuna tangazo hapa limetoka kwa Katibu wa Bunge. Anawatangazia Waheshimiwa Wabunge na watumishi ofisi ya Bunge kuwa wataalam wa Afya kutoka Hospitali ya Macho ya Dkt. Aguial Tanzania wapo kwenye viwanja vya Bunge eneo la nyuma ya ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya kutoa huduma maalum ya upimaji macho pamoja na miwani. Huduma hii itatolewa kuanzia leo tarehe 11 hadi tarehe 14 Aprili, 2022. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Nassor Amar - Mwenyekiti wa Jamii ya Waislam Bungeni anawaomba Waislam wote kukutana leo tarehe 11 kwenye ukumbi wa Msekwa baada ya kuahirishwa kwa Bunge mchana huu kuzungumzia masuala ya ibada ya Mwezi huu Mtukufu.

Tutakaporudi jioni panapo majaariwa tutaanza na Mheshimiwa Fatma Toufiq, Janejelly Ntate, Yustina Rahhi na Zuena Bushiri.

Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

*(Saa 07:00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi saa 10:00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae.

Waheshimiwa, ahsante. Tunaendelea, nilishamwita Mheshimiwa Toufiq, ajiandae Mheshimiwa Janejelly, atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Rahhi.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Pia naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri pamoja na wataalam wote walioandaa hotuba hii. Hali kadhalika, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana ya kutuletea maendeleo Watanzania. Mwenye macho aambiwi tazama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia kuhusu mfumuko wa bei ambayo ipo ukurasa wa 17 na upandaji wa bei katika hotuba hii, ambayo ipo katika ukurasa wa 82. Ni ukweli usiopingika kuwa bidhaa nyingi zimepanda bei kutokana na masuala mbalimbali, lakini baadhi ya wafanyabiashara hupandisha bidhaa hizo bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia upandaji wa vifaa vya ujenzi ikiwemo bidhaa ya nondo. Awali nondo milimita 12 ilikuwa ikiuzwa kati ya shilingi 16,000 mpaka shilingi 17,000, lakini sasa hivi nondo hiyo imeshapanda na kuuzwa kati ya shilingi 27,000 hadi shilingi 28,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tuna chuma chetu kule eneo la Liganga, sasa ili kuweza kupata bidhaa hii kama malighafi yetu wenyewe, ni budi Serikali ikaweka utaratibu au mkakati mzuri wa kuhakikisha kwamba chuma chetu cha Liganga kinapatikana kwa wingi ili kusudi tuweze kupata malighafi ambayo itapunguza baadhi ya bei ikiwemo na bei ya nondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 10 wa hotuba hii, Waziri Mkuu amezungumzia kuhusu ujenzi wa madaraja makubwa na ujenzi wa barabara. Niendelee kuipongeza Serikali, lakini sisi wana-Dodoma tuna kila sababu ya kuishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo makubwa ambayo tumefanyiwa sisi katika suala zima la miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukurani hii, naiomba Serikali yetu sikivu itusaidie katika ujenzi wa daraja la Godegode. Daraja hili kwa kweli limekuwa ni kero sana wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa. Kwa kweli pindi inapofikia mvua, daraja hili mawasiliano yanakatika kabisa. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu Tukufu, hili daraja la Godegode hebu lipewe kipaumbele ili tuwanusuru hawa wananchi wa Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kuna korongo kubwa ambalo linaendelea katika Mji wa Mpwapwa, nalo pia limekuwa ni hatari kwa maisha ya wananchi wa pale Mpwapwa. Basi naomba hatua za haraka zichukuliwe ili kusudi tuweze kukinga badala ya kutokea madhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, naomba niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, aliweza kuzindua barabara ya mzunguko tarehe 9/2/2022 yenye kilomita 112.3 na hatimaye ujenzi ule umeanza. Sisi wana-Dodoma kwa kweli tunampongeza sana; na kwa niaba ya wananchi wa Dodoma naomba niendelee kumpongeza sana Rais wetu kwa sababu hii inaendelea kuifanya sura ya Makao Makuu iweze kuonekana katika Mkoa wetu wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilete ombi kwa Serikali kwamba kuna upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara ya Arusha - Kibaya - Kongwa, lakini mradi huu haujatangazwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba, kwa kuwa Dodoma ni Makao Makuu na fursa ni nyingi sana na tunatamani Dodoma ifunguke kweli kweli, natoa ushauri kwa

Serikali, itakapotangaza mradi huu wa hii barabara, basi ujenzi huu uanzie kutokea Wilaya ya Kongwa na hatimaye iweze kwenda Kibaya hadi Arusha. Naamini kwa ombi hili Serikali italichukulia uzito wa pekee ili kusudi sisi wananchi wa Dodoma iweze kutufungulia maeneo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa *TARURA* una barabara ambayo ni kiungo kikubwa kati ya Kondoa - Tumberu na Thawe. Barabara hii nayo inahitaji sana kutengenezwa kwani inatakiwa ipitike kipindi chote, lakini wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakipata adha kubwa sana kwa sababu barabara hii bado ina shida. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kama itawezekana, basi Serikali nayo ione kwamba sisi wana-Dodoma tunaleta *special request* ili kusudi iweze kupatikana pesa iweze kujenga barabara hii ili wananchi wa Dodoma waweze kupata urahisi wa kusafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, naomba nikumbushe ujenzi wa barabara ya Ihumwa – Hombolo, Ihumwa – Stesheni *SGR.* Hii ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Marehemu Rais Dkt. John Pombe Magufuli, basi tunaiomba Serikali iendelee kutusaidia kutekeleza mradi huu katika bajeti hii kama itawezekana ili tuendelee kuifungulia Dodoma kwa suala zima la usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijatenda haki kama nisipo zungumzia kuhusu suala zima la zabibu, kwa sababu zabibu ni nembo ya Dodoma, zabibu ni biashara Dodoma, zabibu ni siasa Mkoa wa Dodoma. Kwa hiyo, bado zao la zabibu lina wazalishaji. Wananchi wanaozalisha wapo, lakini tatizo ni kwamba hakuna soko la uhakika la zabibu. Kwa hiyo, nilikuwa naikumbusha Serikali ione namna bora ya kusimamia mkataba wa kilimo wa zao la zabibu ili kusudi tuweze kupata uhakika wa soko kupitia *TBL* ambayo ni kampuni tanzu ya *TBL.*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu waraibu ambayo pia ameizungumzia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake. Kwanza niendelee kuipongeza

Serikali kwa kuanzisha kliniki zinazohudumia waraibu wa dawa za kulevya, maarufu tumekuwa tunawaita mateja, lakini hilo siyo jina zuri, lakini wale ni wagonjwa, kwa sababu wana tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia *program* ya kukuza ujuzi na kutoa mafunzo kwa waraibu 200, hii ni hatua kubwa sana kwa sababu Serikali inaona umuhimu wa hawa watu na hawa ni binadamu na wana haki zote kama binadamu yeyote yule katika nchi yetu hii. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba kupitia *program* hii, ni vizuri hawa waraibu wakapata mikopo ya Halmashauri 4, 4, 2; yaani wale waraibu ambao wameshapata dawa, wamepitia *methadone,* wameweza kupona na wamekuwa katika hali ya kawaida, basi Serikali ione jinsi gani ya kuwaingiza katika *program* mbalimbali waweze kupata mikopo na fursa mbalimbali ili mwisho wa siku waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya maeneo tumeenda tumewakuta hawa vijana ambao wameacha kutumia madawa ya kulevya na wameanzisha familia zao; na wamekuwa ni raia wema kabisa, lakini hawana miradi ya kufanya. Kwa hiyo, naiomba Serikali ione namna ya kuwabaini na kuweza kuwasiadia ili mwisho wa siku waweze kurudi katika mazingira yao ya kawaida, kwa sababu hawa vijana wengine wanaingia kwenye uraibu kwa sababu ya kukosa kazi au kukosa shughuli ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kuhusu hawa waraibu, wale ambao wamezidi miaka 15, tunaona kabisa kwamba kama ni kundi la vijana, wao wana fursa; wanawake wana fursa, vijana wana fursa, lakini wale waraibu wanaume ambao wana zaidi ya miaka 35, bado naomba Serikali ione namna bora ya kuweza kuwasaidia ili kusudi na wao waweze kufaidi hizi fursa ambazo ziko hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, niliomba pia nizungumzie kuhusiana na suala la UKIMWI; hasa nilipenda kuzungumzia kuhusu tohara ya kitabibu. Inaonyesha kabisa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Janejelly, jiandae Mheshimiwa Yustina.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye bajeti ya Waziri Mkuu. Kwanza, nampongeza Waziri Mkuu kwa uwasilishaji mzuri ambao ume-*cover* mambo yote ya Kitaifa. Pia nampongeza Mheshimiwa Mama Samia kwa jinsi alivyoendelea kuinua maisha ya watumishi; na aliyowaahidi yote alitekeleza. Nina imani kubwa hata lile alilowaambia la mishahara, basi mwaka huu litatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitajikita ukurasa Na. 58 aya 107. Tunashukuru sana bajeti ya Waziri Mkuu imekuja na vitu vyote walivyofanya, jinsi walivyokagua mikataba ya kazi, jinsi walivyokagua Usalama, lakini kuna jambo wamelisahau ambalo ni muhimu sana kwenye ushirikishwaji wa watumishi. Hawajatuletea taarifa ya Mabaraza ya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabaraza haya yako kisheria kwa Tamko la Rais Na. 1 la Mwaka 1970. Mwalimu Nyerere alishaona mbali kuhusu ushirikishwaji wa watumishi. Ofisi ya Waziri Mkuu kina kitengo ambacho kinakagua Mabaraza ya Wafanyakazi; na *CAG* sasa hivi anakagua ukaaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika kwenye baadhi ya taasisi na Wizara, Mabaraza hayafanyiki kisheria inavyotakiwa. Wanafanya Baraza moja la Kupitia Bajeti kwa sababu wanajua isipopitishwa, haitapitishwa hapa Bungeni,

lakini lile Baraza la kupitia utekelezaji wa bajeti na kupanga mikakati ya taasisi au Wizara, hayafanyiki.. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaweza tukawa tunasema bajeti hazitekelezwi vizuri, watumishi hawafanyi kazi vizuri, lakini ni kwa sababu hawapati ule ushirikishwaji. Hawapangi ile mikakati ya taasisi. Baadhi ya Wizara wanachofanya, wanafanya siku hiyo hiyo mabaraza mawili. Nimekaa huko, nimeishi huko najua. Wanaanza na utekelezaji, kesho yake wanafanya upitishaji wa bajeti.

Je, sasa mikakati waliyopanga itaingia kwenye bajeti wakati bajeti imeshapitishwa? Naomba Ofisi ya Waziri, kuhusu Mkuu ukaguzi wa Mabaraza, mkayakague kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee mifuko ya jamii. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, amepeleka fedha kweli kweli kwenye mifuko ya watumishi ili wastaafu wetu walipwe. Hata hivyo, wastaafu wamebaki na changamoto mbili, huwa zinaniumiza sana. Mtumishi kabla hajastaafu kwa hiyari, Serikali humpa barua kwamba ujiandae kustaafu kwa miezi sita; lakini inapompa barua, haijiandai kutafuta zile *documents* zake zinazotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu kaanza kazi mwaka 1970, leo akifikia kustaafu, unamwambia barua ya kuajiriwa atafute yeye, kuthibitishwa kazini atafute yeye, ya cheo cha mwisho atafute yeye. Atavipata wapi? Mtumishi huyo ameshahama zaidi ya taasisi kama kumi, anaipata wapi barua ya ajira ya kwanza? Anapata wapi barua ya kuthibitishwa kazini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashauri tu, mnapompa barua ya miezi sita ile kwamba unaenda kustaafu, pangeni na zile *documents* zake peleka kwenye mfuko, tuwasaidie hawa wastaafu wetu kuumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingineni ya kutokupeleka makatako ya watumishi ipasavyo.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Kuna taarifa Mheshimiwa Janejelly.

**T A A R I F A**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kumpa taarifa mwongeaji kwamba siyo tu *documents* zinazotafutwa kwenye maeneo mbalimbali, imefika wakati mtumishi anaacha kazi, halafu anaenda kudai pensheni yake, wanamwambia tajiri yako alikuwa hajalipa michango, kwa hiyo, hatuwezi kukupa hata *pensheni.* Kwa hiyo, kwa kweli ni jambo gumu sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly taarifa hiyo.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea hiyo taarifa na ndiyo *point* niliyokuwa naenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi na Wizara hazipeleki makato ipasavyo; wanakaa, hawapeleki. Kwa hiyo, mtumishi anapofikia kustaafu, akienda kwenye mfuko, anaambiwa una *gap* la miaka miwili, una *gap* la miaka mitatu; shughulikia. Sasa huyu ameshatoka ofisini na nafasi yake imeshachukuliwa, anashughulikia kupitia wapi? Kwa nini kwenye hiyo miezi sita mwajiri asiangalie kama mtumishi wake anayo hayo mapengo akayaziba mapema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Ofisi ya Waziri Mkuu, mifuko iko chini yenu, hebu mjaribu kupeleka hata maelekezo ndani ya Wizara na Idara za Serikali wawasaidie hawa wastaafu kupanga vitu vyao kabla hawajastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, anapopandishwa daraja, hawarekebishi; na hili suala liko kwa watumishi wa Halmashauri na walimu. Sasa anafanyiwa kokotozi kwa cheo kile kilichokuwa cha zamani, analipwa malipo pungufu, sasa kuja kupata hiyo tofauti itamchukuwa

hata miaka minne au mitano au anafariki kabla hajalipwa. Naomba na hilo mliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye michezo. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mwana-*sports* namba moja, lakini hii michezo ya Idara ya Wizara za Serikali tumeifanyia utani. Leo hii bajeti zote zitapita hapa, lakini angalia kila Wizara imeweka bajeti kiasi gani kwenye michezo? Michezo hii ina faida kwa watumishi, huwa inatufanya tunafahamiana, tunashirikiana na tunajenga afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yalipokuja maelekezo ya Katibu Mkuu Kiongozi kwamba kila Wizara ishiriki michezo, sasa taasisi nyingine wanachofanya, wanapeleka mshindani wa baiskeli mmoja na wacheza bao wawili. Wanasema taasisi imeshiriki na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia kiti chako, Ofisi ya Waziri Mkuu itilie mkazo hili la michezo ndani ya Idara za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi hapa Menejimenti ya Utumishi wa Umma wamejibu swali kuhusu watumishi waliosimamishwa kazi na kesi zao hazijaisha. Zinachukuwa muda mrefu; miaka mitatu mtumishi yuko nyumbani anasubiri hatma ya kesi yake. Mtumishi huyu anaporudi kazini, utendaji umekwisha, muda wa kustaafu umefika; na hapa katikati mnapoteza ambapo angeweza kupata hata *promotion* nyingine, anastaafu kwa cheo cha chini, lakini ni kwamba eti *evidence* hamna. Sasa kama ushahidi huna, ulimsimamishaje huyu? Naomba tuangalie hawa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa Serikali Kuu, lakini kipindi ambacho nimekuwa Diwani kwenye Halmashauri, nimegundua mengi kwenye Halmashauri zetu, watumishi wananyanyaswa kiajabu. Naomba tu, ukiangalia watumishi wa Halmashauri, mwajiri ni TAMISEMI, mpandisha daraja ni TAMISEMI, lakini ikifika nidhamu, tunasema Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuliangalie kwa makini sana hili. Hata nidhamu yao irudi kwa yule anayemwajiri. Tunawaumiza sana watumishi ambao wako Halmashauri. Naomba hili tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tuangalie mahusiano ya viongozi na watumishi wao. Viongozi wengi wamekuwa ni watoa maelekezo, sio wa kushauriwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kengele ya pili.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Yustina, jiandae Mheshimiwa Venant.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Naelekeza mchango wangu kwenye changamoto hii kubwa ya ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wanamaliza kusoma katika madaraja mbalimbali, lakini wanapata changamoto kubwa sana ya kutafuta ajira ili waweze kujikimu kwa maisha. Tunafahamu kwamba kwa demokrasia ya nchi yetu idadi kubwa ni vijana, asilimia 35 ni vijana wenye umri wa kuanzia miaka 15 mpaka 35. Hao ndio nguvu kazi tunayoitegemea, hao ndio wenye ari na morali wa kuijenga nchi yetu ambayo tunafikiria tunaingia kwenye uchumi wa kati, lakini hautajengwa na wazee utajengwa na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *crises* ya ajira ni kubwa sana na sisi wenyewe tunaiona, hebu ona ukitangaza nafasi 100 ya ajira, *applicants* walivyo wengi ni elfu na zaidi, sisi wenyewe tukija huku Bungeni tumebeba mabahasha ya vijana wetu,

wanataka kazi. Wengine wanao-*sustain* maisha pengine wanafanya kazi ya boda boda au wenye miamala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, boda boda wanakaa vijana kwenye kituo kimoja 20 au 40 akisubiria mteja akiwa na *stress* ya kufikisha mahesabu ya tajiri wake na ndiyo maana pengine wanapata ajali na wanaishia kukatwa viungo vyao. Nafikiri tuliangalie vizuri hii *crises* ya ajira na tunaona kwamba kwa mahesabu *Word Bank* kwamba kila mwaka Tanzania kuna vijana kama 800,000 wanaingia kwenye soko la ajira, fikiria kuna mwaka juzi hawajapata ajira, wa mwaka jana, mwaka huu na hatuwezi kuepuka kwa sababu tunawasomesha na tunaendelea kuzaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kuna fursa kubwa pengine kwenye kilimo, kama tutakifanya kilimo kikawa kizuri na kikavutua kwa vijana na kilimo kitakachovutia vijana ni kilimo cha bustani ya mboga mboga na maua, kwa sababu ni kilimo ambacho atapata fedha haraka sana. Nafikiria hivyo, lakini changamoto ya vijana hawana ardhi, changamoto ya vijana hawana nyenzo, wala hawana mtaji. Sasa ni kwa nini basi Serikali nilikuwa nafikiria kwa kusaidiana pengine na halmashauri, wakaweza kutafuta ardhi ya kilimo hata kwenye halmashauri, wakawapa hawa vijana kwa kuwasimamia wakazalisha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano nilikuwa naangalia kijana ukampa nusu heka ya kuzalisha labda mchicha tu ambao anaweza akapata fedha kila baada ya wiki tatu maana mchicha unaweza kuiva haraka. Katika nusu heka anaweza akapata tani nne, sawa sawa na kilo elfu nne, akiuza kwa elfu mbilimbili ana uwezo wa kupata elfu nane, fikiria ni katika wiki tatu, akitoa gharama za uzalishaji anabaki na kiasi cha fedha cha karibu shilingi elfu tano. Sasa ni kwamba sisi tuangalie hiyo namna kuwasaidia hao vijana tukawajengea mazingira mazuri ya upatikanaji wa maji, sehemu ambayo tunaona ni muhimu na maji ni kidogo tukawafungie ile mirija ya kufanya *dripping irrigation*. Ofisi ya Waziri Mkuu imejenga kitalu nyumba kwenye halmashauri lakini tunaona zile haziko *sustainable* pengine kwa sababu

wangeendelea kujenga vitalu nyumba pengine huko vijijini, lakini vijana wanashindwa kwa sababu ya hizi changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwaacha hawa vijana wakajikatia tamaa kesho ndiyo watajiingiza kwenye makundi ya majambazi na baadaye tutakuwa hatuna usalama na sisi na nchi yetu. Kwa hiyo naomba Serikali itupe jicho la pekee, wakati inaendelea kujenga fursa na ajira pengine kwenye sekta maalum basi waweze ku-*accommodate* hiki kikundi cha vijana katika kilimo kwa sababu kilimo ndiyo kina fursa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kwenye majanga au maafa. Najaribu kufikiria namna ambayo nchi yetu inashughulikia maafa, Tanzania kama nchi nyingine duniani tunapata maafa mengi, tunapata maafa ya ukame, mafuriko, vimbunga, magonjwa na kadhalika. Sasa kuna sehemu ambayo kwa kweli naipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu na nchi yetu kwamba kwa kweli wanashughulikia maafa tunaona. Kwa mfano yakija maafa labda ya ukame na mazao kukauka pengine kukawa hakuna chakula, Ofisi ya Waziri Mkuu imejipanga na nchi yetu imejipanga na nina imani kubwa kabisa kwa jitihada ya Rais wetu hakuna Mtanzania atakufa na njaa, kwa sababu kuna chakula cha kutosha kwenye maghala ya Taifa *NRFA* imenunua chakula, kwa hiyo hapo nawasifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasifu pia Kamati za Maafa zilizoko kijijini kama kule kwangu ni mfano mzuri tu Kamati za Maafa Vijijini wamejipanga, wakipata maafa ya misiba wana namna yao wanasaidiana, wamejiwekea *level* yao ya michango, wamenunua viti, maturubai, masufuria na kila kitu. Kwa hiyo wako *well equipped*, utaona kwamba ni namna gani sasa watu wameelewa namna ya kusaidiana kwenye maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shida yangu ni namna ambayo tunapambana na maafa tunapokuja kwa upande wa mifugo ambao hawajui kusema. Nchi yetu imekuwa

ikipata maafa ya kufa mifugo karibu kila wakati ikijirudia rudia. Kama tunafahamu tu kwamba kipindi cha ukame na bahati nzuri watu wa hali ya hewa huwa wanatuelekeza kwamba kipindi fulani kitakuwa cha maafa, hivi mfugaji anapopoteza mifugo yake 10, 20, 30 au hata zizi lake lote boma lake likaisha, hivyo anakosa gani mpaka hapo na hatuna mpango mkakati, hatuna *coping strategic* kama ambazo tunafanya kwa binadamu, maana kwa binadamu chakula kikipungua tunapeana *coping strategic* tutakula mara chache chakula chetu tutahifadhi, tusipikie pombe, lakini tunapokuja kwa wanyama, tunawaacha wale wafugaji wana-*suffer* peke yao, mfugaji anapoteza mifugo yake anabaki maskini. Mifugo hii ni chakula, mifugo hii ni benki yao, mifugo hii ndiyo bima ya afya akiugua mtu ndiyo inatumika, mifugo hii ni kila kitu lakini tunawaachia wanahangaika wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiria kwa nini tusiwe na mkakati *coping strategic* kwenye mifugo ni nini? Kwa nini hata wakati mwingine basi tusiruhusu pengine mifugo ikaenda kuchungwa pengine kwenye *buffer zone* au sehemu ambayo ni *reserved* kwa wakati ule wa mwezi mmoja au miwili ili ku-*risk* mifugo yetu isife kama tunavyowaachia wanakufa mizoga imezidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tufanye utaratibu mzuri hata wafugaji wakalipia kuliko wajanja wachache wachache wao wanaweza wakaingiza mifugo kwenye *game reserved,* wakatoa rushwa lakini wengine huku wakiwa na *stress* ya ukame, mifugo ikisogea kwenye hizi *buffer zone* wanakamatwa na askari na wanashughulikiwa vya kutosha.

Kwa hiyo, nafikiri Serikali sasa iangalie kwa upande mwingine jinsi ya kupambana na haya maafa. Hata hivyo, nafikiria hivi huyu mfugaji anayepoteza mifugo yake yote akabaki maskini Serikali ina mpango gani? Kwa nini isimfidie sasa mfugaji ambaye amerudi kwenye *zero point,* ndiyo wafidiwe kwa sababu siyo kosa lake, ana kosa gani kama ni hali ya ukame, yeye ametimiza wajibu wake, amepewa mifugo yake amekwenda kuchunga amerudisha jioni, kwa hiyo anapopata maafa kama haya, Serikali ijipange na

ikawafidie wafugaji ambao wanapoteza mifugo yao katika ukame wa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, yanapokuja maafa haya kwa watu binafsi, pengine ya mafuriko, yakachukua nyumba pengine tena za wazazi wetu, ndiyo nyumba ambazo siyo bora au mapaa yakachukuliwa na vimbunga, ninachoona pale ni utashi wa mwanasiasa ambaye yuko pale au ndiyo uwanja wa mwanasiasa, akienda pale na bati mbili au tatu akapigapiga picha ndiyo unafikiri ni *solution,* kumbe yule mhanga pale pengine amepoteza chakula, amepoteza mavazi, amepoteza kila kitu.

Kwa hiyo nafikiria, Ofisi ya Waziri Mkuu ione namna gani ipambane kwa sababu kwenye shida Watanzania ni sisi na kwenye raha Watanzania ni sisi, tusiache kikundi cha Watanzania wachache wanaokuwa wahanga na majanga haya, wakapata mateso siku zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huo ndiyo mchango wangu na naiunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Venant Daud, jiandae Mheshimiwa Zuena Bushiri.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili kuwa mmoja wa wachangiaji katika hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, nianze kwa kuipongeza Serikali inayoongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa inayoendelea kuifanya katika maeneo yetu na katika majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata fedha nyingi ambazo kila jimbo, kila kata na kila kijiji kuna miradi inayoendelea chini ya Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi. Katika Jimbo langu la Igalula juzi tu nimepokea fedha za kwenda kujenga Vituo vya Afya vya Tula na Kata ya Loya ambavyo wananchi hawa hawakuwa kabisa kwenye

mafikirio ya kupata huduma bora ya afya, kwa hiyo sina budi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Igalula kufikisha salamu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kujadili hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ameiwasilisha hapa yenye mambo mengi ambayo yatakwenda kusaidia wananchi wetu katika majimbo yetu. Kazi yetu sisi Wabunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali pindi inapofanya vizuri lazima tuipongeze lakini pindi ambapo wanaenda ndivyo sivyo lazima tuwape ushauri ili waweze kwenda kwenye mstari. Jukumu la kuleta maendeleo ni la sisi sote wala siyo Serikali peke yake na ndiyo maana kuna miradi ambayo wananchi wao wenyewe wanaanza kwa kujenga na baadaye Serikali inaiunga mkono. Kwa hiyo Serikali ina jukumu la kuwaletea maendeleo lakini na sisi wenyewe kama wananchi tuna jukumu la kusaidiana na Serikali kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nishauri kwenye mambo machache. Jambo la kwanza tumekuwa na miradi mingi sana ambayo ipo katika maeneo hasa miradi ya maji, tunaiomba Serikali sasa ifike mwisho miradi hii iwe inafika mwisho kuliko kuwa tunaenda vipande vipande na baadaye haileti tija. Kwa mfano, mimi nina mradi wa tangu mwaka 2019 wa kutanua maji ya Ziwa Victoria ambao umeanza kuongelewa toka mwaka 2019 katika Kata za Goweko, Igagula, Nsololo na Kigwa, lakini mpaka leo mradi huu unakwenda taratibu. Kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia bajeti hii basi tutenge fedha ambayo tutakwenda kumaliza mradi huu ambao tumekadiria wananchi zaidi ya 150,000 watanufaika na vijiji zaidi ya ishirini watanufaika na upatikanaji wa maji haya. Kwa hiyo, niiombe Serikali twende tukamalize changamoto hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote ni mashahidi tulipokea fedha ambazo Mheshimiwa Rais alikwenda kuzitafuta kule na zikaenda kila mkoa, kila jimbo. Fedha hizo zimeenda kutekeleza miradi mbalimbali, lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo fedha hiyo ipo lakini bado haijaanza kutelekeza miradi hiyo. Kwa mfano, katika jimbo langu tulipewa bilioni

moja na milioni mia tano kwenda kutekeleza barabara tatu katika kata tatu tofauti tofauti; kuna barabara ya kutoka Izumba kupitia Idekamizo mpaka Simbojigulu mkandarasi amesaini mkataba lakini mpaka leo hajaanza kazi. Vilevile kuna barabara zingine wakandarasi wapo *site* lakini hawafanyi kazi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jukumu la kuleta maendeleo ni letu sote ni kuikumbusha Serikali iweze kuongeza *speed governor* ya kuwasimamia vizuri wakandarasi hawa basi wamalize kazi na makusudio ya Mheshimiwa Rais kuwasaidia wananchi kufungua mitandao ya barabara yaweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo lakini wananchi wa Jimbo la Igalula walinituma; wana changamoto kubwa Serikali ilitoa maelekezo ya upandaji wa uunganishaji wa nishati ya umeme, wakasema zaidi kwamba kutoka shilingi 27,000 mpaka shilingi 320,000; Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa wewe ndiye baba wa Wizara zote niiombe kupitia Wizara ya Nishati iweze kuangalia kuna maeneo mengine wameyapandisha kimakosa wananchi sasa wameshindwa hata kuendeleza kupata huduma ambayo Serikali ilikusudia kuwafikishia hasa katika Kata ya Goweko Kijiji cha Goweko wamekipandisha hadhi ya kutoka shilingi 27,000 kwenda shilingi 320,000. Kata ya Kigwa, Kijiji cha Kigwa wamekipandisha hadhi kutoka shilingi 27,000 mpaka shilingi 320,000; vilevile Kata ya Igalula na kwingineko katika Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali, kama mnaona hii miji imekuwa kwa sababu wananchi wanapenda maendeleo na sisi Serikali kazi yetu ni kuwasaidia wananchi yale maendeleo yao yasiweze kuwaponyoka katika mikono yao, tusiende kuwavuna sana. Niiombe Serikali iweze kuangalia ni namna gani ya kuwasaidia angalau kushusha kufikia hata nusu au robo ya gharama hizo ilimradi wananchi wengi wapate huduma na sababu Serikali kusudio lake si kufanya biashara ni kufikisha huduma kwa wananchi niiombe Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo sasa nirudi kwenye michango na mijadala ambayo ipo katika nchi yetu kwa sasa. Kila Mbunge humu nadhani kama alifanya mikutano wiki mbili au tatu zilizopita, wamekutana na maswali mengi kwa wananchi wao hasa mfumuko wa upandaji wa bei. Bado Serikali ina haja ya kuliangalia hili suala kwa umakini mfumuko huu wa bei watu wamechukua *advantage* kwa sababu wamekwisha ona na sisi watu wa Serikali tumeanza kulalamika kuwa kuna hiki kimesababisha mfumuko wa bei, lakini kuna bidhaa ambazo hazihitaji kabisa kupandishwa bei, lakini wananchi au wafanyabiashara wameona wapitie humo humo kwa sababu na sisi kama Serikali tumeanza kulalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, leo tuna bidhaa ambazo tunazizalisha humu, zimepanda mara mbili kwa kile ambacho tulichokuwa tunakizania. Kwa hiyo kuna haja kama Serikali kuangalia huu mfumuko wa bei, tusiruhusu sasa wafanyabiashara wakaanza kupitisha mambo yao ambayo yanakwenda kuwaumiza wananchi ninyi wote ni mashahidi wakati tumeingiza fedha za UVIKO ziliingia katika majimbo yetu, miradi mingi ikaenda kutekelezwa kule tulikuwa tuna janga la *COVID-19* ilikuwa ikiendelea katika nchi yetu, lakini mfahamu baada ya fedha kupatikana wafanyabiashara walichukua fursa hiyo ya fedha nyingi zimeletwa na Mheshimiwa Rais wakapandisha vifaa vya ujenzi mara mbili tofauti na awali walivyokuwa wanauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ilipanda *cement* kutoka shilingi 19,000 mpaka tukaenda shilingi 24,000 mpaka shilingi 26,000 katika baadhi ya maeneo, lakini leo ninavyokuambia *cement* imeshuka na vita ya Ukraine inaendelea, imeshuka mpaka shilingi 18,500. sasa najiuliza kwa nini wakati ule fedha zilizopatikana walipandisha saizi wameshusha kitu gani kilichosababisha kushusha wakati nchi sasa hivi tunasema tupo kwenye janga kubwa la vita ya wenzetu kule Ukraine na Urusi, lakini bidhaa hii imeshuka. Vilevile Waziri wa Viwanda na Biashara yupo, hakuna majibu ambayo tuliyatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaishauri Serikali, iangalie huu mfumuko wa bei umetokana na nini? Mfumuko wa bei ni halali kweli bei kupanda maana sasa hivi bajaji au bodaboda tulikuwa tunaenda kwa sh.1,000 imekuwa Sh.3,000 imepanda kwa asilimia 200. Je, yale mahitaji yamepanda kwa asilimia hizo? Nauli za mabasi sehemu ya Sh.15,000 imekwenda mpaka Sh.25,000 au Sh.30,000, uhalisia wa upandaji wa gharama za uendeshaji na uhalisia wa upandaji ambao wanatozwa wananchi wetu hauendani. Kama Serikali tuone ni namna gani ya kuboresha katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo mijadala ambayo inaendelea na nataka nigusie na Serikali itusaidie, tunapoleta humu changamoto tunahitaji tuweze kutengeneza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ya pili hiyo.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiru, jiandae Mheshimiwa Azizi Abood.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuchangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Rais wetu Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana anazozifanya katika Taifa hili Mungu aendelee kumlinda na kumbariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Makamu wa Rais, nimpongeze Waziri Mkuu, Baraza la Mawaziri, Spika na wewe Naibu Spika kwa kazi nzuri mnazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi nianze kuchangia katika Sekta ya Maliasili na Utalii.

Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake za kuitangaza Tanzania kimataifa kupitia programu yake ya *Royal Tour* nakuiingizia nchi yetu mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio tunayoyapata, tunapata lakini pia tuna changamoto za wanyamapori. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kwa wananchi wanaoishi kwenye mipaka ya hifadhi. Kumekuwa na matukio makubwa mawili ya Tembo kuua wananchi na Tembo kuharibu mazao ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Kilimanjaro tunazo wilaya tatu ambazo ni Wilaya ya Rombo, Mwanga na Same ambazo zinaathirika sana na wanyamapori. Katika Wilaya ya Same vijiji vya Mahore, Muheza, Kihurio, Bagamoyo, Kalamba na Kadando vimekuwa vikiathirika sana na wanyamapori hawa kwa kusababisha vifo kwa wananchi pamoja na uharibifu wa mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatoa fidia, fidia inayotolewa na Serikali ni Sh.25,000 endapo mwananchi atakuwa ameharibiwa zao lake kwa hekari moja. Hivi tunavyoongea nimepata malalamiko kutoka kwenye Kijiji cha Mahore, aliyekuwa Diwani wa Kata ya Mahore ametuma meseji kwamba tuombe msaada kwa kuwa askari wa wanyamapori wamezidiwa na tembo na hivyo wananchi wa maeneo hayo wameacha kazi zao na kwenda kulinda tembo ili kuhakikisha kwamba mazao yao yanakuwa. Naomba sana Serikali iangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Serikali inatoa Shilingi Milioni Moja kama kifuta machozi kwa mwananchi ambaye ameuawa na tembo. Kulingana na hali ya maisha ambayo tunayo sasa hivi na kupanda kwa vitu, viwango hivi tukiviiangalia haviendani na hali ya maisha. Baba huyu au Mama huyu ambaye atuuawa na tembo, ameacha familia ambayo yeye ndiye alikuwa akitegemewa kiasi cha Shilingi Milioni Moja hakiwezi kusaidia chochote. Naiomba Serikali yangu sikivu, iangalie kwa makini fidia hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote Serikali hii sasa hivi tunayokwenda nayo ya Mama Samia Suluhu Hassan, ni lazima tumpongeze kwa kuwa anajaribu sana kutatua matatizo ya Hifadhi za Wanyama. Tushirikiane Serikali pamoja na wananchi ili tuangalie ni nini ambacho kinaweza kuzuia wale wanyama wasisogee katika makazi ya wananchi ili kulinda mali zao pamoja na uhai wao. Niiombe Serikali kupitia Bunge hili Bajeti ya 2022/2023 iongezwe katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo naomba sasa niende katika sekta ya barabara. Niendelee kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri ambayo imefanya, kwa kujenga barabara zetu nchini kote. Niiombe Serikali imalize barabara ambazo zimejengwa vipande vipande ili ziweze kumalizika na wananchi waweze kufaidi katika shughuli zao za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee barabara ambayo imejengwa vipande vipande barabara ya Same – Mkomazi. Hivi karibuni Kamati yangu ya Uwekezaji Mitaji ya Umma tukiwa kwenye ziara tulitembelea Hifadhi ya Mkomazi. Katika mojawapo ya mambo ambayo wameomba Serikali iwasaidie ni barabara ya Mkomazi - Same. Wamedai barabara ile ni fupi kwa wale ambao wanatokea Tanga na Dar es Salaam wanaifahamu, lakini wamesema watalii wengi wanaotokea Dar es Salaam na Tanga wanapenda barabara ile kwa kuwa ni fupi, lakini barabara ile imejengwa vipande kwa vipande, imeanza Kiurio kipande, ikaachwa Ndungu kipande, Maore kipande, Kisiwani kipande.

Mheshimiwa NaibU Spika, hivyo wanaiomba Serikali Hifadhi ya Mkomazi *Game Reserve* imetuma Kamati ya *PIC*, Mwenyekiti wangu yupo pale atathibitisha kauli hiyo. Tuiombe Serikali ili watalii wale waweze kupita njia iliyo rahisi kufika katika hifadhi na barabara ile ikiboreshwa kwa madai yao watalii wetu watapata urahisi wa kufika katika hifadhi vizuri na kwa usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niendelee kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana inazofanya na niendelee kuiomba Serikali iangalie yale matatizo ambayo yanawagusa sana wananchi wa Tanzania, kama vifo na kuharibiwa mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Aziz Abood, jiandae Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza nichukue fursa hii ya kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri Mkuu na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi nimesikia wakizungumzia kuhusu kilimo na ajira. Tatizo kubwa ambalo lipo sasa hivi ni vijana wengi kukosa ajira, lakini njia fupi na njia nyepesi duniani kote kuondoa uhaba wa ajira ni kilimo na hasa kilimo cha umwagiliaji. Tanzania tuna kila aina ya uwezo wa kufanya kilimo cha umwagiliaji. Tuna maziwa, tuna mito, tunaweza tukajenga mabwawa makubwa ya kuweza kukinga maji ya mvua na kufanya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijikite kwenye kilimo kimoja tu cha mpunga. Kilimo cha mpunga Tanzania tunaweza kuwa wazalishaji wakubwa Kusini mwa Afrika na Bara zima, kama tutaweza kutumia ardhi yetu vizuri katika kilimo hiki cha mpunga na hasa kilimo cha umwagiliaji. Kwa mfano, Morogoro tuna eneo linalofaa kwa umwagiliaji hekta 1,510,339 wakati eneo hilo sasa hivi linatumika hekta 40,558. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali tujaribu sana kujikita upande huo na ajira kubwa itatoka kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudi Jimboni. Morogoro tuna tatizo kubwa la maji, tunao mradi wa maji wa *AFD* wa Shilingi Bilioni 180 lakini mpaka leo hii bado ni hadithi tu, kila siku tunasaini, tunatangaza, tunafanya hivi, tunafanya hivi. Ninaiomba Serikali itusaidie ili mradi huu uweze kutekelezwa usaidie Manispaa ya Morogoro na Morogoro unajua ni sehemu ya uwekezaji mkubwa unahitaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wawekezaji wanakuja kitu cha kwanza wanauliza maji yapo? na sisi tuna upungufu mkubwa sana wa maji na hasa katika Mji wa Morogoro maeneo mengi sana yamepata miradi midogomidogo ambayo Serikali imetoa pesa zake lakini imetoa pesa kutengeneza tenki, kupeleka mabomba lakini mabomba ya kusambaza kwa wananchi haikutoa pesa. Kwa hiyo, ninaomba Serikali itufikirie katika Bajeti hii 2022/2023 kutupatia pesa katika miradi hii ili iweze kupunguza kero ya maji katika Manispaa ya Morogoro, kusambamba mabomba kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kero ingine katika Halmashauri ya Morogoro tuna stendi mpya ambayo kijiografia ya Manispaa ya Morogoro iko mbali na wananchi. Kwa hiyo, wananchi wana safari ndefu ya kwenda kupanda basi kule wa mabasi ya daladala haya. Tuna stendi ya zamani iko Mjini Manispaa ya Morogoro, lakini nashangaa stendi ile haitumiki lakini imeamuliwa yale mabasi yapaki barabarani palepale karibu na stendi wakati Halmashauri inapoteza Shilingi Milioni 32 kwa mwezi. Tungeruhusu yale mabasi yaingie pale ingeweza kulipa hata deni ya stendi mpya. Kwa hiyo, mimi ninaiomba Serikali irudishe stendi ya zamani ili iendelee kutumika, wananchi wa Morogoro wapate huduma kwa sababu eneo kubwa la Morogoro linatumika ni stendi ya Morogoro Manispaa ya Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya Afya tuna Hospitali ya Wilaya. Hii hospitali ya Wilaya tumepewa Shilingi Milioni 500 tu ambazo zimefika kujenga *OPD* na Maabara, hakuna maeneo ya kulaza wagonjwa. Kwa hiyo, tunaomba Serikali Mradi huu tuumalize kwa sababu huu mradi una miaka

saba sasa, tunaomba Serikali itumalizie mradi huu ili tupate na wodi za wagonjwa katika Hospitali hii ya Wilaya ya Morogoro. Katika bajeti tulitengewa Milioni 500 hazitoshi, tunaomba tuzidishiwe ili tumalize, kwa sababu Hospitali ya Mkoa wa Morogoro imeelemewa. Kwa hiyo, tunaomba na Hospitali ya Mkoa wa Morogoro nayo iweze kupata upanuzi wa majengo yake ili nayo iweze kupokea wagonjwa wengi zaidi, kwa sababu Morogoro ni katikati ya Miji yote, wagonjwa ni wengi, ajali zinatokea nyingi zinahitaji Hospitali ya Mkoa wa Morogoro ya Rufaa ipanuliwe iwekwe majengo mengine yaongezwe ili iweze kutoka huduma vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa ushauri kwa Serikali kwa sababu sisi Wabunge tuna wasaidizi. Wasaidizi wenyewe katika Majimbo yetu ni Madiwani, Madiwani wasaidi wao ni Wenyeviti. Kwa hiyo, mimi ninaishauri Serikali hali ya Madiwani na Wenyeviti na hasa Madiwani hali zao katika kipato ni kidogo sana. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali tuwaongezee kidogo ili wafanye kazi vizuri, hata sisi Wabunge tunapokwenda kwenye Kata zao tunakuta kidogo kumechangamka na wameweza kuzungukia Kata zao. Kwa hiyo, maslahi yao tuyaboresha kidogo Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa, tuwape posho za kuweza kujikimu katika kutumikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kaboyoka, jiandae Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Mimi nitajikita zaidi katika ule ukurasa wa 32 wa hotuba hii ambayo imezungumzia juu ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwamba jambo hili tatizo kubwa la wafugaji na wakulima limekuwa ni janga la Taifa. Watu wameuana kwa ajili ya mipaka, wafugaji

wakienda kulisha kwenye mashamba ya wakulima, sasa mimi naomba kwa vile Waziri Mkuu yupo hapa akihitimisha hotuba yake alitueleze hii Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, kazi yake kubwa ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua wazi kwamba nchi yetu ni kubwa sana yenye *square kilometers* 947,303 ukiondoa 61,500 unabaki na 885 ambayo ndiyo ukubwa wa ardhi yetu. Kwa sehemu ya kilimo amesema kwamba ni hekta milioni 44 ambazo zinafaa kwa kilimo, ingawa mpaka sasa hizi ni hekta 14.5 Milioni ambazo zinatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia yote haya ni kwamba nchi yetu haitilii umuhimu wa wafugaji, wanaona wafugaji ni watu tu wa kuswaga ng'ombe na kukimbia huku na huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwamba nchi yetu inaringa kwamba ni nchi ya tatu katika Afrika kwa kuwa na mifugo mingi Milioni 25, lakini hotuba ya Waziri Mkuu inaonyesha kwamba katika hizo ng'ombe Milioni 25 pato letu limekuwa ni Dola za Marekani Milioni 22,400. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikilinganishwa na wenzetu wa Kenya ambao wao wameweka msisitizo kwenye kufuga kisasa, *zero grazing*. Utakuta kwamba wao pato lao ni karibia Bilioni Moja za Marekani, wakati ng'ombe wao wanaofuga ni Milioni 21 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Milioni 25 ya ng'ombe wetu wa Tanzania asilimia 98 ni wa kienyeji na wanafugwa kienyeji. Ukiangalia nchi ya Denmark ambayo ina ng'ombe 1,500,000 wao wamepata Milioni 330 USD kutokana na mauzo ya ng'ombe. Kwa hiyo, tunachojiuliza ni kwamba hivi Tanzania tutangoja lini wananchi wetu waendelee kuuana, wafugaji na wakulima kwa ajili ya ardhi, wakati tuna ardhi kubwa lakini haijapangiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia unakuta kwamba takwimu zinaonyesha eneo la kulima ni kiasi gani,

lakini takwimu hazionyeshi eneo la wafugaji ni kiasi gani. Swali ninalojiuliza ni kwamba hawa wataalam wetu wa ugani wa mifugo wao hawajui faida ya *zero grazing* wala hawajui faida ya *cross breeding* kiasi kwamba ng'ombe wetu wote ni wa kienyeji ni kiasi kwamba tuna ng'ombe lakini wasio na tija? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kwamba Serikali yetu kwa vile imeunda Wizara nzima ya Mifugo, Wizara hii ije na mpango mkakati mzima wa kutuonyesha kwamba imetengwa ardhi kiasi gani ya wafugaji na wafugaji hawa wangapi wameshapewa maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wawekezaji wameweza kutengewa nafikiri Milioni 200 *hectors*, kwa nini wafugaji wetu wasitengewe maeneo ya kulima? Ni kwamba tunaamini kwa watu wa nje kuliko watu wetu wenyewe, hata fedha hizi ambazo Waziri Mkuu ameweka hapa kuonyesha kwamba ndiyo zimepatikana, naamini sehemu kubwa ni wafugaji wenyewe waliohangaika kuingiza pato hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mara nyingi wanasema wafugaji wapunguze ng'ombe, lakini hawajaweka kiwango kwamba wapunguze kutoka kiasi gani ifikie kiasi gani, na wakipunguza wanawasaidia nini katika malisho yao na maji yao. Maana wafugaji wanafugaji wanafuga ng'ombe wengi wakijua kwamba hata nusu wakifa watabaki na nunu. Sasa Serikali unapoendelea kusema punguzeni mifugo bila kuweka idadi hujawasaidia wafugaji wala wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine hebu tuangalie hizi Ranchi zetu utakuta kwamba ukienda kama kwenye Ranchi ya Kongwa ina eneo kubwa sana ambalo limetengewa kufuga lakini *productivity* ya pale haiendani na eneo lile. Hawa ni watu wamewekwa pale wanalipwa mshahara, lakini *production* ni ndogo mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba kwa nini Serikali isiangalie haya maeneo nakuona kwamba kama

hawa wanaoendesha hizi Ranchi hawawezi kwa nini wasiwape wafugaji wakafanya kazi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali imeweza kuhamisha wafugaji kutoka Ngorongoro kwenda Handeni, kitu gani kinashindikana kuhamisha wafugaji wale wenye ng'ombe wengi na kuwapeleka kwenye maeneo ambayo wametengenezewa kwa ajili ya ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wenzetu wa huko Kenya tunasema kwamba wanaofuga ni wale ma-*settlers* lakini *what does it mean*, *settlers* ina maana wamefanya *zero grazing* na wanaweka miundombinu yote inayotakiwa, sisi tunashindwaje ku-*settle* wafugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiona ni hapa kwamba Serikali ipo tayari kupeleka hela nyingi kwenye migodi tubaki na mashimo baada ya miaka 100 ijayo, kuliko kusaidia wafugaji wetu na kuwaweka mahali, wakawatengenezea *biogas*, wakawapandia majani, wakawasaidia ile *slung* ya *biogas* wakapandia kama mbolea ikasaidia katika kukuza majani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mna kazi kubwa ya kufanya, hamjatu-*impress* kwenye upande wa wafugaji. Kwa ajili hiyo, hatuna haja ya kuringa kwamba tuna ng'ombe wengi maana wale ng'ombe wote wamechoka na wachungaji wamechoka hawana tija. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Maimuna Mtanda jiandae Mheshimiwa Hassan Kungu.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai ambayo ametupatia. Lakini kipekee niipongeze Ofisi ya Waziri Mkuu kwa wasilisho zuri la hotuba ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo imefanya jitihada

kubwa, ya kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ambayo ndicho kichocheo kikubwa cha maendeleo ya kiuchumi katika nchi yetu. Wamefanya hivyo, tumeshaona, wote ni mashahidi. Ukienda Mkoa wa Dar es Salaam utakuta Daraja la *Tanzanite* lakini pia kuna *Flyover* mbalimbali, na katika maeneo mbalimbali Serikali yetu imejitahidi kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji. Sababu ya kufanya hivyo ni kuchochea maendeleo ya wananchi na mtu mmoja mmoja kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia, niende sasa kwenye sekta hiyo ya usafiri na usafirishaji katika Mkoa wetu wa Mtwara. Tuna kilio cha muda mrefu cha barabara ya Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala hadi Masasi, kilomita 210. Tunaishukuru Serikali kwamba tarehe 25 Novemba, 2021 ilisaini mkataba wa mkopo wa shilingi bilioni 268 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika; tunashukuru kwa hilo. Sasa, ni yapi matarajio ya wananchi ambao wameteseka muda mrefu? Wananchi wanatumia gharama kubwa sana za nauli kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwa sababu ya ubovu wa barabara. Kwa hiyo, wanachotarajia wananchi hivi sasa baada ya kusaini mkopo ule ni kuona ujenzi unaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kusini wameshaumwa na nyoka na sasa wakiona jani hushtuka, bado hawajaamini kama kweli barabara ile pamoja na kusaini mkopo itajengwa. Hii ni kwa sababu ahadi nyingi zilishapita huko nyuma, tukaelezwa pia na idadi ya wakandarasi, ambao wanakwenda kujenga barabara hizo, lakini ilipita na ahadi hizo ziliyeyuka. Sasa, leo tumeshapata hizo fedha, tunachotarajia sisi wananchi wa Kusini ni kuona kwamba barabara ile ya kiuchumi, ambayo inasafirisha zao la korosho linaloipatia nchi hii fedha nyingi za kigeni; ni barabara hiyo sasa kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujengwa kwa barabara ile kuna manufaa sana. Kwanza kutachochea maendeleo ya Bandari ya Mtwara ambayo Serikali imewekeza fedha nyingi lakini matumizi yake hadi sasa sio ya kuridhisha. Lakini vilevile

kutokana na barabara na Bandari ile maendeleo ya wana Kusini hasa wa maeneo ya Mtwara yatachangamka, kutakuwa na kima mamalishe watapika pale Bandarini na pia wauzaji wa bidhaa mbalimbali nao watauza kwa sababu bandari sasa itakuwa *active*.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya miundombinu ya usafiri katika Mikoa ya Kusini kwa ujumla bado si nzuri, sio nzuri kabisa kiasi kwamba umasikini unazidi kuongezeka kwa wananchi badala ya kutoweka. Sasa hivi barabara ya kutoka Newala kwenda Amkeni – Kitangali – Mtama; barabara ile hata wale waliokuwa wanapeleka mabasi yao hawapeleki tena. Mabasi yanayopita kwenye njia hizo yameharibika, mabasi ni mabovu hayamalizi safari. Kwa hiyo, wananchi wanazidi kudidimia wafanyabiashara hawawezi kupeleka magari yao kwa sababu, wanakwenda kuangamiza hayo magari yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *effect* ya hivyo ni kwamba uchumi wa mwananchi mmoja mmoja unazidi kudorora. Niiombe sana Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi ifanye kweli, miundombinu ile iboreshwe ili uchumi wa wananchi wale nao upate kuchangamka.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya Mtwara iko mingi lakini hiyo mingi haitekelezeki. Kulikuwa na suala la reli ya kutoka Mtwara kwenda Mbamba Bay, tuliambiwa kwamba mwaka 2019 Juni mkataba ungesainiwa wa ujenzi wa reli ile lakini mpaka leo hakuna kinachoeleweka. Lakini pia, kuna *Mtwara Development Corridor,* imesemwa sasa hivi imepotea. Haya mambo yakiendelea hivi tunazidi kuwapoteza watu ambao wangezalisha chakula lakini pia tungepata manufaa makubwa sana kama ile miundombinu ya usafiri ingeweza kuboreshwa. Tunazo tani nyingi tu za makaa ya mawe kutoka Mchuchuma ambayo yangepita kwenye reli kwenda kwenye Bandari ya Mtwara. Hii kwa sasa haiwezekani kwa sababu reli hiyo haijajengwa hadi hivi tunavyoongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la bandari bado ni kizungumkuti. Pamoja na Serikali kuwekeza fedha nyingi, kitu pekee ambacho kilikuwa kinapita kwenye Bandari ile ni korosho peke yake. Sasa korosho ina msimu, si muda wote. Sasa hivi tunamshukuru Dangote kwamba *cement* yake anataka kupitishia kule. Lakini basi tuchangamshe na hivi vingine ili Bandari ile ilete manufaa ambayo Serikali imeikusudia kwa wananchi wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuhusu suala la umeme. Umeme si anasa, umeme ni ulinzi kwa sababu wote tu mashahidi kinachoendelea nchi jirani ya Msumbiji wote tunakifahamu. Lakini wananchi wa Newala, hasa wa Newala vijijini wako gizani. Newala vijijini ina vijiji 107 lakini ni vijiji 33 tu ndivyo vyenye umeme. Vijiji 74 havina umeme. Sasa, vijana wetu wanajiajirije kama hakuna umeme katika maeneo yao? Lakini je, ulinzi na usalama wa wananchi wa Newala ukoje kama wanaishi gizani mpaka leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali ilituletea mkandarasi tangu Agosti mwaka jana, anaitwa *Central Electrical International Limited.* Lakini tangu akabidhiwe mradi mwaka jana Agosti, kati ya vijiji 74 ambavyo havina umeme amevipitia mpaka leo hii vijiji 21 tu. Na hivyo 21 si kwamba ameshasimamisha nguzo, bado mpaka leo sasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Maimuna ya pili hiyo.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Kungu jiandae Mheshimiwa Innocent Kalogeris.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Na mimi pia niungane na Wabunge wenzangu kuipongeza bajeti hii ya Waziri Mkuu. Nimpongeze Waziri

Mkuu pamoja na wataalam wote waliohusika kuiandaa bajeti hii. Lakini pili, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kutupa miradi mingi kwenye majimbo yetu na sisi Wabunge wote ni mashahidi, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, nianze kwa kuchangia upande wa afya. Wilaya ya Tunduru tuna Hospitali ya Wilaya ambayo ni kongwe kweli kweli. Hospitali ile imejengwa mwaka 1905, majengo yake mpaka hivi sasa ni chakavu kweli kweli. Niliwahi kukutana na Waziri wa *TAMISEMI,* kwa kipindi kile, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, nilipiga picha ile hospitali majengo yake nikamuonyesha ili kutaka kuomba fedha ya ukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ummy Mwalimu yeye mwenyewe akaridhia akasema kwamba, majengo haya kama tunakarabati ni sawa na kupoteza fedha za Serikali. Kwa hiyo, tukashauriana kwamba nitafute eneo ambalo tunaweza kupata hospitali mpya ya wilaya. Bahati nzuri tumepata hekari 20 ambapo tunaweza kujenga hospitali mpya ya wilaya, pamoja na nyumba za watumishi wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uchakavu wa hospitali ile ya wilaya bado pia ina idadi chache sana ya watumishi. Ikama yake ni asilimia 55 katika 100. Lakini pia, katika hospitali ile tunao pia uhaba wa mtoa huduma wa mionzi, yupo mmoja tu. Sasa anapopata dharura ya kuugua ama akasafiri kwa muda wa wiki nzima maana yake huduma ya *X-Ray* inakosekana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru hotuba hii ya Waziri Mkuu imezungumzia watumishi kwa hiyo, niombe watumishi watakapopatikana basi tuangaliwe sana katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru. Lakini pia, upande huo huo wa afya tukienda kwenye vijiji vyetu kuna zahanati, lakini katika zahanati zile bado watoa huduma wa afya ni wachache mno. Zahanati nyingi zina mtoa huduma wa afya mmoja mmoja. Tunazo zahanati takriban 11 ambazo zina mtoa huduma wa afya mmoja mmoja. Kwa mfano, Zahanati

za Kidodoma, Nampungu, Majala, Cheleweni, Kitanda, Twende Mbele, Kajima, Kalulu, Mkowela pamoja na Zahanati ya Machemba. Hizi zote zina watoa huduma wa afya mmoja mmoja. Sasa, wanapopata changamoto ama dharura ya kawaida, ama siku wanakwenda kupokea mshahara mjini basi zahanati zile huwa zinafungwa na watu wanakosa huduma kabisa ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia upande wa elimu, nako kuna walimu wachache kweli kweli. Shule nyingi zina walimu wanne mpaka walimu watatu. Kwa hiyo tunaomba ajira hizi za walimu zikipatikana basi tuangaliwe kwa macho mawili kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutupatia shule za sekondari, na shule zile tayari tumeanza kuzijenga. Lakini kuna jambo ambalo limejitokeza, ama *BOQ* inaeleza kwamba tujenge kwa kuilaza tofali. Sasa, tunaona, tangu tumeanza mwanzo shule nyingi zinajengwa kwa tofali za inchi sita, na tofali zile zinakuwa zimesimama na majengo yanadumu na yapo mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, *BOQ* inaeleza kwamba tulaze tofali kwenye majengo yote. Sasa tukiangalia kwa namna ya wingi wa majengo na idadi ya fedha iliyopo kwa kweli tunaona kana kwamba bado haitoshi, na kwamba tutahitaji fedha iongezeke zaidi. Kwa hiyo, kwa namna ya kujenga tofali kwa kuilaza kwa kweli bila shaka tunaweza kuwalaumu Wakurugenzi, kwa sababu ya kwamba fedha haikidhi majengo ni mengi. Kwa hiyo, niishauri *TAMISEMI,* kupitia wakandarasi wake ama mainjinia waangalie namna nyingine ya kuweza kutoa *BOQ*, ambayo inaeleza tujenge tofali la inchi sita kwa kawaida kwa namna tunavyojenga ya kusimama badala ya kulaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Tunduru tulikuwa na uwanja wa ndege. Uwanja wa ndege ule una miaka zaidi ya 20 sasa haufanyi kazi, na kwa tafsiri sahihi ni kwamba umesimama ama umefungwa kabisa, haupo; na eneo lile

lipo katikati ya mji. Kwa hiyo nilikuwa naomba Serikali, ikiwezekana eneo lile litolewe na wagawiwe wananchi ili wafanye shughuli za maendeleo, kama vile ujenzi wa nyumba za makazi; nilikuwa naomba sana hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuhusu miundombinu ya elimu ya msingi, ambayo kwa kweli ni mibovu sana. Tunaishukuru Serikali kwa fedha ile za UVICO upande wa elimu ya sekondari tuko vizuri. Sasa, nilikuwa naomba tugeukie kwenye upande wa shule za msingi. Miundombinu ya elimu ya shule za msingi imechakaa mno, tena sana. Lakini pia, shule hizo hizo za msingi pamoja na miundombinu hiyo ya elimu hazina vyoo kabisa. Unakuta shule moja ina uhaba wa matundu 22, shule nyingine ina uhaba wa matundu 30. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana kwenye upande huu, basi na sisi tuweze kukaa sawa sawa na hatimaye tuweze kuboresha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunavyo vituo vya afya ambavyo vinafanya kazi vizuri lakini pia, vituo vile, kwa mfano Kituo cha Afya cha Nakapanya jengo la upasuaji limekamilika. Tunayo *Ambulance,* tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kwenye kuomba kura tulimuomba na alituahidi kutuletea; na tunamshukuru tumepata *Ambulance*. Hata hivyo upasuaji haufanyiki kutokana na kwamba tumekosa baadhi ya vifaa vichache ili hospitali ile, tuweze kupata huduma ya upasuaji na hatimaye tumsaidie mama na mtoto. Vilevile katika Kituo cha Afya cha Matemanga majengo yote yamekamilika na vifaa vyote... *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa, taarifa, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nataka nimpe taarifa kaka yangu Hassan Kungu kwamba, ni kweli kabisa kile Kituo cha Afya

cha Nakapanya, kutoka Nakapanya mpaka Makao Makuu ya Wilaya ni kilomita 80, ambapo wanawake wengi sasa wamekuwa wakijifungulia njiani. Sasa ni vizuri sasa Serikali ikasaidia kuleta hivyo vifaa kukamilisha kwa haraka sana ili wanawake hao wasiendelee kupata adha hii ambayo wanajifungulia barabarani. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante! Haya ahsante! Mheshimiwa Hassan, taarifa hiyo.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa hii kwa mikono miwili. Lakini pia, kwa kuongezea hapo, akina mama wajawazito huwa wanakwenda Wilaya ya Jirani ya Nanyumbu kwenda kufuata huduma ya upasuaji, na hatimaye Mbunge wa kule huwa ananitania sana kwamba hatuna Vituo vya Afya. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Serikali tupate hivyo vifaa tukamilishe na tuweze kutoa hiyo huduma. Lakini pia, Kituo cha Afya cha Matemanga majengo yote yamekamilika vifaa vyote vipo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri, muda wako umekwisha.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent, ajiandae Mheshimiwa Wambura Annastazia.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaitenda akiwa kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakumbuka katika Bunge lililopita

nilisema kwamba mama huyu anatosha, na ni kielelezo tosha kwamba tumeshuhudia utendaji wake wa kazi uliotukuka. Sasa hivi majimboni mambo mazuri, sisi Wabunge tuko vizuri tukiamini kabisa kwamba utendaji wake wa kazi unatusaidia katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo anaitenda ndani na nje ya Bunge, akiwa kama Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Na nimpongeze kwa bajeti nzuri ambayo ameileta imesheheni katika kila sehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini ikipita na tunaamini itapita, na kwamba italeta matokeo mazuri katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya chama changu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi nijikite moja kwa moja katika kuchangia hoja. Cha kwanza, nichangie hoja katika hotuba yake namba 57 ukurasa wa 33 ambayo inaonekana itakuwa mwarobaini wa migogoro ya wakulima na wafugaji. Tumeona hapa Serikali imepanga katika mwaka huu wa fedha kutengeneza mashamba darasa katika Wilaya ya Handeni na Longido. Niiombe Serikali, Mkoa wa Morogoro vile vile ni Mkoa ambao una migogoro mikubwa ya wakulima na wafugaji, lakini una ardhi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba katika mwaka ujao wa fedha au mwaka huu wa fedha wangeweka utaratibu wa kutengeneza mashamba darasa katika Mkoa mzima wa Morogoro na ikiwezekana Mkoa wa Pwani ili wale wafugaji wenyeji walioko pale wapate utaalamu wa kutengeneza haya mashamba darasa, ili wawe na utaratibu kwamba, Januari atalisha hapa, Februari atalisha hapa, Machi atalisha hapa, mpaka mwaka mzima unapita na kuacha kwenda kuzurura ovyo kuchunga na kuingia katika migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo uliifanya katika utunzaji wa mazingira Kitaifa katika Mbuga ya Ngorongoro. Ninaamini kabisa Ngorongoro ni urithi katika Taifa hili, kuendelea kuiachia watu wakaivamia, tutakuwa tunapoteza urithi huo, lakini kubwa zaidi tutapoteza fedha nyingi za kigeni ambazo zinasaidia katika kuendesha nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hili alilolifanya kama Waziri Mkuu, na ninaamini alishirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Mazingira, sasa hivi tujielekeze katika kukabiliana na janga lingine la migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo mbalimbali katika mkoa huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kama tumeweza kupata hekta 500,000 ambazo Serikali imezipata Handeni, Tanzania bado ina maeneo makubwa ambayo tunaweza kwenda kuyapima na kuwapeleka wafugaji wakakaa huko wakanusuru mifugo yao katika kipindi cha kiangazi na tukaondokana na migogoro mikubwa ya wakulima ambayo haina sababu. Hili ni janga kubwa huko tuendako kama Serikali haitalisimamia na kulichukulia kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini Mheshimiwa Waziri Mkuu akiamua na timu yake; Wizara ya Mifugo, Wizara ya Ardhi, wanaweza waka-*allocate* maeneo mbalimbali katika Tanzania yetu kama vile tulivyofanya Handeni tukapeleka huko nako wafugaji wengine wakakaa wakajengewa miundombinu ya barabara, maji na nyumba. Leo hii tunaambiwa kwamba tumepata ardhi, tumepata nyumba na tayari 101 zimeshajengwa kati ya nyumba 300; visima vinne vimeshachimbwa kati ya visima 13. Naamini Serikali ikiamua inaweza. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kama watu walivyokuwa wanapiga kelele kwamba tunafanyaje katika kunusuru mifugo? Tunafanyaje katika kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji? Naamini kama hii Serikali itashughulikia hili, itakuwa imetusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikwambie, kuwaachia Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji, haitawezekana kabisa kwa sababu hili tayari limeshakuwa janga kubwa na hawana uwezo nalo. Kinachotokea sasa hivi, tutakuja kufika mahali tutagombana kati ya wachuguliwa na watendaji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala la barabara. Tumefanya mambo mengi, naipongeza Serikali yangu kwa kazi kubwa iliyoifanya. Kuna suala la *TARURA,* tulipata shilingi bilioni 1.5. Naomba na ninaielekeza Serikali, ikiwezekaa *TARURA* waongezewe fedha ili waweze kujenga madaraja huko vijijini. Kwa baadaye, naiomba Serikali ikiwezekana kuwe na *special program* kwa majimbo na wilaya zilizokuwa pembezoni ili ziongezewe fedha zaidi katika kutekeleza majukumu yake ya kutengeneza barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naipongeza Serikali kwa suala la *TANROADS.* Tumepata lami katika Barabara ya Bigwa – Kisaki yenye kilometa 15, tunasubiri mkandarasi tu, muda wowote aanze kazi. Pia kuna barabara yenye kilometa 63 kutoka Kiloka kwenda Mvuha, tayari tunatarajia kuitangaza. Ombi langu kwa Serikali, barabara ya Bigwa – Kisaki yenye kilometa 140 kwenye mradi wa umeme, lakini vilevile kwenye hifadhi ya Mwalimu Nyerere, ni hifadhi ambayo utalii wake utaweza kuwa mkubwa kama tukifika katika kilometa zilizobakia 40. Naiomba Serikali kushughulikia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali katika suala la afya. Wilaya ya Morogoro Vijijini, hospitali yao imekamilika; vituo vya afya, sita vipo; changamoto zetu, nianze na kimkoa. Mheshimiwa Mbunge wa Morogoro Mjini amezungumzia Hospitali ya Rufaa ya Mkoa; Morogoro ni katikati, lakini hakuna Hospitali ya Rufaa, tuna Hospitali ya Mkoa. Tunaiomba Serikali itujengee Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Morogoro ili tuweze kunusuru maisha ya watu katika ajali za barabarani zinazotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna changamoto ya uhitaji wa vifaa tiba na dawa na majengo ya *OPD* katika Halmashauri ya Morogoro vijijini…

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango mzuri wa Morogoro na maeneo mengine.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wambura, jiandae Mheshimiwa Daimu Mpakate.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii. Pamoja na kumshukuru Mwenyezi Mungu, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Ofisi yake kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya bajeti ya ofisi yake, lakini pia kwa kuiwasilisha vizuri kwa umahiri mkubwa. Pia naipongeza sana Serikali yetu ya CCM ambayo inaongozwa na mama yetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa utekelezaji mzuri wa miradi ya maendeleo kwa njia jumuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia ujenzi wa uboreshaji wa miundombinu katika sekta ya elimu, sekta ya afya, sekta ya maji, barabara, na kadhalika, lakini hivi karibuni pia tumeshuhudia jinsi Maafisa Ugani ambavyo wamewezeshwa kwa kupewa vitendea kazi. Ni jambo jema na la kupongeza sana. Nampongeza pia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa kazi nzuri. Tumeona wakulima wamepewa matumaini makubwa sana ya kuwezeshwa kwa kupewa pembejeo kwa mfumo wa ruzuku, tunaishukuru sana Serikali yetu. Naomba nitoe ushauri kidogo tu kwa upande wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mwelekeo mzuri wa utekelezaji wa kiujumla katika sekta ya kilimo, nasi sote ni mashahidi, lakini pamoja na jitihada zote hizi, mkulima kwa mfano wa korosho anazalisha korosho, lakini utaona kwamba, korosho hii haitumii vizuri ipasavyo, pamoja na kwamba, ni mzalishaji wa korosho. Ninasema haitumii ipasavyo kwa sababu ulaji wa korosho kwa kweli kwa Mtanzania ni kidogo sana. Ukichukulia kwa mfano wa nchi kama ya India, ni ya tatu duniani kwa uzalishaji wa korosho. Inazalisha zaidi ya tani 700,000. Tanzania inazalisha zaidi ya tani 200,000, lakini ukiangalia kwa matumizi ya korosho, India inatumia korosho zaidi ya tani 300,000 wakati Tanzania sisi hatupo hata kwenye ramani ya utumiaji wa korosho. Tunatumia korosho kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutokutumia mazao ambayo anazalisha mkulima, hasa yale ya chakula, tutaona pia bei inashuka mara kwa mara na kwa kiasi kikubwa; na utakuta hata kila mwaka bei inashuka, lakini zaidi ya hapo, maisha ya mkulima yanaendelea kuwa duni. Hakuna tafsiri ya moja kwa moja ya uzalishaji wake na uboreshaji wa maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitoe ushauri kidogo tu kwamba, Serikali ifanye *integration* ya kilimo na viwanda. Nasema hivi ili tuweze kupata *multiplier effect.* Kwa mfano, suala la ajira limezungumzwa sana hapa, tuweze kupata pia mapato, tuweze ku-*regulate* pia bei. Kwa mfano, bei ya korosho; tukiwa na viwanda vyetu vya korosho kwa ajili ya kusafirishwa nje ambayo ni ghafi, itapungua na hii itasababisha mvutano; *demand and supply principle* pale, bei itapanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya korosho vipo vingi sana katika nchi yetu, vipo. Kwa mfano watu binafsi wana viwanda 39 vya korosho; lakini ukiangalia ni viwanda 20 tu ndivyo vinavyofanya kazi. Sasa hii inashangaza. Utaambiwa kwamba, vile viwanda 19 ambavyo havifanyi kazi, havina changamoto ya mtaji, wala havina changamoto yoyote. Nami naiomba Serikali iangalie na kuchunguza ni kwa

nini lile lengo la kubangua korosho ghafi 56,000 halikutekelezwa, inakuja kubanguliwa 9% tu? Inategemewa kubanguliwa korosho tani 4,900 kwa kipindi cha mwaka 2021/ 2022, tatizo ni nini hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iliangalie hili kwa umakini kwa sababu suala la viwanda tumekuwa tukilizungumzia muda mrefu, hususan, viwanda vya korosho. Tumezungumza mara tumesema vibinafsishwe, mara vianzishwe viwanda, leo wanaanzisha watu viwanda 39 viwanda 19 visifanye kazi bila sababu yoyote ambayo inaelezwa hapa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kilimo labda nimalizie tu kuiomba sasa Serikali ihimize utumiaji wa vile ambavyo tunavizalisha, hususan kwenye korosho. Korosho ina lishe, ina ubora mkubwa sana kwenye upande wa lishe, tutumie korosho Watanzania, ina manufaa makubwa sana hasa kwenye ku-*control diabetes, pressure* na magonjwa mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie kwenye upande wa afya. Tuna hospitali inajengwa kule Mtwara inakaribia kukamilika, hospitali ya rufaa ya Kanda ya Kusini ambayo iko Mitengo. Hii hospitali imekamilika kwa hatua za kwanza, lakini ina matatizo ya watumishi, inahitaji watumishi takribani 400 kwa hatua za kwanza ambapo ikikamilika itahitaji watumishi 1,200, lakini kwa sasa ina watumishi 46 tu ambapo madaktari bingwa ni wawili na madaktari wa kawaida ni watatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba maprofesa wale ambao wanastaafu na madaktari bingwa, waajiriwe angalau kwa mkataba katika hospitali hii na hata katika hospitali nyingine Tanzania, kwa sababu hili siyo tatizo la hospitali hii moja tu, ni katika maeneo mengi. Hata hivyo, naomba *retirement age* ikiwezekana iongezwe kwa sababu hili ni tatizo ili kusudi tuweze kukabiliana nalo. Mimi niko Kamati ya *LAAC* tunazunguka na tunaona shida ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongezee tu kidogo hapa kwamba, kuna tatizo pia katika hiyo hospitali. Maji yanayokwenda pale ni ya chumvi na wataalam wanasema itachukua muda mfupi sana vifaa kuharibika; na hakuna bajeti tena ya kutoa maji katika mradi mwingine. Kuna chanzo cha Mchuchu pale Mikindani kina maji baridi.

Sasa naomba Waziri wa Maji aangalie uwezekano wa kutoa maji ya baridi kutoka chanzo cha Mchuchu ili kusudi kupeleka pale kuzuia tatizo ambalo linaweza likajitokeza la kuharibika kwa vifaa katika ile hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kuomba uboreshaji wa miundombinu ya maji uende kwa kasi kubwa zaidi ya hivi ilivyo sasa, uende kwa kasi kubwa ambayo itazidi ongezeko la watu...

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** ...kwa sababu hili ni tatizo kubwa. Kwa mfano, Kisasa kule maji hatupati, tunachukua wiki mbili kupata maji.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mpakate, jiandae Mheshimiwa Anatropia na tutamalizana na Mheshimiwa Londo.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii kuchangia bajeti ya Waziri Mkuu. Kwanza napenda niishukuru Serikali kwa namna ambavyo Rais wetu amehangaika na kutupatia pesa kwa ajili ya kujenga majengo ya madarasa katika shule za sekondari. Jimbo letu tulipata takribani madarasa 51 ambayo yamewezesha shule zile kuonekana kama mpya, lakini

pamoja na upya huo, kuna changamoto kwenye shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyozungumza mwenzangu Mheshimiwa Hassan Kingu, shule zetu zimechakaa. Pamoja na kuchakaa, watoto ni wengi sana. Nitatoa mfano mmoja kwenye Kata yangu ya Mtina ambayo ina shule saba. Tunahitaji madarasa 72. Shule ya Tupendane ina madarasa matano, lakini tunahitaji nane, ambayo yamepungua ni matatu. Shule ya Angalia ina madarasa nane, inahitaji madarasa 20, upungufu ni madarasa 12. Shule ya Azimio kuna madarasa saba, tunahitaji madarasa 21 na upungufu ni madarasa 14. Shule ya Mtina ina madarasa nane, tunahitaji madarasa 23 na upungufu ni madarasa15. Shule ya Semeni ina madarasa saba, yanahitajika madarasa 23 na upungufu ni madarsa 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utaona mfano halisi, tumetoa tatizo kwenye shule za sekondari, lakini shule za msingi ni changamoto kubwa sana. Huo mfano ni kwenye kata moja tu kati ya kata 15. Kwa hiyo, tunahitaji zaidi ya madarasa 300 kwenye shule za msingi. Naomba sana tumwombe mama kama alivyofanya kwenye shule za sekondari, ahangaike atutafute pesa kwa ajili ya madarsa kwenye shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na madarasa hayo, tuna upungufu mkubwa wa walimu. Kwenye shule za sekondari tumejenga madarasa mengi, lakini walimu hakuna. Pia katika sekta hiyo tunashukuru tumetangaziwa kutakuwa na ajira ya wafanyakazi 32,000, LAKINI kuna changamoto kubwa ambayo imezungumzwa na mwenzangu Mbunge wa Liwale, kwamba tunapata watumishi wengi lakini baada ya muda fulani wote wanahama kwa maana kwamba, maeneo yote ya Kusini yanakuwa ni sehemu za kuchukulia *check number.* Akishapata *permanent employment,* maana yake anahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mapendekezo ambayo kidogo yanaweza yakatusaidia kupunguza hizi

*movements* za wafanyakazi katika maeneo mbalimbali. Mnapopanga hao watumishi au mnavyoajiri, basi tuangalie kiukanda au kila Halmashauri au wilaya ipewe idadi ya kuajiri hawa wafanyakazi kulingana na mahitaji ambayo yapo. Tukifanya hivyo kila mmoja ataendelea kukaa katika maeneo yake ambayo ameajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kumtoa mtu Kagera kumpeleka Tunduru inakuwa ni mtihani mkubwa sana. Japo ni Tanzania, lakini mazingira yanatofautiana. Kwa hiyo, tunaomba sana kwenye ajira hii ya 32,000 Wizara ya Utumishi ijitahidi kugawa idadi hii katika maeneo mbalimbali kulingana na wilaya kwa sababu, huko vijijini kote tuna wasomi wamejaa; tuna walimu, watu wa afya, Maafisa Ugani na kada mbalimbali, *degree* zimejaa siku hizi vijijini. Sasa ajira hii tukiigawa kulingana na wilaya au Halmashauri, basi kila wilaya tutapata angalau wafanyakazi kadhaa ambao wataweza kufanya kazi katika maeneo hayo yanayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi inavyoonekana, watumishi wengi wanatoka katika sehemu moja, maeneo mengine kunakuwa watumishi hawapo, sasa tunakuwa tunawanyima haki ya kuendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilipenda niongelee katika bajeti hii ni suala la kilimo. Kwetu Kusini, mfumo wa stakabadhi ghalani kwa kweli, umekuwa ni mkombozi mkubwa katika kumkomboa mkulima. Kwenye korosho tumefanikiwa, kwenye ufuta tumefanikiwa na sasa tunaomba Serikali, kuna maeneo tunateleza kwenye mazao mchanganyiko. Kwa mfano, choroko, uzalishaji ni mdogo sana. Naamini kama tungeacha kununua choroko kwa mtindo holela, mapato yangekuwa ni makubwa kwa wakulima, lakini tunapopeleka choroko kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani na choroko zenyewe ni chache, kwa kweli inaleta kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo haya mazao madogo madogo basi tuyaangalie kiukanda. Kama mbaazi, stakabadhi ghalani inafanyika Tunduru, basi hata

wenzetu wa Mtwara, Nanyumbu na Masasi wafanye stakabadhi ghalani. Hii inasababisha mbaazi za Tunduru kwenda Nanyumbu na kuinyima mapato Halmashauri ya Tunduru. Kwa hiyo, stakabadhi kwa sababu ni sheria, naamini kwenye maeneo ambayo wamekubali hii sheria, iendelee kutumika basi kwenye mazao yote, itumike kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani ili kila mmoja aone wanakwenda sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa sana kulizungumzia ni tembo. Naomba sana, Waziri wa Maliasili simwoni; Tunduru tembo wamekuwa wengi sasa. Kipindi hiki ni cha mavuno ya wakulima, tembo saa hizi ndiyo wanashamiri, watu hawalali.

Tunaiomba Serikali kama walivyotoa ahadi siku za nyuma, pelekeni vikosi vya dharura katika maeneo ya Tunduru, tuna shida sana Mbati, leo hii wameingia kwenye nyumba za watu. Tuna shida Mpanji, Misyaje, Marumba, Imani na Kazamoyo. Tembo wamekuwa ni wengi na wale wanatokea sehemu ya Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iangalie kwa jicho la huruma, mazao ya wananchi wa Tunduru yanateketea kwa tembo, yanaliwa. Naomba tupeleke askari wa dharura ili waweze kudhibiti wale tembo wasiendelee kudhuru mazao ya wananchi na wananchi wenyewe wanadhurika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la afya. Kwenye Jimbo langu kuna vituo vya afya vitatu. Naishukuru Serikali, Halmashauri ya Wilaya inajenga kituo kingine pale Nalasi na Serikali kupitia fedha zilizotolewa na Mheshimiwa Rais, tumepata shilingi milioni 250. Tunajenga kituo kingine cha afya katika Tarafa ya Lukumbule, lakini tuna kituo cha afya cha muda mrefu, kimejengwa tangu miaka ya 1980, majengo yake yamechakaa, hakuna *operation* inayofanyika, hakuna chochote zaidi ya yale majengo ambayo yapo mpaka sasa. Naomba sana Halmashauri... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa hii nafasi ya kuchangia katika Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukiangalia leo changamoto ya uchumi tuliyonayo pengine tusingekuwa tumefikia kwa kiwango hiki kama tungeweza kuwa tumewekeza vya kutosha katika sekta mbalimbali ambazo ni dhahiri zingeweza kuleta matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea sekta ya mifugo nikiendeleza alikomalizia mwenzangu mama Kaboyoka. Mama Kaboyoka ameongelea takwimu zinaonyesha kwamba idadi ya ng'ombe na mbuzi na kondoo wameongezeka na mimi nitasema kwa mujibu wa takwimu zenu. Mnasema ng'ombe leo tuna takriban milioni 33, tunakuja mbuzi milioni 25 mpaka 28, tunakuja kondoo na vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo inaonyesha kwamba sekta ya mifugo inakua kama takwimu ni za kweli, lakini ukiangalia ukuaji wa sekta ya mifugo unachangiaje kwenye pato la Taifa wamesema mifugo inachangia kwa 7% mpaka 7.4% kwa miaka miwili mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona kwamba hicho ni kiwango kidogo ukilinganisha kwamba ni watu wengi wanaweza kushiriki na kujiajiri katika ufugaji. Ufugaji leo tunaouongelea na kwa kiwango kikubwa katika nchi yetu ni ufugaji wa asili, ufugaji wa asili ambao ungeweza kama ukiwekezwa vizuri kama alivyoeleza mama yangu unaweza ukaleta tija katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sisi Tanzania ni wa pili katika mifugo nyuma ya Ethiopia na mmejinasibu kwa takwimu kwamba leo tunaweza kusindika tunapeleka mpaka Uarabuni na maeneo mengine. Hata hivyo, bado hatujafanya vizuri, nguvu kubwa tumeiwekeza kwenye maziwa lakini na bidhaa ya ng'ombe, tumesahau maziwa na nyama. Tumesahau kwamba bado kuna *asset* kubwa ambayo inatoka kwenye ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kila mtu anaenda kununua kitu dukani kama ni *bag,* kama ni kiatu, kama ni *hand bag* chochote atatamani kiwe cha ngozi na ataanza kuangalia *quality* ya ngozi kumbe kuna fursa kubwa sana kwenye ngozi kama tukiwekeza vizuri. Nimepitia takwimu nimeona tunaeleza kwamba tukiwa na mifugo zaidi ya milioni 33 kwa takwimu za mwaka huu zinaonyesha mmeweza kupata *piece* za ngozi zaidi ya milioni 13. Katika *piece* zaidi milioni 13 hizo *piece* zimeweza kuleta zaidi au zikiuzwa zinaweza kuleta zaidi ya bilioni 28. Kwa mwaka uliopita ziko *piece* milioni 11, lakini katika *piece* za ngozi milioni 11 inaonekana zilikuwa zimeshauzwa zaidi au chini ya milioni 1.5. Kwa hiyo unaweza ukaona kwamba ngozi ambayo inakusanywa haiuziki na hapo ndiyo nataka nieleze vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya mifugo ya 2006 inaongelea nini kuhusu bidhaa za ngozi? Bidhaa za ngozi duniani na nchi ikishafahamika inatoa ngozi nzuri *automatic* tutapata bei nzuri. Nchi kama Ethiopia leo nimesoma mnaonyesha kwamba mnauza ngozi Ethiopia lakini kwa nini mnauza ngozi Ethiopia kwa sababu sisi hatuna *repetition* ya ku-*trade* ngozi duniani. *Repetition* ya ngozi yetu ni duni na kwa sababu wanajua ni duni na uduni huo umetokana na kufuga vibaya. Kuna mtu amefanya *research* anaitwa Mahmood na wenzake, ameeleza kwamba zaidi ya asilimia 60 ya ngozi inaharibikia kwenye machinjio, kwamba ng'ombe anaweza akawa ametunzwa vizuri *despite challenges* lakini wanavyoingia kwenye machinjio zaidi ya asilimia 60 ya ngozi inakuwa imeharibika. Akaenda mbali zaidi akasema kwa nyama inayokuwa *consumed* Tanzania ni 10% tu ya nyama ambazo zinachinjwa katika mabucha sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ngozi leo zipo *tans* and *tans* na nimesoma taarifa ya wafanyabiashara wanasema wana tani zaidi ya 3,000 *tans* zipo zimekosa soko kwa sababu hazina ubora na hivyo nitaongelea *specific* sera ambayo inaendelea leo mtaani kwamba tuweze kuweka alama ng'ombe, Serikali inabandika alama kwenye ng'ombe kwa kutumia hata *traditional method* ile ngozi inabandikwa na pasi ngozi inaunguzwa kwa hiyo inapoteza *value.* Kwa hiyo tunarudi kwa Mahmood alivyosema kwamba 60% ya ngozi inaharibikia kwenye mabucha mbali na sababu nyingine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikasoma taarifa ya Wizara inasema kwamba, wameweza kupeleka visu 100 nadhani *something like* 116 kwenye mabucha maalum, hivi visu vya uchinjaji 116 vinasaidiaje katika ng'ombe au mabucha au wazalishaji wa nyama katika nchi hii. *Which means* hatujawekeza vya kutosha na hatuwezi kupata faida ya ngozi ambayo kwa kiwango kikubwa ngozi ndiyo bidhaa nzuri duniani. Wafugaji wanaendelea, viwanda au wawekezaji wa kwenye *industry* ya *lather* nchini wanalalamika, mazingira mabovu ya uwekezaji, wanalalamika kukosa *incentive,* wanalalamikia pia ubovu wa ngozi ambayo tunazalisha nchini. Hapa anaendelea ku-*capitalize* kwamba ni lazima sera ieleze bayana ni kwa kiwango gani tunaenda kupunguza ubovu wa ngozi inayopatikana ili tuweze kupata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutajinasibu kwamba tuna ng'ombe wengi tunajinasibu tunazalisha nyama ya kutosha, lakini hebu tu-*focus* kwenye ngozi pia. Kama tukifanya vizuri kwenye *finished product* za ngozi na siyo tu viwanda tulivyonavyo leo *by the way* tulikuwa na viwanda mpaka 11, leo tuna viwanda kama vitatu au vine, lakini siyo tu kwamba vinazalisha *finished goods* bali vinakuwa na vyenyewe ni kama vina *export raw material,* vinachakata kidogo halafu vinaenda kuuza kwenye nchi za wenzetu pamoja na Burundi. Hivi leo Burundi ni wa kununua ngozi Tanzania? Leo Burundi ndiyo wanapaswa kuonekana wanazalisha ngozi nafuu ukilinganisha na Tanzania? *I think something is wrong*

*somewhere* na hiyo ndiyo nataka Ofisi ya Waziri Mkuu itueleze ni mkakati gani mahsusi uliopo kupunguza ubovu wa ngozi ambayo imekuwa ikizalishwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hiyo tu, tunataka tuambie hiyo sera leo tuliyonayo ya mifugo ya 2006, ni lini itakuwa *reviewed* ili iendane na wakati nimejipa *homework,* nikasoma sea ya mifugo ya Kenya, nikasoma sera ya mifugo ya Ethiopia, nikaone wenzetu *so far* wanajua wanachokifanya kwenye *industry.* Nadhani Ofisi ya Waziri Mkuu ni wakati umefika tuweze ku-*review* tuone tunaweza kufanya vizuri kwa kiwango gani zaidi kwenye soko la ngozi duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hiyo tu ambayo naweza nikaeleza bidhaa za ngozi ambayo nimekuwa nikizieleza au nimekuwa nikieleza hapa ikikabiliwa na changamoto ya kuwa mbovu bado pia kuna ujanja ujanja hapa katikati, kwamba wanaodili na bidhaa za ngozi wanakuwa na madalali ambao wanalalia hata wao wenyewe wafanyabiashara wanaonunua ngozi, *which means* tumetengeneza *middle men* hapa katikati. Wafanyabiashara wa ngozi au wa viwanda vya ngozi wamesema kwamba ngozi yenyewe inayozalishwa ngozi nzima ni chini ya 15% ambayo ni *first grade* na *second grade*.

Kwa hiyo, naomba nitoe wito kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inasimamia sera itusaidie kama ambavyo nguvu kubwa inaelekezwa kwenye maziwa na nyama, tuone mabadiliko kwenye ngozi pia, ndiyo tutaweza kupata tulichokuwa tunataraji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuongelea changamoto leo ambayo tunapitia ya kupanda kwa bei ya mafuta. Kupanda kwa bei ya mafuta ya petrol na mafuta ya kula yatakuwa na *impact* kwenye uchumi baadaye...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Londa.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi pia ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu. Awali ya yote naomba nianze kwa kumpongeza Rais wetu mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Serikali yake kwa kazi kubwa ambayo inafanywa hasa katika Majimbo ya pembezoni kama Mikumi. Kuna kazi kubwa inaendelea kuna mambo mengi ambayo yalikuwa yameshindikana lakini sasa yanafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Ruhembe kuna daraja kubwa ambalo linaenda kuunganisha Kata za Ruhembe, Kidodi na Ruaha zinaenda kupunguza umbali wa wananchi na wakulima kutoka kilometa 30 mpaka kilomita mbili. Pia kuna kata inaitwa Vidunda ambayo ilishatengwa na haikuwa na mawasiliano ya barabara lakini sasa hivi inaenda kuwa na mawasiliano ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kata za pembezoni kama Malolo, kama Uleling'ombe, Kilangali hata Kisanga ambazo sasa hivi zinaenda kuunganishwa na barabara kuu lakini pia uzalishaji wake wa bidhaa za kilimo unaenda kuunganishwa na masoko. Jitihada zote hizi zinaendana pamoja na uboreshaji mkubwa wa vituo vya afya, shule na maeneo mengine ya huduma za kijamii. Tafsiri yake ni kwamba huko tunakoenda wananchi wengi watabakia vijijini na *migration* kutoka vijijini kuja mjini itaendelea kupungua kwa sababu ya uboreshwaji wa miundombinu lakini pia huduma za kijamii katika kata na vijiji vya pembezoni. Maana yake nini tunaenda kushuhudia rural *transformation* ambayo haijawahi kuonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali hapa je ni kwamba elimu inayotolewa na vyuo vyetu inaakisi maendeleo haya ambayo yanaendelea vijijini? Kozi ambazo zinatolewa na vyuo vyetu zinaandaa vijana wetu kurudi vijijini na kwenda

kutumikia maisha katika kata na maeneo ya pembezoni? Ninapoona tunaendelea ku-*admit* wanafunzi katika vyuo vyetu vikuu katika kozi ambazo hazitoi ajira, sioni kama kuna *seriousness* katika ku-*transform* vijiji vyetu na hasa katika kata za pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye hili kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu inasimamia sera, lakini pia ajira vijana na hata walemavu, ningependa sana kuona uratibu katika huu Mfuko 10% za wanawake, vijana na walemavu za TAMISEMI zinaratibiwa vizuri kuwa sehemu ya kutoa majibu ya changamoto katika maeneo yetu ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali yetu, mwaka 2014 ilifanya *study* ya kuangalia kiwango cha ujuzi wa nguvu kazi na katika *study* hiyo tulikuwa tumeona kwamba lengo ilikuwa ni kuangalia namna ya kujenga uwezo unaohitajika katika soko la ajira, watu kujiajiri na kuajiriwa. Tuliona matokeo ya utafiti ule, asilimia 79.9 ya nguvu kazi ilikuwa chini ya kiwango cha ujuzi, kwa maana *low skilled*, 16.6% ni *semi skilled* kwa maana kiwango cha ujuzi katika soko la ajira kilikuwa ni kiwango cha kati. Tuliona 3.6% ya nguvu kazi katika ajira na ujuzi wake ni chini ya 3.6% ambao walikuwa ni *higher skilled* na ndiyo matokeo yake Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali ikaja na mikakati minne ya kukuza ujuzi kwa maana utarajali *internship*, lakini pia urasimishaji wa ujuzi ambao umepatikana nje ya mfumo kukuza ujuzi wa wafanyakazi na wale waliojiajiri lakini pia uanagenzi kwa maana ya *friendship*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizi *program* zilikuwa ni muhimu sana na kwa kweli kwenye baadhi ya maeneo tumeona matokeo chanya. Ombi langu ni vyema sasa tukafanya *study* kuona ni jinsi gani tunaenda ku-*transform* hizi *program* nne kuona kwamba zinaenda kutatua tatizo la ujuzi kwenye nguvu kazi ya vijana wetu katika soko la ajira. Hapa tunaweza tukajifunza kutoka katika Nchi kama za Ujerumani ambazo zilifanikiwa sana, Nchi ya Finland, Korea lakini hata China juzi hapa tuliona wameamua kubadilisha Vyuo vyao Vikuu zaidi ya 600 kuwa *polytechnics* na

*vocational* kwa ajili ya kufunza ama kutoa ujuzi kwa vijana wao ili waende kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hili tuna la kujifunza, kama wenzetu wana Vyuo Vikuu 600 na wameona kabisa *module* ya elimu wanayoitoa pale ni nadharia zaidi, haiendi kujibu changamoto ya ajira, wamebadilisha kwenda kutoa ujuzi, kuna jambo kubwa la kujifunza kwao. Je, tunavyobadilisha vyuo vyetu vya kati kwenda kuwa Vyuo Vikuu na kutoa *degree* za nadharia, tunapotoa *graduates* 5000, 10,000 ambao wamesomea *procurement* wanaenda kuajiriwa na nani wanaenda kufanya kazi wapi hawa? Tunapoenda kutoa ajira ama *graduates* 10,000 wanasheria. Je, wahalifu wameongezeka kwenye hii nchi? Mahakama zimeongezeka? Shughuli zao ni nini wanaenda kuwaajiri wapi, je, kuna mkakati wa kuenda ku-*absorb* hili kundi kubwa ambalo lina *graduate* kutoka kwenye vyuo vyetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mambo haya tukiyatafakari kwa kina, tunaona kwamba kuna umuhimu wa ku-*review* elimu tunayoitoa kwenda kujibu changamoto za ajira zetu. *Study* hii ambayo imefanyika 2017 leo ni 2022 ni miaka mitano utekelezaji wake umefikia wapi kuna umuhimu wa kuifanyia tena *study* ili kujua je, asilimia hizi ambazo zilitajwa 2014 zimebakia kama zilivyo ama vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu inashughulikia pia majanga, majanga mengi ukiondoa yale ya kiasili kama matetemeko na mafuriko, mengi tunaweza tukayadhibiti. Migogoro ya wakulima na wafugaji ni moja ya majanga ya Taifa hili ambayo tunaweza tukayadhibiti kama tunajipanga. Vyuo Vyetu vya Ufundi vyuo vyetu vya kati, vinaweza vikawa sehemu ya suluhisho la changamoto hizi kama vitaenda kutoa elimu ama ujuzi kwenye kilimo, kwenye ujenzi, kwenye miundombinu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili ningeomba kusisitiza vyuo vya ufundi na vyuo vya kati vipewe jicho la kipekee. Tuna sheria ambayo 4% ya *private sector* inatoka

ama inalipwa kwenye *skill development levy*. Bunge lako hatujui zinatumikaje ni vizuri tukajua kwa sababu lengo la *skill development levy* ni kuendeleza ujuzi wa nguvu kazi yetu. Je, fedha hizi zinaenda kwenye lengo lililokusudiwa na sheria? Tunajua 2% inaenda kwenye mikopo ya *higher learning,* lakini hizi 2% zinatumikaje katika kujenga na kuendeleza ujuzi wa vijana wetu? Ni swali ambalo tunatakiwa kulijibu na katika jibu lake linaweza kutupa changamoto ambazo tunazo lakini majibu ya kukosekana kwa ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili ninapozungumzia 2% ya *skills development levy,* ni zaidi ya shilingi bilioni 150. Bilioni 150 inaweza ikatumika sehemu kwa ajili ya kuwanunulia vifaa vijana 90,000 ambao wanasoma katika vyuo vyetu vya *VETA,* wakatoka pale na vifaa vya kuanzia kazi, wakajiajiri na wakaajiri vijana wenzao na sisi tukapunguza mzigo wa vijana wetu kukosa ajira katika soko la ajira. Katika hili tunahitaji uratibu taasisi zetu za *SIDO, VETA, TIRDO* wana wajibu wa moja kwa moja ku-*incubate* vijana ambao wana ari ya kujiajiri na kuajiri wengine. Changamoto ya *bureaucracy* katika leseni na vitu vingine imekuwa ni zuio kwa vijana wengi kujiajiri. Sasa taasisi hizi zinapaswa kubeba jukumu la kulea vijana wajasiriamali ambao wanatumia ujuzi wao ambao wameupata kwenye vyuo vyetu vya ufundi kujiajiri na katika kuwalea wanapaswa kuangalia hizi *compliance* kama *TBS, OSHA*, *Weight and Measures* wanazi-*meet* katika kipindi cha uangalizi. Hilo linaweza likatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho la…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge orodha ya Wabunge wote imekwisha na sasa nina tangazo la wageni

wa Wabunge. Wageni wanne wa Mheshimiwa Maimuna Pathan ambao ni ndugu zake kutoka Jiji la Dar es Salaam ndugu Agnes Kapinga, ndugu Zainab Thabit, Maimuna Pathan na Mary Mushi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kama mtakumbuka leo asubuhi kulikuwa na mchango wa Mheshimiwa Gambo na hatimaye Mheshimiwa Asia akaomba taarifa, akampa taarifa Mheshimiwa Gambo na majibu ya Mheshimiwa Gambo kama mlivyoyasikia, lakini Mheshimiwa Shangazi akaomba mwongozo. Nikamwambia Mheshimiwa Shangazi tutarudi kwenye *Hansard* kutazama maneno halisi yaliyosemwa ili tujiridhishe na majibu ambayo tukiyatoa.

Mwongozo wa Spika uliombwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi Mbunge kuhusu kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Mrisho Gambo baada ya kupewa taarifa na Mheshimiwa Asia Hamlaga.

Waheshimiwa Wabunge leo tarehe 11 Aprili, 2022 katika kikao cha Nane cha Mkutano wa Saba wa Bunge, Mkutano wa Bajeti niliombwa Mwongozo na Mheshimiwa Rashid Shangazi kuhusu kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Mrisho Gambo, baada ya kupewa taarifa na Mheshimiwa Asia Hamlaga.

**WABUNGE FULANI:** Ni Mheshimiwa Halamga.

**NAIBU SPIKA:** Hamlanga samahani.

**WABUNGE FULANI:** Halamga.

**NAIBU SPIKA:** Nani?

**WABUNGE FULANI:** Halamga.

**NAIBU SPIKA:** Sawa, haya Halamga, hivyo hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge wakati Mheshimiwa Mrisho Gambo akichangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na Kazi, Vijana na Ajira na Watu Wenye Ulemavu mchango wake ulijikita katika sekta ya madini mojawapo eneo alilolichangia ni soko la madini ya *tanzanite*. Kwa ufupi alitoa takwimu za mauzo ya *tanzanite* kuanzia mwaka 2019 mpaka 2020 wakati *tanzanite* ilipokuwa ikiuzwa katika soko la madini la Arusha kama madini mengine.

Alieleza kuwa Serikali iliweza kukusanya kodi hadi kufikia kiasi cha shilingi bilioni 1.3 na kwamba baada ya Soko la *Tanzanite* kuhamishiwa Mererani kati ya Julai, 2021 hadi Januari, 2022 Serikali ilikusanya kodi kati ya shilingi milioni 339 tu kutoka shilingi bilioni 1.3 iliyokuwa ikipata wakati ilipokuwa ikiuzwa katika soko la madini la Arusha. Hivyo alieleza kwamba uamuzi wa kuhamisha Soko la *Tanzanite* Mererani kutoka Arusha unatia hasara Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Mbunge akiendelea na mchango wake huo ndipo Mheshimiwa Asia aliposimama na kumpa taarifa akieleza kwa ufupi kuwa Soko la *Tanzanite* lilihamishiwa katika Mji wa Mererani, Mkoa wa Manyara ambako ndipo madini ya *tanzanite* yanapochimbwa na kwamba takwimu zinaonesha kuwa Serikali imeweza kuongeza kipato tangu soko liliporejeshwa Mererani. Hivyo alimaliza kwa kumkaribisha Mheshimiwa Mrisho Gambo kuja Mererani kuwekeza katika Soko la madini ya *Tanzanite*.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutolewa taarifa hiyo, nilimtaka Mheshimiwa Mrisho Gambo kuipokea ambapo alijibu kuwa nanukuu: "Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri kwamba Wabunge watafute hoja za kuchangia, siyo tunadandia tu ili mradi tuonekane na wananchi wetu, hapa tunaongelea mambo serious, kwa hiyo tupokee taarifa yake".

Waheshimiwa Wabunge, majibu haya ndiyo sababu iliyomfanya Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge kuomba Mwongozo wa Spika na chini ya Kanuni ya 76 ya Kanuni za

Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020. Mheshimiwa Shangazi alisema kwamba hayo maneno ni ya kejeli na dharau. Nilipokea mwongozo huo na kuamua kwamba nitautafakari na kupitia *Hansard* na baada ya hapo nitatoa mwongozo kama nilivyosoma.

Mwongozo wangu ni huu, Mbunge yeyote anaruhusiwa kwa idhini ya Spika kutoa taarifa kwa Mbunge mwingine anayekuwa akisema au akichangia hoja, hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 77 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Mbunge anayepewa taarifa ataulizwa na Spika kama anaikubali au anaikataa taarifa hiyo. Kwa mantiki ya kanuni hii Mbunge akipewa taarifa atasema tu kama anaikubali au anaikataa taarifa na kisha kuendelea na mchango wake.

Waheshimiwa Wabunge, kauli ya Mheshimiwa Mrisho Gambo baada ya kupewa taarifa hiyo kwamba Wabunge watafute hoja za kuchangia siyo tunadandia tu ili mradi tuonekane na wananchi wetu si kauli ya kibunge na ni lugha ya kuudhi na ya kumdhalilisha Mbunge aliyeomba taarifa. Kanuni 71(1)(j) Kanuni ya Kudumu za Bunge inaeleza kuwa Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Hivyo basi, natoa mwongozo wangu kwa maneno aliyotumia Mheshimiwa Mrisho Gambo hayaruhusiwi kwa sababu siyo lugha ya kibunge. Nichukue fursa hii kuwataka Waheshimiwa Wabunge, kuzingatia na kutumia lugha ya kibunge ili kuepuka kuvunja kanuni zetu. Huo ndiyo mwongozo wangu.

Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 12 Aprili, 2022, Saa 3.00 Asubuhi)*